# HOTUBA YA WAZIRI WA KILIMO, MHESHIMIWA DANIEL GODFREY CHONGOLO (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA KILIMO KWA MWAKA 2026/2027



MHE. DANIEL GODFREY CHONGOLO (MB)
***Waziri***



MHE. DAVID ERNEST SILINDE (MB)
***Naibu Waziri***



BW. GERALD GEOFREY MWELI
***Katibu Mkuu***



MHA. ATHUMANI J. KILUNDUMYA
***Naibu Katibu Mkuu (Umwagiliaji na Zana za Kilimo)***



PROF. PETER L.M. MSOFFE
***Naibu Katibu Mkuu (Maendeleo ya Mazao na Usalama wa Chakula)***

# YALIYOMO


Dira, Dhima, Majukumu na Malengo ya Wizara.. xvi

Dira ........................................................................ xvi

Dhima........................................................................ xvi

Majukumu .................................................................. xvi

Malengo .................................................................... xvii

1 UTANGULIZI.........................................................1

2 HALI YA KILIMO KATIKA MWAKA 2025 .....12

2.1 Ukuaji na Mchango katika Pato la Taifa.....12

2.2 Hali ya Chakula ..............................................12

3 UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2025/2026 ...........................................14

3.1 Makusanyo ya Maduhuli ................................14

3.2 Fedha Zilizoidhinishwa kwa Fungu 43, 24 na 05 ...............................................................14

4 UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2025/2026 ...............................16

4.1 Kuongeza Uzalishaji na Tija ...........................17

4.1.1 Utafiti wa Mbegu..............................................20

4.1.2 Uzalishaji na Usambazaji wa Mbegu na Miche Bora kwa Mpango wa Ruzuku kwa baadhi ya Mazao ...............................................28

4.1.3 Uwekezaji kwenye Utoaji wa Ruzuku ya Mbolea na Viuatilifu ........................................37

4.1.4 Usajili wa Wakulima na Urasimishaji wa Shughuli za Kilimo ...........................................45

4.1.5 Kuweka kwenye Ujuzi kwa Wataalam wa Ndani ............................................................47

4.1.6 Uwekezaji kwenye Huduma za Ugani ..........47

4.1.7 Kupima Afya ya Udongo kwa Wakulima Wadogo na Wakubwa......................................52

4.1.8 Uendelezaji wa Kilimo cha Umwagiliaji .......54

4.1.9 Uanzishaji wa Vituo vya kutoa Huduma na Ununuzi wa Zana za Kilimo......................60

4.1.10 Kuendeleza Shoroba za Kilimo na Uzalishaji............................................................64

4.2 Kuongeza Ajira zenye Staha na Ushiriki wa Vijana na Wanawake kwenye Kilimo.....97

4.2.1 Kuwezesha Upatikanaji wa Ardhi ya Kilimo na Uanzishaji wa Mashamba Makubwa ya Pamoja (BBT – Mashamba).............................97

4.2.2 Kuwezesha Uendelezaji wa Programu ya BBT Ngazi ya Halmashauri .............................99

4.2.3 Kuwezesha Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji kwa Wakulima wadogo (BBT visima) 100

4.2.4 Kuwezesha Upatikanaji wa Mikopo kwa Vijana na Wanawake (BBT mitaji)...............101

4.2.5 Kuwezesha Vijana na Wanawake Kuongeza Thamani ya Mazao ........................................102

4.2.6 Kuwezesha Vijana na Wanawake kutoa Huduma za Ugani (BBT Ugani) ....................103

4.3 Kuimarisha Usalama wa Chakula na Lishe ..................................................................104

4.3.1 Uwekezaji kwenye Miundombinu ya Uhifadhi ili kufikia Uwezo wa Kuhifadhi tani 3,000,000 ifikapo Mwaka 2030...........104

4.3.2 Kuiongezea NFRA Uwezo wa Kununua Mazao ya Wakulima ili Kuongeza Hifadhi 105

4.3.3 Kuhamasisha Matumizi ya Mazao yaliyoongezewa Virutubishi ili Kukabiliana na Matatizo ya Lishe Nchini.........................106

4.4 Kuimarisha Upatikanaji wa Masoko, Mitaji na Mauzo ya Mazao Nje ya Nchi ..................108

4.4.1 Kujenga Miundombinu ya Masoko ya Mazao ya Kilimo kwa ajili ya Wakulima katika Halmashauri mbalimbali Nchini .................108

4.4.2 Kuimarisha Uongezaji Thamani kwa Kushirikisha Sekta Binafsi...........................110

4.4.3 Kuongeza Mauzo ya Mazao ya Kilimo Ndani na Nje ya Nchi.....................................111

4.4.4 Kuimarisha Upatikanaji wa Mitaji .............114

4.4.5 Kuziwezesha Maabara za Serikali ziweze kufikia Viwango vya Ubora vinavyotakiwa Kimataif.................................115

4.5 Kuimarisha Maendeleo ya Ushirika ...........117

4.5.1 Kuimarisha Mifumo ya Kidijiti kwenye Vyama vya Ushirika na Mamlaka za Usimamizi ........................................................117

4.5.2 Kuimarisha Usimamizi na Udhibiti wa Vyama vya Ushirika.......................................118

4.5.3 Kuhamasisha Vyama vya Ushirika Kujiendesha Kibiashara na Kuviwezesha kupata Mitaji...................................................120

4.5.4 Kuhamasisha Ushirika kwenye Sekta Mbalimbali na Makundi Maalum................122

4.6 Kuimarisha Matumizi ya Mifumo ya TEHAMA Katika Uendelezaji wa Sekta ya Kilimo ................................................................124

4.6.1 Kuwekeza kwenye Matumizi ya Mifumo ya Kidijiti katika Sekta ya Kilimo................124

4.6.2 Kuimarisha Mifumo ya Kidijiti itakayowezesha Upatikanaji wa Taarifa Sahihi kwa Wakati..........................................127

5 MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2026/2027..........................................................133

5.1 Kuongeza Tija na Uzalishaji..........................140

5.1.1 Utafiti wa  Kilimo.............................................140

5.1.2 Uzalishaji na Usambazaji wa Mbegu Bora na Miche 145

Uzalishaji wa Mbegu..................................................145

5.1.3 Utoaji wa Ruzuku ya Mbolea, Mbegu na Viuatilifu 151

5.1.4 Usajili wa Wakulima na Urasimishaji wa Shughuli za Kilimo ....................................155

5.1.5 Kuimarisha Huduma za Ugani.....................156

5.1.6 Kuanzisha Mashamba Makubwa ya Pamoja na Kupima Afya ya Udongo ...........159

5.1.7 Uendelezaji wa Kilimo cha Umwagiliaji .....160

5.1.8 Uanzishaji wa Vituo vya kutoa Huduma na Ununuzi wa Zana za Kilimo ....................162

5.2 Kuchangia Kuongeza Ajira zenye Staha na Ushiriki wa Vijana na Wanawake kwenye Kilimo....................................................184

5.2.1 Kuwezesha Uendelezaji wa Programu ya BBT Ngazi ya Halmashauri ...........................184

5.2.2 Kuwezesha Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji kwa Wakulima Wadogo (BBT Visima) ...........................................................186

5.2.3 Kuwezesha Upatikanaji wa Mikopo kwa Vijana na Wanawake (BBT Mitaji)...............186

5.2.4 Kuwezesha Vijana na Wanawake Kuongeza Thamani ya Mazao .......................187

5.2.5 Kuwezesha Vijana na Wanawake kutoa Huduma za Ugani (BBT Ugani)....................187

5.3 Kuimarisha Usalama wa Chakula na Lishe ..............................................................188

5.3.1 Uwekezaji kwenye Miundombinu ya Uhifadhi ili Kufikia Uwezo wa Kuhifadhi tani 3,000,000 ifikapo Mwaka 2030 ........... 188

5.3.2 Kuiongezea NFRA Uwezo wa Kununua Mazao ya Wakulima ili Kuongeza Hifadhi ........... 189

5.3.3 Kuhamasisha Matumizi ya Mazao yaliyoongezewa Virutubishi (Biofortified) ili Kukabiliana na Matatizo ya Lishe Nchini ........ 190

5.4 Kuimarisha Upatikanaji wa Masoko, Mitaji na Uongezaji Thamani ........ 191

5.4.1 Kujenga Miundombinu ya Masoko ya Mazao ya Kilimo ........ 192

5.4.2 Kuongeza Mauzo ya Mazao ya Kilimo Ndani na Nje ya Nchi ........ 193

5.4.3 Kuimarisha Uongezaji Thamani kwa Kushirikisha Sekta Binafsi ........ 194

5.4.4 Kuimarisha Upatikanaji wa Mitaji ........ 195

5.4.5 Kuziwezesha Maabara za Kilimo Kufikia Viwango vya Ubora Vinavyotakiwa Kimataifa ........ 196

5.5 Kuimarisha Maendeleo ya Ushirika ........ 197

5.5.1 Kuimarisha Ukaguzi na Usimamizi wa Uendeshaji wa Vyama vya Ushirika ........ 197

5.5.2 Kuhamasisha Vyama vya Ushirika Kujiendesha Kibiashara na Kuviwezesha Kupata Mitaji ........ 198

5.5.3 Kuhamasisha Ushirika kwenye Sekta mbalimbali na Makundi Maalum ....................200

5.6 Kuimarisha Matumizi ya Mifumo ya TEHAMA Katika Uendelezaji wa Sekta ya Kilimo....................201

5.6.1 Kuimarisha Mifumo ya Kidijiti itakayowezesha Upatikanaji wa Taarifa Sahihi kwa Wakati ....................202

5.6.2 Kuwekeza kwenye Matumizi ya Mifumo ya Kidijiti katika Sekta ya Kilimo ....................203

6 MAOMBI YA FEDHA MWAKA 2026/2027 211

6.1 Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli.....211

6.2 Fedha za Matumizi kwa Mafungu yote......212

6.2.1 Fedha kwa Fungu 43 ....................212

6.2.2 Fedha kwa Fungu 05 ....................212

6.2.3 Fedha kwa Fungu 24 ....................213

## MAJEDWALI

Jedwali Na. 1: Uzalishaji wa Mazao ya Chakula kwa Msimu 2024/2025 (Tani) na Upatikanaji wa Chakula kwa Mwaka 2025/2026 – kwa Mlinganisho wa Nafaka ............................... 13

Jedwali Na. 2: Uzalishaji wa Mazao Asilia ya Biashara Mwaka 2025/2026.......................... 18

Jedwali Na 3: Uzalishaji wa Mazao ya Bustani Mwaka 2024/2025 ........................ 18

Jedwali Na. 4: Uzalishaji wa Mazao ya Mafuta Mwaka 2024/2025 ........................ 19

Jedwali Na. 5: Malengo na Uzalishaji wa Mazao Asilia ya Biashara (Tani) katika Mwaka 2025/2026 ........................ 66

Jedwali Na. 6: Malengo ya Uzalishaji wa Mazao Asilia ya Biashara (Tani) katika Mwaka 2026/2027 ...................... 163

## VIAMBATISHO


Kiambatisho Na. 1: Mchanganuo wa Usambazaji wa Mbegu ........................ 192

Kiambatisho Na. 2: Orodha ya viuatilifu vilivyoondolewa sokoni ........................ 204

Kiambatisho Na. 3: Mchanganuo wa Maeneo yaliyochukuliwa Sampuli za Afya ya Udongo ....... 215

Kiambatisho Na. 4: Orodha ya Miradi ya Umwagiliaji Ujenzi na Ukarabati .................... 216

Kiambatisho Na. 5: Orodha ya miradi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina .......... 228

Kiambatisho Na. 6: Orodha ya Visima vilivyochimbwa............ 236

Kiambatisho Na. 7: Orodha ya Miradi iliyofanyiwa Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii......................... 249

## VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| *ACU* | *Arusha Cooperative Union* |
| *AGCOT* | *Agriculture Growth Corridor of Tanzania* |
| *AGITF* | *Agricultural Inputs Trust Fund* |
| *AI* | *Artificial Intelligence* |
| *AMCOS* | *Agricultural Marketing Cooperatives Societies* |
| *AMP* | *Agricultural Transformation Master Plan* |
| *ASA* | *Agriculture Seed Agency* |
| *ASIs* | *Authorized Seed Inspectors* |
| *ATO* | *Agriculture Transforming Office* |
| *BBT* | *Building a Better Tomorrow* |
| *BBTV* | *Banana Bunchy Top Virus* |
| *BRELA* | *Business Registrations and Licensing Agency* |
| *CAADP* | *Comprehensive Africa Agricultural Development Programme* |
| *CAMARTEC* | *Centre for Agricultural Mechanization and Rular Technology* |
| *CCM* | *Chama Cha Mapinduzi* |
| *CHAWAKIM* | *Chama cha Ushirika wa Wafugaji Kiluvya – Mpiji* |
| *COASCO* | *Cooperative Audit and Supervision Corporation* |
| *COPRA* | *Cereal and Other Produce Regulatory Authority* |
| *CORECU* | *Coastal Regional Cooperative Union* |
| *CPB* | *Cereal and other Produce Board* |

| | |
|---|---|
| *CSDS* | *Crop Stock Dynamics* |
| *DOTA* | *Digital Online Tea Auction* |
| *EAC* | *East African Community* |
| *ESG* | *Environmental Social and Governance* |
| *ESIA* | *Environmental and Social Impact Assessment* |
| *EUDR* | *EU Deforestation Regulation* |
| *EUTCO* | *East Usambara Tea Company Limited* |
| *FAO* | *Food and Agriculture Organization* |
| *FTC* | *Farmers Training Centre* |
| *GDP* | *Gross Domestic Product* |
| *IFAD* | *International Fund for Agricultural Development* |
| *ITC* | *International Trade Centre* |
| *KACU* | *Kahama Cooperative Union* |
| *KCU* | *Kagera Cooperative Union* |
| *KDCU* | *Karagwe District Cooperative Union* |
| *KYECU* | *Kyela Cooperative Union* |
| *MAMCU* | *Masasi Mtwara Cooperative Union* |
| *MATI* | *Ministry of Agriculture Training Institute* |
| *MRLs* | *Maximum Residual Limits* |
| *MSD* | *Medical Stores Department* |
| *MUVU* | *Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika* |
| *MVIWATA* | *Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania* |
| *MVYULU* | *Muungano wa Vyama vya Ushirika Lupembe* |
| *NAESA* | *National Agricultural Extension Services Agency* |

| | |
|---|---|
| *NEOS* | *National Edible Oil Strategy* |
| *NFRA* | *National Food Reserve Agency* |
| *NIDA* | *National Identification Authority* |
| *NiRC* | *National Irrigation Commission* |
| *NMB* | *National Microfinance Bank* |
| *NMC* | *National Mechanization Centre* |
| *NSAAP* | *Nutrition Sensitive Agriculture Action Plan* |
| *NSSF* | *National Social Security Fund* |
| *PRA* | *Pest Risk Analysis* |
| *QDS* | *Quality Declared Seed* |
| *SACCA* | *Savings and Credit Cooperatives Associations* |
| *SACCOS* | *Savings and Credit Cooperative Society* |
| *SADC* | *Southern African Development Community* |
| *SAT* | *Sustainable Agriculture Tanzania* |
| *SDGs* | *Sustainable Development Goals* |
| *SIMCU Ltd* | *Simiyu Cooperative Union Limited* |
| *TaCRI* | *Tanzania Coffee Research Institute* |
| *TADB* | *Tanzania Agriculture Development Bank* |
| *TAHA* | *Tanzania Horticultural Association* |
| *TAKUKU RU* | *Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa* |
| *TAM* | *Tathmini ya Athari kwa Mazingira na jamii* |
| *TANCIS* | *Tanzania Customs Integrated System* |
| *TANECU* | *Tandahimba Newala Cooperative Union* |

| | |
|---|---|
| *TARECU* | *Tanga Regional Cooperative Union* |
| *TARI* | *Tanzania Agriculture Research Institute* |
| *TARURA* | *Tanzania Rural and Urban Road Agency* |
| *TASTA* | *Tanzania Seed Trade Association* |
| *TCDC* | *Tanzania Cooperative Development Commission* |
| *TCJE* | *Tumbaku Cooperative Joint Enterprise* |
| *TEHAMA* | *Teknolojia ya Habari na Mawasiliano* |
| *TFC* | *Tanzania Federation of Cooperatives* |
| *TFC* | *Tanzania Fertilizer Company* |
| *TFRA* | *Tanzania Fertilizer Regulatory Authority* |
| *TIN* | *Taxpayer Identification Number* |
| *TIRA* | *Tanzania Insurance Regulatory Authority* |
| *TMA* | *Tanzania Meteorological Authority* |
| *TMX* | *Tanzania Mercantile Exchange* |
| *TOAS* | *TOSCI Online Application Service* |
| *TOSCI* | *Tanzania Official Seed Certification Institute* |
| *TPC Ltd* | *Tanganyika Planting Company (TPC) Limited* |
| *TPHPA* | *Tanzania Plant Health and Pesticides Authority* |
| *TRA* | *Tanzania Revenue Authority.* |
| *TSP* | *Triple Super Phosphate* |
| *UJE* | *Ushirika Joint Enterprise* |
| *UKIMWI* | *Upungufu wa Kinga Mwilini* |
| *UMBEGU* | *Ubora wa Mbegu Uliobainishwa na Mkulima* |

| | |
|---|---|
| *USSD* | *Unstructured Supplementary Service Data* |
| *VETA* | *Vocational Education and Training Authority* |
| *VSS* | *Voluntary Sustainability Standards* |
| *VVU* | *Virusi Vya Ukimwi* |
| *WARCs* | *Ward Agricultural Resource Centers* |
| *WETCU* | *Western zone Tobacco Growers Co - operative Union* |

## Dira, Dhima, Majukumu na Malengo ya Wizara

**Dira**

Tujilishe na tuwalishe wengine kibiashara

**Dhima**

Kujenga Sekta ya Kilimo endelevu na yenye ushindani ili kukuza uchumi shirikishi, kuboresha maisha ya mkulima na Taifa lenye utajiri

**Majukumu**

Majukumu ya Wizara ya Kilimo yameainishwa katika Hati ya Rais ya Mgawanyo wa Majukumu ya Mawaziri (Presidential Instrument) iliyotolewa kupitia Tangazo Na. 686 na kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 19 Desemba, 2025. Majukumu hayo ni kama ifuatavyo:-

i. Kuandaa na kutekeleza Sera za Kilimo, Usalama wa Chakula, Umwagiliaji na Ushirika;

ii. Kusimamia Usalama wa Chakula;

iii. Kutoa/kusajili Leseni za ghala za mazao;

iv. Kusimamia Uhifadhi wa Kimkakati wa Chakula;

v. Kusimamia Maendeleo ya Ushirika na Vyama vya Ushirika;

vi. Kuratibu Maendeleo ya Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo;

vii. Kuendeleza Miundombinu ya Kilimo;

viii. Kusimamia Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Kilimo;

ix. Kusimamia Haki za Wagunduzi wa Mimea na Kuendeleza Uboreshaji wa Vinasaba vya Mimea;

x. Kuratibu Upatikanaji wa Masoko na Kuongeza Thamani ya Mazao ya Kilimo;

xi. Kusimamia Maendeleo ya Rasilimali watu na Utendaji Wizarani; na

xii. Kusimamia Idara zinazojitegemea, Taasisi za Serikali, Wakala, Programu na Miradi ya maendeleo iliyo chini ya Wizara.

**Malengo**

Katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara, Malengo Mkakati 10 yanatekelezwa kupitia Fungu 43 (Wizara ya Kilimo), Fungu 24 (Tume ya Maendeleo ya Ushirika) na Fungu 05 (Tume ya Taifa ya Umwagiliaji). Majukumu hayo yanatekelezwa kupitia Idara, Vitengo, Mamlaka na Taasisi zilizo chini ya Wizara. Malengo Mkakati hayo ni:-

i. Kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya kilimo;

ii. Kuongeza uzalishaji wa mazao ya bustani;

iii. Kupunguza gharama za uagizaji wa mafuta ya kula na ngano;

iv. Kupunguza upotevu wa mazao baada ya kuvuna kutoka wastani wa asilimia 35 hadi asilimia tano (5) ifikapo mwaka 2030;

v. Kuchangia kupunguza umaskini kwa asilimia 50 ifikapo mwaka 2030;

vi. Kuhakikisha upatikanaji wa malighafi za viwanda vinavyotumia mazao ya kilimo unafikia asilimia 100 ifikapo mwaka 2030;

vii. Kutengeneza ajira 3,000,000 za vijana na wanawake ifikapo mwaka 2030;

viii. Kuongeza thamani ya mauzo nje ya nchi kutoka Dola za Marekani Bilioni 1.2 hadi Dola za Marekani Bilioni 5 ifikapo mwaka 2030;

ix. Ukuaji wa kilimo kufikia asilimia 10 ifikapo mwaka 2030; na

x. Kuzingatia masuala mtambuka katika kilimo.

# 1 UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lipokee, kujadili na kupitisha taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka 2026/2027.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba Hotuba yangu iliyowasilishwa mezani iingie kwenye kumbukumbu za Bunge lako Tukufu. Aidha, Hotuba yote itapatikana kwenye tovuti ya Wizara ya Kilimo, www.kilimo.go.tz

## Shukrani na Pongezi

3. ***Mheshimiwa Spika,*** ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana hapa siku ya leo tukiwa na afya njema kwa ajili ya kujadili Taarifa ya Utekelezaji ya Wizara ya Kilimo ya mwaka 2025/2026 na Mpango na Bajeti kwa mwaka 2026/2027.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba nitumie nafasi hii kumpongeza Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuaminiwa na kuchaguliwa na wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika Oktoba 2025.

Kuchaguliwa kwake ni ishara tosha kuwa wananchi wana imani kubwa katika kuwaletea maendeleo wanayohitaji. Ninamuombea afya njema na ninampongeza sana!

5. ***Mheshimiwa Spika,*** pia ninampongeza Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kutekeleza vyema wajibu wake wa kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kuliongoza Taifa letu. Ninamtakia utekelezaji mwema wa majukumu yake.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** nitoe pongezi za dhati kwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kuchaguliwa kwa mara nyingine kuiongoza Serikali ya Zanzibar. Ninamuombea afya njema na mafanikio katika kutekeleza majukumu yake.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** nichukue nafasi hii pia kumpongeza Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb) kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninaamini kupitia yeye uratibu wa shughuli za Serikali utaendelea kuimarika na kuwezesha kufikiwa kwa malengo ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2025 – 2030 na Dira ya Taifa ya mwaka 2050.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** ninakupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kwa kishindo na Waheshimiwa Wabunge kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Daniel Baran Sillo (Mb), kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninaamini weledi, maarifa na busara zenu zitaendelea kutuongoza katika majadiliano ndani ya Bunge hili. Pia, ninawapongeza wabunge wenzangu wote kwa kuaminiwa na kuchaguliwa na wananchi wa Majimbo yenu kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

9. ***Mheshimiwa Spika***, nitumie fursa hii kumshukuru sana Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Kilimo. Ninamuahidi Mheshimiwa Rais na Watanzania wote kuwa nitatumikia nafasi ya uwaziri kwa bidii, maarifa, weledi na uadilifu mkubwa ili kuhakikisha malengo na matarajio ya Taifa na Wananchi yanafikiwa. Pia, ninampongeza Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Jimbo la Tunduma kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Kilimo. Ninaahidi kuwa nitaendelea kushirikiana naye katika kuendeleza jitihada za kuimarisha kilimo nchini.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** ninawapongeza Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini; Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum; na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninawapongeza kwa jinsi mnavyoliongoza Bunge letu Tukufu kwa weledi na maarifa.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** ninawapongeza Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini na Mheshimiwa Mariamu Ditopile Mzuzuri, Mbunge wa Jimbo la Kondoa Mjini kwa kuchaguliwa kuiongoza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo. Pia, ninawapongeza wabunge wote walioteuliwa kuwa Wajumbe wa Kamati hiyo. Ninawaahidi nitaendelea kutoa ushirikiano wa dhati katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Kamati.

12. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kwa ushirikiano, maoni, usimamizi, ufuatiliaji na miongozo mbalimbali waliyotoa kwa ajili ya kuendeleza sekta ya kilimo. Maoni na ushauri wao umezingatiwa katika kipindi chote cha utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2025/2026 na maandalizi ya mpango na bajeti ya mwaka 2026/2027.

13. ***Mheshimiwa Spika,*** ninamshukuru Ndugu Gerald Geofrey Mweli, Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Mhandisi Athumani Juma Kilundumya Naibu Katibu Mkuu anayesimamia Umwagiliaji na Zana za Kilimo na Prof. Peter Lawrence Makenga Msoffe Naibu Katibu Mkuu anayesimamia Maendeleo ya Mazao na Usalama wa Chakula. Vilevile, ninawashukuru Wakuu wa Idara na Vitengo, Wakuu wa Taasisi, Bodi, Wakala zilizo chini ya Wizara na Watumishi wote kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu.

14. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya kipekee na kwa unyenyekevu mkubwa, ninawashukuru wananchi wa Jimbo la Makambako kwa kuniamini na kunichagua kwa kura nyingi. Imani hiyo kwangu ni deni la kuwatumikia usiku na mchana katika kuwaletea maendeleo kwa vitendo. Mipango yetu tuliyoiweka ni msingi bora wa maendeleo na tumaini jipya la kuimarisha uchumi wa mtu mmoja mmoja na Makambako kwa ujumla, ikizingatiwa kuwa Makambako ni lango la uchumi kwa mikoa ya Nyanda za juu kusini.

15. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee ninamshukuru sana mke wangu Bi. Getrude na familia yangu kwa ujumla kwa kuniunga mkono katika utekelezaji wa majukumu yangu.

**Salamu za Pole**

16. ***Mheshimiwa Spika,*** ninatoa pole kwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwako wewe binafsi, wabunge, familia na watanzania wote kwa msiba wa aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu) Hayati William Vangimembe Lukuvi aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ismani. Hakika Taifa limepoteza kiongozi shupavu aliyekuwa mwalimu kwa wengi katika uwanja wa siasa na uongozi.

17. ***Mheshimiwa Spika,*** pia, ninatoa pole kwako wewe, Bunge lako Tukufu, familia na watanzania wote kwa ujumla kwa kuondokewa na wapendwa wetu, Hayati Jenista Joakim Mhagama aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Peramiho; na Hayati Halima Iddi Nassor aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalumu (Wafanyakazi). Wakati wote tutaendelea kukumbuka mchango wao katika maendeleo ya Taifa letu. **Bwana alitoa, Bwana ametwaa, Jina lake lihimidiwe** Amina.

**MAFANIKIO YA WIZARA YA KILIMO KWA KIPINDI CHA MWAKA 2021/2022 – 2025/2026**

18. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Kilimo imeendelea kutekeleza Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 – 2025/2026) chini ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na kiongozi

shupavu na mwenye maono ya kuleta mapinduzi katika sekta ya kilimo, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

19. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita, sekta ya kilimo imeimarika kwa kuendelea kuwekeza katika maeneo muhimu yanayodhihirisha dhamira ya dhati ya kumuinua mkulima na kuifanya Tanzania kuwa ghala la chakula barani Afrika.

20. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Awamu ya Sita tumeshuhudia ongezeko kubwa la bajeti ya Wizara ya Kilimo kutoka Shilingi Bilioni 294 mwaka 2021/2022 hadi Shilingi Trilioni 1.19 mwaka 2025/2026 ikiwa ni ishara tosha kuwa kilimo si ajenda ya pembeni bali ni kipaumbele namba moja cha Taifa katika kukuza uchumi na kuzalisha ajira.

21. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki tumeshuhudia dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Rais ya kumpunguzia mkulima gharama za uzalishaji kwa kuwezesha ruzuku ya pembejeo za kilimo kupitia mfumo wa kidijiti hadi vijijini. Huu ni ushahidi kuwa, Serikali hii inajali utu na ni hatua inayolenga kuhakikisha kuwa jasho la mkulima linazaa matunda kwa kuimarisha kipato cha mkulima.

22. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Sita imedhamiria kuandaa kizazi kipya cha wakulima matajiri kupitia Programu ya Jenga Kesho Iliyobora (BBT). Programu hii inawatambua vijana kama injini ya mabadiliko kwa kuwapatia teknolojia, ardhi kwa ajili ya kilimo, mitaji, kuwajengea miundombinu ya umwagiliaji na kuwaunganisha na masoko ya mazao ya kilimo.

23. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Awamu ya Sita tumeshuhudia jitihada kubwa za Mheshimiwa Rais katika kuimarisha masuala ya kidiplomasia na kuwezesha mazao yetu kuuzwa kwa wingi katika masoko makubwa yaliyopo nchi za Asia, Ulaya, Amerika na Afrika.

24. ***Mheshimiwa Spika,*** jitihada hizo zimechangia kupatikana kwa mafanikio yafuatayo:-

i. Sekta ya Kilimo katika mwaka 2024, ilikua kwa asilimia 4.1 ikiliganishwa na ukuaji wa asilimia 3.9 mwaka 2021. Aidha, mchango wa Sekta ya kilimo katika ukuaji wa Pato la Taifa ulikuwa asilimia 26.3 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 26.8 mwaka 2021;

ii. Uzalishaji wa mazao ya chakula umeongezeka kutoka tani 17,148,290 mwaka 2021/2022 hadi tani 23,783,128 mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia

38.69 na kufanya utoshelevu wa chakula nchini kufikia asilimia 130 ikilinganishwa na asilimia 126 mwaka 2021/2022;

iii. Uzalishaji wa mazao asilia ya biashara umeongezeka kutoka tani 973,436 mwaka 2021/2022 hadi tani 1,596,311.18 mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia 63.99;

iv. Uzalishaji wa mbegu bora ndani ya nchi umeongezeka kutoka tani 30,167.11 mwaka 2020/2021 hadi tani 54,750.47 mwaka 2025/2026 sawa na ongezeko la asilimia 81.49. Uzalishaji huo umechangia kuongezeka kwa upatikanaji wa mbegu bora kutoka tani 44,581.08 mwaka 2020/2021 hadi tani 79,214.48 mwaka 2025/2026 sawa na ongezeko la asilimia 77.68;

v. Uzalishaji wa mazao ya bustani umeongezeka kutoka tani 7,304,723 mwaka 2020/2021 hadi tani 9,781,236.74 mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia 33.9;

vi. Uzalishaji wa mazao ya mbegu za mafuta umeongezeka kutoka tani 1,713,178 mwaka 2020/2021 hadi tani 2,248,046.24 mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia 31.22;

vii. Uzalishaji wa ndani wa mbolea umeongezeka kutoka tani 32,239 mwaka 2020/2021 hadi tani 123,203 mwaka 2025/2026 sawa na ongezeko la asilimia 282.16. Uzalishaji huo umechangia upatikanaji wa mbolea kuongezeka kutoka tani 678,017 mwaka 2020/2021 hadi tani 1,098,990 mwaka 2025/2026 sawa na ongezeko la asilimia 62.09;

viii. Uwezo wa Hifadhi ya Taifa ya Chakula (NFRA) umeongezeka kutoka tani 251,000 mwaka 2020/2021 hadi tani 776,000 mwaka 2025/2026 sawa na ongezeko la asilimia 209.16; na

ix. Thamani ya mauzo ya mazao ya kilimo nje ya nchi imeongezeka kutoka Dola za Marekani Bilioni 2.1 mwaka 2021/2022 hadi kufikia Dola za Marekani Bilioni 3.73 mwaka 2024/2025.

25. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza dhamira ya Mheshimiwa Rais ya kuleta mageuzi makubwa ya sekta ya kilimo, Serikali ipo katika hatua za mwisho za kuanzisha Wakala ya Taifa wa Huduma za Ugani Kilimo (National Agriculture Extension Service Agency - NAESA). Uanzishaji wa NAESA si tu uamuzi wa kiutawala bali ni mkakati unaolenga kufikisha huduma za ugani karibu zaidi na mkulima.

26. ***Mheshimiwa Spika,*** katika eneo la miundombinu ya umwagiliaji, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imeendelea kutekeleza miradi 780. Kati ya hiyo, ujenzi na ukarabati wa miradi 28 yenye uwezo wa kumwagilia hekta 23,528 umekamilika na miradi 118 yenye uwezo wa kumwagilia hekta 232,658 ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Aidha, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa miradi 189 umekamilika na miradi 445 ipo katika hatua mbalimbali ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

27. ***Mheshimiwa Spika,*** katika eneo la Ushirika, usajili wa vyama vya ushirika kwenye Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika - MUVU umeongezeka kutoka vyama 4,661 mwaka 2022/2023 hadi vyama 6,545 mwaka 2025/2026. Kati ya hivyo, Vyama vya Ushirika wa Kilimo na Masoko (AMCOS) ni 4,685 na Vyama vya Akiba na Mikopo (SACCOS) ni 1,182. Aidha, mauzo ya mazao ya kilimo kupitia AMCOS yameongezeka kutoka Shilingi Trilioni 1.696 mwaka 2021/2022 hadi Shilingi Trilioni 3.74 mwaka 2025/2026. Vilevile, mali zinazomilikiwa na SACCOS zimeongezeka kutoka Shilingi Bilioni 836.74 mwaka 2021/2022 hadi Shilingi Trilioni 1.46 mwaka 2024/2025.

## 2 HALI YA KILIMO KATIKA MWAKA 2025

### 2.1 Ukuaji na Mchango katika Pato la Taifa

28. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Januari hadi Septemba 2025, Pato halisi la Taifa lilikua kwa wastani wa asilimia 6.0 ikilinganishwa na asilimia 5.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Aidha, Sekta ya kilimo imeendelea kuwa mhimili muhimu katika kuhakikisha usalama wa chakula, upatikanaji wa ajira, malighafi za viwandani na kuchangia katika Pato la Taifa (GDP). Katika kipindi cha Januari hadi Septemba 2025, Sekta ya Kilimo ilikua kwa asilimia 4.0. Vilevile, katika kipindi hicho, Sekta ya Kilimo iliongoza kwa kuchangia Pato la Taifa kwa asilimia 24.6.

### 2.2 Hali ya Chakula

29. ***Mheshimiwa Spika,*** tathmini ya hali ya chakula nchini ilibaini kuwa, uzalishaji wa mazao ya chakula katika msimu wa kilimo wa 2024/2025 ulifikia tani 23,783,128 ikilinganishwa na tani 22,803,316 katika msimu wa kilimo wa 2023/2024 sawa na ongezeko la asilimia 4.3. Kwa mazao ya nafaka uzalishaji ulikuwa tani 14,924,582 msimu wa 2024/2025, ikilinganishwa na tani 14,587,177 msimu wa 2023/2024 sawa na ongezeko la asilimia 2.3. Aidha, uzalishaji wa mazao yasiyo ya nafaka ulifikia tani 8,858,546 msimu wa 2024/2025 ikilinganishwa na tani 8,216,139 msimu wa 2023/2024 sawa na ongezeko la asilimia 7.8. Uzalishaji wa mazao

ya chakula umeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 1.**

30. ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa mazao ya chakula kwa msimu wa kilimo wa 2024/2025 ulitosheleza mahitaji ya chakula ya tani 18,279,054 kwa mwaka 2025/2026 na kuwepo kwa ziada ya tani 5,504,074. Kutokana na hali hiyo, Taifa limejitosheleza kwa chakula kwa asilimia 130.

**Jedwali Na. 1: Uzalishaji wa Mazao ya Chakula kwa Msimu 2024/2025 (Tani) na Upatikanaji wa Chakula kwa Mwaka 2025/2026 – kwa Mlinganisho wa Nafaka**

| **Nafaka** | **Mahindi** | **Mtama** | **Uwele na Ulezi** | **Mchele** | **Ngano** | **Nafaka** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Uzalishaji | 10,925,025 | 1,029,306 | 214,456 | 2,639,969 | 115,826 | 14,924,582 |
| Mahitaji | 7,386,333 | 582,045 | 2,521,245 | 1,238,367 | 328,703 | 12,056, |
| Uhaba (-)/Ziada(+) | 3,538,692 | 447,261 | 2,306,790 | 1,401,602 | -212,876 | 2,867,889 |
| SSR (%) | 148 | 177 | 9 | 213 | 35 | 124 |
| | | | | | | |
| **Yasiyonafal** | **Maharage** | **Mikunde mingine** | **Ndizi** | **Muhogo** | **Viazi** | **Yasiyona** |
| Uzalishaji | 1,245,906 | 1,277,302 | 1,413,582 | 2,649,254 | 2,272,502 | 8,858,546 |
| Mahitaji | 483,645 | 497,036 | 1,148,964 | 2,868,655 | 1,224,060 | 6,222,361 |
| Uhaba (-)/Ziada(+) | 762,261 | 780,266 | 264,618 | -219,402 | 1,048,443 | 2,639,286 |
| SSR (%) | 258 | 257 | 123 | 92 | 186 | 142 |
| **Jumla** | **Nafaka** | **Yasiyonafaka** | | | | **Jumla** |
| Uzalishaji | 14,924,582 | 8,858,546 | | | | 23,783,128 |
| Mahitaji | 12,056,694 | 6,222,361 | | | | 18,279,054 |
| Uhaba (-)/Ziada(+) | 2,867,889 | 2,639,286 | | | | 5,504,074 |
| **SSR (%)** | **124** | **142** | | | | **130** |

**Chanzo:** W*izara ya Kilimo, 2026*

# 3 UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2025/2026

## 3.1 Makusanyo ya Maduhuli

**Fungu 43**

31. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Wizara ilipanga kukusanya Shilingi **8,665,370,000.00** kupitia Fungu 43 kutokana na ukaguzi wa mazao, kodi za mazao na uuzaji wa nyaraka za zabuni. Hadi Machi 2026, kiasi cha Shilingi **13,780,925,984.21** sawa na asilimia 159.03 zimekusanywa.

**Fungu 05**

32. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Wizara ilipanga kukusanya mapato ya Shilingi **3,600,000,000.00** kupitia Fungu 05, kutokana na vyanzo mbalimbali. Hadi Machi 2026, Wizara imekusanya Shilingi **2,059,882,529.88** sawa na asilimia 57.22 ya lengo.

## 3.2 Fedha Zilizoidhinishwa kwa Fungu 43, 24 na 05

33. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Wizara ya Kilimo ilitengewa jumla ya Shilingi **1,192,975,075,000.00** kupitia Fungu 43, Fungu 24 na Fungu 05. Kati ya fedha hizo, Shilingi **961,695,070,000.00** ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na Shilingi **231,280,005,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

34. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Fungu 43 lilitengewa jumla ya Shilingi **788,259,822,000** ikijumuisha Shilingi **652,275,933,000** kwa ajili ya miradi ya maendeleo na Shilingi **135,983,889,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Aidha, Fungu 24, lilitengewa jumla ya Shilingi **22,576,845,000** ambapo kati ya hizo Shilingi **697,176,000** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo na Shilingi **21,879,669,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Pia, jumla ya Shilingi **382,138,408,000** zilitengwa kwa ajili ya Fungu 05, ambapo Shilingi **308,721,961,000** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo na Shilingi **73,416,447,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

**Fedha zilizotolewa**

35. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi 2026, jumla ya Shilingi **532,512,056,288.15** sawa na asilimia 42.84 ya fedha zilizoidhinishwa kwa Fungu 43, Fungu 24 na Fungu 05 zimetolewa. Kati ya fedha hizo, Shilingi **436,540,226,893.57** ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na Shilingi **95,971,829,394.58** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

36. ***Mheshimiwa Spika,*** fedha zilizotolewa zinajumuisha Shilingi **369,926,241,178.68** kwa ajili ya Fungu 43 (maendeleo Shilingi **294,210,308,543.25** na matumizi ya kawaida Shilingi **75,715,932,635.43**); Shilingi **14,387,652,536.16** kwa ajili ya Fungu 24 (maendeleo Shilingi **278,880,000** na matumizi

ya kawaida Shilingi **14,108,772,536.16**); na Shilingi **152,709,956,737.82** kwa ajili ya Fungu 05 (maendeleo Shilingi **142,051,038,350.32** na matumizi ya kawaida shilingi **10,658,918,387.50**).

## 4 UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2025/2026

37. ***Mheshimiwa Spika***, utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2025/2026, umezingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025; Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano Awamu ya Tatu (2021/2022 - 2025/2026); Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Sera ya Taifa ya Kilimo ya Mwaka 2013; Sera ya Taifa ya Umwagiliaji ya Mwaka 2010; na Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya Mwaka 2002. Aidha, utekelezaji umezingatia Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030; Mpango Kabambe wa Mageuzi ya Kilimo wa Mwaka 2050; Mkakati wa Ukuzaji wa Sekta ya Kilimo 2030; Mkakati wa Kuongeza Fedha za Kigeni (2023/2024 – 2027/2028); Azimio la Kampala kuhusu Program ya Kuendeleza Kilimo Barani Afrika (CAADP 2035); Mwongozo na Mpango wa Bajeti wa Mwaka 2025/2026; Maoni na Ushauri wa Kamati za Kudumu za Bunge; Maoni ya Baraza la Rais la Ushauri wa Usalama wa Chakula na Kilimo, wadau wa maendeleo na masuala mtambuka ya jinsia, mazingira, lishe, mabadiliko ya tabianchi, vijana, kutokomeza ajira kwa watoto katika Sekta ya kilimo, VVU na UKIMWI.

38. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2025/ 2026, Wizara ya Kilimo imetekeleza vipaumbele sita (6) ambavyo ni kuongeza uzalishaji na tija; kuchangia kuongeza ajira zenye staha na ushiriki wa vijana na wanawake katika kilimo; kuimarisha usalama wa chakula na lishe; kuimarisha upatikanaji wa masoko, mitaji na mauzo ya mazao nje ya nchi; kuimarisha maendeleo ya ushirika; na kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika uendelezaji wa sekta ya kilimo. Vipaumbele hivyo, vimetekelezwa kupitia mikakati 30. Mafanikio ya utekelezaji wa bajeti ni kama ifuatavyo:-

## 4.1 Kuongeza Uzalishaji na Tija

39. ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa mazao ya chakula katika msimu wa kilimo wa 2024/2025 ulifikia tani 23,783,128 ikilinganishwa na tani 22,803,316 katika msimu wa kilimo wa 2023/2024 sawa na ongezeko la asilimia 4.3. Mathalani:- uzalishaji wa mazao ya nafaka ulifikia tani 14,924,582 ikilinganishwa na tani 14,587,177 mwaka 2023/2024 na mazao yasiyo ya nafaka tani 8,858,546 ikilinganishwa na tani 8,216,139 mwaka 2023/2024.

40. ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa mazao asilia ya biashara unaohusisha mkonge, miwa/sukari, pamba, kahawa, korosho, tumbaku, pareto, chai na kakao umefikia tani 1,599,945.66 sawa na asilimia 71.9 ya lengo la kuzalisha tani

2,225,000. Mwenendo wa uzalishaji wa mazao hayo umeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 2.**

**Jedwali Na. 2: Uzalishaji wa Mazao Asilia ya Biashara Mwaka 2025/2026**

| Na. | Mazao | Uzalishaji (Tani) |
|---|---|---|
| 1 | Korosho | 617,683.77 |
| 2 | Pamba | 222,014 |
| 3 | Pareto | 2,780* |
| 4 | Kahawa | 74,663.60 |
| 5 | Tumbaku | 185,776 |
| 6 | Chai | 11,631.48* |
| 7 | Mkonge | 64,321.77 |
| 8 | Sukari | 410,979.04* |
| 9 | Kakao | 10,096* |
| **Jumla** | | **1,599,945.66** |

***Chanzo:*** *Wizara ya Kilimo, 2026*
**Uzalishaji unaendelea*

41. ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa mazao ya bustani umefikia tani 9,781,936.74 mwaka 2024/2025 sawa na asilimia 108.68 ya lengo la kuzalisha tani 9,000,000. Aidha, uzalishaji wa mazao ya bustani umeoneshwa katika **Jedwali Na. 3**.

**Jedwali Na 3: Uzalishaji wa Mazao ya Bustani Mwaka 2024/2025**

| Na. | Mazao | Uzalishaji (Tani) |
|---|---|---|
| 1. | Matunda | 8,051,887.41 |
| 2. | Mboga | 1,634,590.96 |
| 3. | Viungo | 95,458.37 |
| | **Jumla** | **9,781,936.74** |

***Chanzo:*** *Wizara ya Kilimo, 2026*

42. ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa mazao ya mafuta ulifikia tani 2,248,046.23 mwaka 2024/2025 sawa na asilimia 102.18 ya lengo la kuzalisha tani 2,200,000 ikilinganishwa na tani 2,181,603.65 mwaka 2023/2024. Uzalishaji wa mazao ya mafuta umeoneshwa kwenye **Jedwali. Na. 4.**

**Jedwali Na. 4: Uzalishaji wa Mazao ya Mafuta Mwaka 2024/2025**

| Na | Mazao | Uzalishaji (Tani) |
|---|---|---|
| 1. | Alizeti | 1,222,209.64 |
| 2. | Ufuta | 257,040.84 |
| 3. | Nazi | 85,152.70 |
| 4. | Chikichi | 74,302.65 |
| 5. | Karanga | 609,340.40 |
| | **Jumla** | **2,248,046.23** |

**Chanzo:** *Wizara ya Kilimo, 2026*

43. ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio haya ya kuongezeka kwa uzalishaji si ya bahati mbaya bali ni matokeo ya uwekezaji wa makusudi katika maeneo ya kimkakati uliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita. Maeneo ya kimkakati ni pamoja na kuwawezesha wakulima kupata pembejeo za kilimo ikiwemo mbolea, mbegu bora, viuatilifu na zana za kilimo kupitia mpango wa ruzuku, ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji, kuimarika kwa huduma za ugani kilimo na masoko.

44. ***Mheshimiwa Spika,*** mikakati iliyotekelezwa na Wizara kufikia mafanikio hayo ni ifuatayo:-

### 4.1.1 Utafiti wa Mbegu

45. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuendeleza teknolojia za kilimo, Wizara kupitia TARI katika mwaka 2025/2026 ilipanga kuendelea na utafiti wa mbegu aina 56 za mazao ya kimkakati; kutafiti teknolojia za afya ya udongo na mbolea; kutafiti na kutambua gharama za uzalishaji wa tumbaku zinazokaushwa kwa mvuke, moshi, hewa na jua; kutoa mafunzo kuhusu kurejesha afya ya udongo kwa wakulima 600; kutafiti magonjwa ya fungashada – BBTV katika zao la migomba, *cashew leaf and nut blight*, ubwiri unga na mnyauko fusari katika zao la korosho; kutafiti funza wa vitumba na chawa jani katika zao la pamba; *thrips* kwenye zao la miwa; na tafiti za viuatilifu vya visumbufu vya mimea katika zao la mtama.

46. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, ilipanga kutafiti aina ya miti ya kivuli inayofaa katika zao la chai; kutafiti teknolojia saba (7) za kuongeza thamani ya mazao ya kilimo; kusafisha na kutunza aina 360 za mbegu za asili za mazao ya kilimo; kukusanya na kutunza vinasaba 12,968 vya mazao ya kilimo; kuzalisha mbegu za mazao ya kimkakati tani 1,500; kuendelea na ujenzi wa ghala 11; kuendelea na ujenzi wa maabara za kuzalisha miche kwa njia ya chupa; na kuendelea na

ujenzi wa maabara ya kudhibiti visumbufu vya mimea na mazao.

47. ***Mheshimiwa Spika***, katika kulinda mashamba ya utafiti wa mbegu dhidi ya uvamizi, Wizara ilipanga kuendelea na ujenzi wa uzio katika mashamba ya utafiti wa mbegu; kulipa fidia kwa wananchi watakaohamishwa katika Kituo cha TARI Uyole; kuhakikisha upatikanaji wa hatimiliki katika vituo 17 na mashamba ya majaribio 18; kuendelea na ujenzi wa Kituo cha *Bioscience;* kuendelea na ujenzi wa Benki ya Mbegu (Genebank) katika Kituo cha TARI Selian; kuendelea na ujenzi wa Ofisi ya TARI Makao Makuu (Njedengwa, Dodoma); kukamilisha ukarabati wa nyumba 49 za watumishi; kujenga ofisi moja (1) katika kituo cha TARI Hombolo na kununua vifaa vya Ofisi ya TARI Kihinga.

48. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ilipanga kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji yenye jumla ya hekta 2,120.9 katika vituo 16 vya TARI; kutoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora na uongezaji thamani wa mazao ya zabibu na korosho kwa wakulima 800 na Maafisa Ugani 180. Vilevile, kuendelea na ujenzi wa nyumba tatu (3) za watumishi, jiko na hosteli katika Kituo cha Utafiti wa Kahawa cha Mwayaya (Buhigwe) na kununua mashine ya kukaanga kahawa.

49. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi Machi 2026, Wizara kupitia TARI imetekeleza yafuatayo:-

**Utafiti**

50. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha utafiti wa mbegu, aina 30 za mbegu za mazao ya kimkakati ya nafaka, jamii ya mikunde, mizizi na mafuta zimefanyiwa utafiti, sawa na asilimia 54 ya lengo la aina 56 za mbegu. Kati ya hizo, aina mbili (2) ni mbegu za muhogo zenye uwezo wa kuzalisha kati ya tani 20 hadi 28.8 kwa hekta ambazo zipo katika hatua za kuidhinishwa kwa ajili ya matumizi; na aina 28 ni mbegu za mazao ya mahindi (6), maharage (3), ufuta (3), mpunga (9), ngano (3) na mtama (4) zimewasilishwa Taasisi ya Uthibiti Ubora wa Mbegu (TOSCI) kwa ajili ya majaribio ya utambuzi na umahiri. Pia, aina 14 za mbegu za migomba zenye uwezo wa kuzalisha kati ya tani 50 hadi 60 kwa hekta zimeidhinishwa na Kamati ya Taifa ya Mbegu kwa ajili ya matumizi.

51. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, imegundua *genotype* tatu (3) za karanga zenye sifa ya mavuno mengi na ustahimilivu wa magonjwa ambazo ni NALX-22-18 (tija kilo 1,356.77 kwa hekta), ICGIL 17113 (tija kilo 1,371.91 kwa hekta) na ICGIL14466 (tija kilo 1,313.65 kwa hekta). Mbegu hizo zitawasilishwa

TOSCI kwa majaribio ya utambuzi na umahiri wa mbegu.

52. ***Mheshimiwa Spika,*** pia, imefanya tathmini ya mbegu mpya aina tatu (3) za tumbaku ya mvuke (PVH2343 na TRF23) na hewa (TRB24) na kubaini kuwa zinafaa kwa uzalishaji nchini. Mbegu hizo zimewasilishwa TOSCI kwa ajili ya Majaribio ya Kitaifa ya Umahiri wa Mbegu kwa hatua za kuidhinishwa. Vilevile, sampuli 34 za udongo zimechukuliwa katika mashamba ya wakulima wa tumbaku katika wilaya za Uyui, Kaliua, Uvinza, Kasulu, Tanganyika, Chunya, Namtumbo, Kahama, Mbogwe na Serengeti kwa ajili ya utafiti wa afya ya udongo ili kubaini kiwango sahihi cha uwekaji wa mbolea ya kupandia na kukuzia kwa tumbaku ya mvuke.

53. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuimarisha udhibiti wa visumbufu vya mimea na mazao, utafiti wa aina 10 za viuatilifu umekamilika na aina tano (5) zipo katika hatua ya uthibitisho kwa ajili ya udhibiti wa ugonjwa wa ubwiri unga katika zao la korosho. Pia, inaendelea na utafiti wa vitumba na chawa jani katika zao la pamba, BBTV katika zao la migomba, *thrips* katika zao la miwa na tafiti za visumbufu vya mimea katika zao la mtama.

54. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara inaendelea kutambua thamani ya kipekee ya mbegu zetu za asili kama nguzo muhimu ya usalama wa

chakula na uhifadhi wa mazingira. Mbegu hizo si tu kielelezo cha urithi wetu bali ni nyenzo madhubuti ya kukabiliana na mabadiliko ya tabiachi kutokana na ustahimilivu wake wa asili dhidi ya ukame na magonjwa. Ukusanyaji na uhifadhi wa mbegu hizo ni chanzo cha utafiti na uzalishaji wa mbegu bora. Pia, ni uwezeshaji wa wananchi kuwa na uwezo wa kulima, kutunza na kuhifadhi mbegu hizo kwa matumizi ya sasa na ya siku zijazo kwa gharama nafuu. Katika kutekeleza hilo, Wizara imesafisha na kutunza aina 54 za mbegu za asili. Kati ya hizo, aina 49 ni za mpunga na aina tano (5) ni za migomba.

55. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, nasaba 33,164 mazao ya korosho (20,573), chikichi (5,885), mpunga (1,519), parachichi (999), matunda (839), mahindi (574), muhogo (521), ufuta (350), pamba (342), viazi vitamu (311), migomba (294), kakao (293), dengu (183), miwa (126), alizeti (91), maharage (85), mkonge (75), zabibu (36), viungo (18), choroko (16), mazao ya misitu (14), nyanya (8), uwele (7) na mtama (5) vimekusanywa na kutunzwa kwa lengo la kuendeleza shughuli za utafiti.

**Miundombinu ya Utafiti**

56. ***Mheshimiwa Spika***, ili kukamilisha mnyororo wa utafiti na uzalishaji, ujenzi wa ghala za kisasa katika vituo vya utafiti ni hitaji la lazima na la kimkakati. Ghala hizo ni

muhimu kwa ajili ya uhifadhi wa mbegu za utafiti ambazo ndiyo msingi wa mbegu bora zinazowafikia wakulima. Bila ghala za kisasa, kazi kubwa ya watafiti wetu inaingia hatarini kwa mbegu za utafiti kuharibika kutokana na unyevu na wadudu.

57. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha uhifadhi wa mbegu za utafiti zinazozalishwa na TARI ujenzi wa ghala 11 zenye uwezo wa kuhifadhi tani 415 kila moja katika vituo vya utafiti vya TARI Maruku, TARI Ukiriguru, TARI Kifyulilo, TARI Uyole (Igeri na Nkundi), TARI Tumbi, TARI Selian, TARI Hombolo, TARI Dakawa na TARI Naliendele umefikia wastani wa asilimia 35.2 na ujenzi unaendelea.

58. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuongeza uzalishaji wa miche kwa ajili ya wakulima, Wizara imezingatia kwa umuhimu wa kipekee matumizi ya teknolojia ya kuzalisha miche kwa njia ya chupa (tissue culture) ikiwa ni hatua muhimu ya kisayansi kuelekea kilimo cha kibiashara. Hivyo, ujenzi wa maabara ya *tissue culture* katika kituo cha TARI Tengeru mkoani Arusha na kituo cha TARI Maruku mkoani Kagera umefikia wastani wa asilimia 30 na ujenzi unaendelea.

59. ***Mheshimiwa Spika***, kukamilika kwa maabara hizo kutachangia kuzalisha kwa wingi miche ya mazao yasiyozalishwa kwa mbegu za kawaida kwa asili yenye uwezo wa kuzalisha

kwa mwaka migomba miche 1,500,000, muhogo pingili 10,000,000 na viazi vipando 1,000,000.

60. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha udhibiti wa visumbufu vya mimea na mazao, ujenzi wa maabara ya kudhibiti visumbufu vya mimea katika Kituo cha utafiti cha TARI Naliendele umefikia asilimia 60 na ujenzi unaendelea. Aidha, ujenzi wa Benki ya Taifa ya Mbegu kwa ajili ya kuhifadhi mbegu za utafiti katika Kituo cha TARI Selian umefikia asilimia 5 na mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha *Bioscience* katika Mkoa wa Morogoro amepatikana.

61. ***Mheshimiwa Spika***, ili kulinda mashamba ya utafiti wa mbegu dhidi ya uvamizi wa wanyama na shughuli za kibinadamu, ikiwa ni hatua muhimu ya kulinda uwekezaji mkubwa wa Serikali na kazi za kitaalamu zinazofanyika, ujenzi wa uzio katika mashamba ya utafiti wa mbegu ya TARI Kifyulilo, TARI Dakawa, TARI Hombolo, TARI Maruku, TARI Ifakara na TARI Kihinga umefikia wastani wa asilimia 30 na ujenzi unaendelea.

62. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha mazingira ya utendaji kazi na kuongeza ufanisi kwa watumishi, TARI inaendelea na ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu (Njedengwa, Dodoma) ambapo ujenzi huo umefikia asilimia 75 na ujenzi wa Ofisi katika kituo cha utafiti cha TARI

Hombolo umefikia asilimia 15. Vilevile, ukarabati wa majengo sita (6) ya ofisi na nyumba za watumishi katika vituo vya utafiti vya TARI Mlingano umefikia asilimia 35, TARI Ilonga asilimia 20 na TARI Tumbi asilimia 20.

63. ***Mheshimiwa Spika***, pia mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa nyumba tatu (3) za watumishi, jiko na hosteli katika Kituo cha Utafiti wa Kahawa cha Mwayaya (Buhigwe) amepatikana. Pia, ununuzi wa vifaa vya ofisi za TARI Kihinga umekamilika.

64. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia na kuongeza ufanisi, Wizara kupitia TARI imetoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora na uongezaji thamani wa mazao ya zabibu, alizeti na korosho kwa wakulima 549 na Maafisa Ugani 990 katika mikoa ya Dodoma, Singida, Mtwara, Lindi, Ruvuma, Pwani na Singida. Aidha, mzabuni kwa ajili ya ununuzi wa mashine yenye uwezo wa kukaanga kahawa kilo 60 kwa siku amepatikana.

65. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha uzalishaji wa mbegu za utafiti unafanyika kipindi chote cha mwaka, ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji yenye jumla ya hekta 1,120.9 katika vituo 16 vya TARI unaendelea. Pia, mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji yenye jumla ya hekta 1,000 katika vituo vya utafiti vya TARI Uyole (hekta 800) na

TARI Ukiriguru (hekta 200) amekabidhiwa maeneo kwa ajili ya kuanza ujenzi.

**Uzalishaji wa mbegu za utafiti na kulinda maeneo ya utafiti**

66. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia TARI imezalisha mbegu tani 1,037.59 sawa na asilimia 69.17 ya lengo la tani 1,500. Kati ya hizo, tani 77.33 ni mbegu mama, tani 355.28 ni mbegu za awali, tani 435.58 ni mbegu za msingi na tani 169.40 ni mbegu zilizothibitishwa.

67. ***Mheshimiwa Spika***, tathmini kwa ajili ya malipo ya fidia kwa wananchi watakaopisha ujenzi wa uzio katika shamba la TARI - Uyole imefanyika na kubaini wananchi wanaotakiwa kulipwa fidia ni 186 ambapo takriban Shilingi Bilioni 6 zitatumika kulipa fidia na taratibu za malipo ya fidia zinaendelea. Pia, upimaji wa maeneo katika vituo 17 vya utafiti wa kilimo vya TARI na mashamba ya majaribio 18 umefanyika na taratibu za upatikanaji wa hatimiliki zinaendelea.

### 4.1.2 Uzalishaji na Usambazaji wa Mbegu na Miche Bora kwa Mpango wa Ruzuku kwa baadhi ya Mazao

68. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2025/2026, ilipanga kuongeza uzalishaji wa mbegu bora kufikia tani 90,000; kuongeza upatikanaji wa mbegu bora kufikia tani

105,000; kutoa ruzuku ya mbegu bora za alizeti tani 5,000 na mahindi tani 52,000; kujenga miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya mbegu yenye ukubwa wa hekta 3,000; na kujenga miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya mbegu yenye ukubwa wa hekta 495.

69. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilipanga kujenga uzio katika mashamba ya kuzalisha mbegu; kujenga ofisi moja (1), karakana katika shamba la mbegu la Kilimi na kukarabati ofisi mbili (2) katika mashamba ya mbegu ya Mwele na Mbozi; kujenga ghala mbili (2); kununua na kusimika mitambo minne (4) ya kuchakata mbegu na mashine moja (1) ya kukausha mbegu; kununua magari matano (5) na lori moja (1); kukarabati nyumba za watumishi, karakana na jengo la kuanikia mbegu katika shamba la mbegu Msimba; na kununua chokaa mazao tani 1,000.

70. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilipanga kuzalisha na kusambaza miche 64,183,900 ya mazao ya kilimo na pingili za muhogo 4,361,600; kuandaa mfumo wa kidijiti kwa ajili ya ufuatiliaji wa maendeleo ya miche; kukagua mashamba ya mbegu yenye ukubwa wa hekta 100; kununua mtambo wa kuchapisha lebo na kutoa lebo 32,000,000 za mbegu bora; kutoa mafunzo kwa wakaguzi wa mbegu 50 na wakaguzi wa mbegu walioidhinishwa (ASI's) 40;

na kuendelea na ukarabati wa ofisi za TOSCI Makao Makuu na ofisi za kanda.

71. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi Machi 2026, Wizara imetekeleza yafuatayo:-

72. ***Mheshimiwa Spika,*** upatikanaji wa mbegu bora ndani ya nchi umefikia tani 79,214.48 sawa na asilimia 75.44 ya lengo la kuzalisha tani 105,000. Kati ya kiasi hicho, tani 54,750.47 sawa na asilimia 69.12 zimezalishwa ndani ya nchi na tani 24,464.01 sawa na asilimia 30.88 zimeagizwa kutoka nje ya nchi. Aidha, kati ya tani 54,750.47 zilizozalishwa ndani ya nchi, tani 47,178.47 zimezalishwa na sekta binafsi na tani 7,572 zimezalishwa na ASA.

73. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa muda mrefu, ASA imekuwa ikizalisha mbegu katika mashamba yake yaliyopo mikoa mbalimbali nchini. Kuanzia msimu wa kilimo 2024/2025, ASA ilianza kuzalisha mbegu bora kupitia mfumo wa kilimo cha mkataba (Contract Growing Scheme) ambapo kumekuwa na utaratibu wa sekta binafsi kutumia mashamba ya ASA kwa ajili ya uzalishaji wa mbegu bora. Mfumo huo umewezesha kuongeza uzalishaji wa mbegu bora kutoka tani 4,510 mwaka 2023/2024 hadi kufikia tani 9,303 mwaka 2024/2025.

**Ruzuku ya Mbegu Bora**

74. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali ilianza rasmi kutekeleza mpango wa ruzuku ya mbegu za mahindi katika msimu wa kilimo wa 2024/2025. Katika mwaka 2025/2026, jumla ya tani 55,041.124 zenye thamani ya jumla ya Shilingi Bilioni 374.2 zimeuzwa kwa mfumo wa ruzuku ikilinganishwa na tani 9,639.63 za mbegu bora za mahindi zenye thamani ya Shilingi Bilioni 12.3 zilizouzwa mwaka 2024/ 2025. Katika mwaka 2025/2026, ruzuku ya Serikali ni Shilingi Bilioni 84.85 na mchango wa wakulima ni Shilingi Bilioni 289.3. Utekelezaji wa mpango huo, umewezesha kuongeza matumizi ya mbegu bora za mahindi ambapo jumla ya wakulima 531,903 wamenufaika.

75. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi hicho, tani 702.43 za mbegu bora za alizeti zimesambazwa kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku na usambazaji unaendelea. Aidha, mbegu bora za ngano tani 500 na mpunga tani 500 zimesambazwa kwa wakulima katika mikoa ya uzalishaji. Pia, mbegu bora za ufuta tani 37.98, mbaazi tani 17.34, choroko tani 10.70, dengu tani nne (4) na soya tani moja (1) zimesambazwa kwa wakulima katika maeneo ya uzalishaji. Mchanganuo wa usambazaji wa mbegu unaonekana katika **Kiambatisho Na 1**. Kadhalika, TOSCI imeainisha wazalishaji 75

watakaozalisha mbegu za kuazimia ubora (QDS) za mazao ya soya, dengu na mbaazi.

**Uthibiti wa Ubora wa Mbegu**

76. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha uthibiti wa ubora wa mbegu ili kukabiliana na changamoto ya mbegu zisizo na ubora, Wizara kupitia TOSCI imekagua mashamba ya mbegu 1,269 yenye ukubwa wa hekta 19,004.1. Kati ya hizo, hekta 18,636 zilikidhi vigezo vya uzalishaji wa mbegu na hekta 368.1 hazikukidhi vigezo. Wamiliki wa mashamba ambayo hayakukidhi vigezo walielekezwa kuzingatia taratibu za uzalishaji wa mbegu bora katika msimu ujao.

77. ***Mheshimiwa Spika***, ujenzi wa Maabara ya Taifa ya Mbegu iliyopo Makao Makuu ya TOSCI - Morogoro umefikia asilimia 95; na wakandarasi kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa maabara nne (4) za Kanda ya Ziwa – Mwanza, Kusini – Mtwara, Kaskazini – Arusha na Magharibi – Tabora wamesaini mikataba kwa ajili ya kuanza ujenzi. Kukamilika kwa maabara hizo kutaongeza kuthibiti ubora wa mbegu kwa kutumia teknolojia za kisasa na kuendelea kulinda taswira ya Tanzania katika viwango vya ubora wa mbegu kimataifa na kufungua fursa mpya kwa uwekezaji katika uzalishaji na biashara ya mbegu.




*Ujenzi wa Maabara ya Taifa ya Mbegu iliyopo Makao Makuu ya TOSCI - Morogoro*

78. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuongeza ufanisi wa uthibiti wa ubora wa mbegu, zabuni kwa ajili ya ununuzi wa mtambo wa kuchapisha lebo zitakazotumika katika vifungashio vya mbegu imetangazwa. Vilevile, lebo 30,882,500 za mbegu bora zimetolewa sawa na asilimia 96.5 ya lengo la kutoa lebo 32,000,000; na mafunzo kwa wakaguzi wa mbegu 144 yametolewa. Kati ya hao, 62 ni wakaguzi walioidhinishwa (ASI's) katika ngazi ya Halmashauri za Wilaya na 82 ni wakaguzi wa mbegu wa TOSCI.

## Miundombinu ya uzalishaji mbegu

79. ***Mheshimiwa Spika***, katika kulinda mashamba ya mbegu dhidi ya uvamizi, ujenzi wa uzio katika mashamba ya Kilangali (km 20.8) umefikia asilimia 30, Mwele (km 14) asilimia 15, Namtumbo (km 33) asilimia 5 na mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa uzio katika shamba la Arusha (km 17) amekabidhiwa eneo kwa ajili ya kuanza ujenzi.

80. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara katika kuongeza ufanisi wa watumishi kwenye mashamba ya mbegu, imeendelea na ujenzi wa nyumba za watumishi ambapo ujenzi katika mashamba ya mbegu ya Msungura (nyumba 3) umefikia wastani wa asilimia 83, Kilimi (nyumba 2) asilimia 55, Mbozi (nyumba 6) asilimia 50, Arusha (nyumba 10) asilimia 35, Namtumbo (nyumba 3) asilimia 35 na Mwele (nyumba 4) asilimia 15. Pia, ujenzi wa ofisi moja (1) katika shamba la mbegu la Kilimi umefikia asilimia 80. Aidha, ujenzi wa karakana katika shamba la mbegu la Kilimi umekamilika. Karakana hiyo itatumika kwa ajili ya ukarabati wa mitambo inayotumika katika uzalishaji wa mbegu bora.

81. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuongeza ufanisi wa usambazaji wa mbegu bora na kuimarisha usimamizi, Wizara kupitia ASA imenunua magari matano (5) na malori matatu (3) yenye uwezo wa kubeba tani 30 za mbegu

kila moja. Aidha, ili kuongeza uhifadhi na kuimarisha ubora wa mbegu, ujenzi wa ghala mbili (2) zenye uwezo wa kuhifadhi mbegu tani 2,500 katika shamba la BBT Ndogowe (tani 1,000) na shamba la mbegu la Arusha (tani 1,500) umefikia asilimia 10 na asilimia mbili (2), mtawalia.

82. ***Mheshimiwa Spika***, upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba saba (7) ya mbegu yenye ukubwa wa hekta 3,495 ya Namtumbo (1,000), Mbozi (600), Msimba (395), Kilimi (260), Arusha (340), Msungura (100) na Luhafwe (800) unaendelea.

83. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuongeza upatikanaji na ubora wa mbegu, Wizara kupitia ASA, imetangaza zabuni kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa kununua na kusimika mitambo minne (4) ya kuchakata mbegu na mashine moja (1) ya kukausha mbegu. Aidha, mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa jengo la kuanikia mbegu katika shamba la Msimba amekabidhiwa eneo. Vilevile, zabuni kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa ujenzi wa karakana itakayotumika kwa ajili ya matengezo ya mitambo na mashine katika shamba la mbegu la Msimba imetangazwa.

84. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuongeza ufanisi wa kazi kwa watumishi kwa kuweka mazingira wezeshi, Wizara kupitia ASA

imekamilisha ukarabati wa nyumba tano (5) za watumishi katika shamba la mbegu la Msimba. Aidha, mzabuni kwa ajili ya kusambaza tani 1,000 za chokaa zitakazotumika katika kuboresha afya ya udongo kweye mashamba ya mbegu ya Kilangali, Msimba na Dabaga ambayo yameathiriwa na tindikali amepatikana.

**Uzalishaji wa Vipando**

85. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha wakulima wanapata miche bora kwa gharama nafuu na kwa wakati, Wizara kupitia taasisi zake na kwa kushirikiana na wadau katika mwaka 2025/2026 imezalisha na kusambaza miche 37,502,071 kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku katika mikoa ya uzalishaji. Kati ya hiyo, miche ya kahawa ni 27,702,090, mkonge 2,480,000, chai 1,634,250, parachichi 533,316, korosho 4,444,580, zabibu 342,000, migomba 314,412, kakao 40,044, karafuu 5,470, chikichi 4,491 na miembe 1,418. Aidha, pingili za muhogo 5,124,429 zimesambazwa kwa wakulima katika mikoa ya Kigoma, Kagera, Morogoro, Mwanza na Pwani.



*Mhe: Daniel G. Chongolo (Mb), Waziri wa Kilimo akikagua kitalu cha uzalishaji wa miche ya korosho – TARI Naliendele*

### 4.1.3 Uwekezaji kwenye Utoaji wa Ruzuku ya Mbolea na Viuatilifu

#### a) Upatikanaji wa Mbolea

86. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Wizara kupitia TFRA ilipanga kuratibu upatikanaji wa tani 1,500,000 za mbolea. Kati ya hizo, TFC ilipanga kununua na kusambaza mbolea tani 200,000 kwa ajili ya mazao ya chakula; kununua mbolea tani 133,000 kwa ajili ya zao la tumbaku na tani 500 kwa ajili ya zao la chai. Vilevile, Wizara

ilipanga kununua tani 200,000 za mbolea na chokaa mazao tani 50,000 katika viwanda vya ndani. Pia, kuanza ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha mbolea aina ya *Triple SuperPhosphate* – (TSP) na kuanzisha mradi wa kuchimba, kufungasha na kusambaza chokaa mazao katika eneo la Visiga Mkoa wa Pwani.

87. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi Machi 2026, Wizara imetekeleza yafuatayo:-

88. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu upatikanaji wa mbolea nchini ili kuwawezesha wakulima kupata na kutumia mbolea kwa lengo la kuongeza uzalishaji na tija ya mazao ya kilimo. Hadi Machi 2026, Wizara kupitia TFRA imeratibu upatikanaji wa tani 1,254,203 sawa na asilimia 83.61 ya lengo la tani 1,500,000 katika mwaka 2025/2026. Kati ya kiasi kilichopatikana, tani 150,686 zimezalishwa ndani ya nchi, tani 869,840 zimeingizwa kutoka nje ya nchi na tani 233,677 ni bakaa ya msimu uliopita.

89. ***Mheshimiwa Spika,*** kati ya kiasi kilichopatikana, tani 674,686.24 za mbolea zenye thamani ya Shilingi 1,210,737,644,482 zimesambazwa kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku katika mikoa yote na usambazaji unaendelea. Kati ya kiasi hicho, Shilingi 929,155,586,025 ni mchango wa wakulima na Shilingi 281,582,058,457 ni ruzuku ya Serikali. Hatua hiyo imeongeza

kiwango cha matumizi ya mbolea kutoka kilo 19 za virutubisho mwaka 2021/2022 hadi kufikia wastani wa kilo 27 za virutubisho kwa hekta mwaka 2025/2026 ambayo ni sawa na asilimia 54 ya lengo la kilo 50 za virutubisho kwa hekta kulingana na azimio la CAADP.

90. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuiwezesha Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC) ili kuongeza upatikanaji wa mbolea nchini. Katika kutekeleza hilo, TFC imenunua tani 150,618 za mbolea, ambapo tani 126,345 zimesambazwa kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku. Aidha, kati ya tani za mbolea zilizosambazwa, tani 69,751 ni kwa ajili ya mazao ya chakula na tani 56,594 ni kwa ajili ya tumbaku. Vilevile, ili kupunguza gharama za mbolea na uzalishaji wa mazao, TFC imenunua malori matano (5) yenye uwezo wa kubeba tani 10 kila moja kwa ajili ya kuwezesha usambazaji wa mbolea kwenda vijijini.

91. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha uhifadhi wa mbolea nchini kwa lengo la kuwa na mbolea yenye ubora na ya kutosha, Wizara kupitia TFC imekarabati ghala za kuhifadhi mbolea zilizopo katika mikoa ya Njombe (tani 18,000) na Ruvuma (tani 15,000). Ukarabati wa ghala hizo utaongeza uwezo wa uhifadhi na upatikanaji wa mbolea katika mikoa ya Njombe na Ruvuma.

92. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza uzalishaji wa mbolea ndani ya nchi, usimikaji wa mitambo ya kuchanganya mbolea (Bulk Blending Facilities) katika Mkoa wa Dar es Salaam yenye uwezo wa kuchanganya tani 120 kwa saa, sawa na tani 300,000 kwa mwaka umefikia asilimia 50. Aidha, TFC kwa kushirikiana na TFRA imesaini mkataba wa awali na wazalishaji wa ndani wa mbolea nchini ili kuwawezesha kuzalisha tani 200,000 za mbolea na tani 50,000 za chokaa mazao.

93. ***Mheshimiwa Spika,*** pia, TFC imepata eneo lenye ukubwa ekari 97.3 katika eneo la viwanda lililopo Amboni, Kata ya Mzizima Mkoa wa Tanga, kwa ajili ya kuanzisha mradi wa kiwanda cha kuchimba, kufungasha na kusambaza chokaa mazao.




*Mkurugenzi wa Kampuni ya Mbolea Bw. Samuel Mshote akiwa Bandari ya Dar es salaam akisimamia zoezi la ufungaji wa mbolea za TFC*

94. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kutumia nafasi hii kuzishukuru kampuni zilizoanzisha viwanda vya kutengeneza mbolea hapa nchini kwa uwekezaji wao ambao umechangia kufikiwa kwa mafanikio tunayojivunia katika sekta ya kilimo mazao. Kwa namna ya kipekee ninaishukuru Halmashauri ya Wilaya ya Kinondoni kwa kuanzisha Kiwanda cha Mboji Mabwepande na Halmashauri ya Wilaya ya Moshi kwa kuanzisha Kiwanda cha Moshi Composit vinavyotengeneza mbolea hai kwa kutumia taka zilizooza. Mchango wao si tu unalenga kuimarisha uzalishaji na tija ya mazao ya kilimo bali unalenga pia kutunza na kuhifadhi mazingira.

> ***Ninatoa rai kwa Halmashauri nyingine nchini kuiga mfano huo kwa kuwekeza kwenye viwanda vya kutengeneza mbolea hai kwa kutumia fursa ya taka ozo ambazo zinapatikana kwa wingi katika maeneo yao. Ikiwa na lengo pia la kusafisha na kutunza mazingira. Kwa mfano Jiji la Dar Es Salaam kwenye dampo la Pugu, kwanza itasaidia kupunguza taka na kuzalisha mbolea hai.***

### b) Upatikanaji wa Viuatilifu na Udhibiti wa Visumbufu vya Mazao na Mimea

95. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2025/2026, ilipanga kununua lita 125,500 za viuatilifu kwa ajili ya kudhibiti milipuko ya visumbufu vya mimea na mazao. Vilevile, ilipanga kununua ndege moja (1) na ndege nyuki 20; kuzalisha wadudu rafiki na kusajili viuatilifu hai; kujenga Ofisi za TPHPA Makao Makuu; kukagua maduka 4,000 ya viuatilifu; na kuanzisha vituo vya kilimo anga katika mikoa ya Mwanza, Dodoma na Mbeya.

96. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi Machi 2026, Wizara kupitia TPHPA imepata mzabuni kwa ajili ya ununuzi wa lita 58,757 za viuatilifu vya kudhibiti milipuko ya visumbufu vya mimea na mazao. Viuatilifu hivyo vinajumuisha lita 8,500 kwa ajili ya kudhibiti kwelea kwelea, lita 780 kwa ajili ya kudhibiti nzige, lita 46,227 kwa ajili ya kudhibiti viwavijeshi vamizi na lita 750 kwa ajili ya kudhibiti nzi wa matunda na kilogramu 2,500 kwa ajili ya kudhibiti panya.

97. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha udhibiti wa visumbufu vya mlipuko, Wizara kupitia TPHPA imeendelea kuwekeza katika upatikanaji wa vifaa na teknolojia ya udhibiti kwa njia ya anga. Katika kuhakikisha hilo, mzabuni kwa ajili ya ununuzi wa ndege nyuki

20 za udhibiti wa visumbufu vya mimea na mazao amepatikana.

98. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, imekamilisha usajili na kibali cha kuruka kwa ndege iliyonunuliwa ili kutoa huduma za kudhibiti visumbufu vya mimea na mazao mfano kwelea kwelea na nzige badala ya kutegemea ndege kutoka nje ya nchi. Ndege hiyo aina ya *Thrush 510P2+* ina uwezo wa kubeba lita 1,930 za viuatilifu pamoja na mbolea au mbegu mita za ujazo 1.9. Pia, ndege hiyo inauwezo wa kunyunyuzia viuatilifu kwenye eneo lenye ukubwa wa takriban hekta 3,000 kwa siku.

99. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha udhibiti wa visumbufu vya mazao na mimea kwa njia ya kibailojia kwa lengo la kupunguza matumizi ya viuatilifu vya viwandani, Wizara kupitia TPHPA imezalisha wadudu rafiki takriban 21,000 aina ya *Trichogramma* na *Telenomus remus spp*. kwa ajili ya udhibiti wa viwavijeshi vamizi; *Diadegma spp*. na *Cotesia spp*. kwa ajili ya kudhibiti nondomgongo almasi (DBM) ambao hushambulia mazao ya bustani aina ya kabichi na spinachi na funza wa mashina; na *Cyrtobagous salviniae* kwa ajili ya kudhibiti gugu la kariba na minyoo rafiki (EPNs) aina ya *Steinernema spp*. na *Heterorhabditis spp*. kwa ajili ya udhibiti wa viwavijeshi vamizi (Fally Armyworm), nondomgongo almasi (DBM) na funza wa *White grub.* Aidha

jumla ya wakulima 2,300 na maafisa ugani 39 wamepatiwa mafunzo kuhusu udhibiti wa visumbufu vya mimea kwa njia ya kibaolojia.

100. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na uwepo wa viuatilifu bandia na chakavu nchini ambavyo vinaweza kusababisha madhara kwa wananchi, wanyama na mazingira. Wizara kupitia TPHPA, ilifanya mapitio ya kina ya viuatilifu vilivyosajiliwa nchini na kuainisha viuatilifu hatarishi vinavyoweza kusababisha madhara kwa binadamu, wanyama na mazingira. Wizara imeviondoa viuatilifu 130 vilivyobainika kuwa na viambata hatarishi na imebaini viuatilifu 675 ambavyo usajili wake haukuhuishwa. **Kiambatisho Na. 2**. Orodha ya viuatilifu vilivyoondolewa sokoni.

101. ***Mheshimiwa Spika,*** TPHPA imekagua maduka 1,404 na ghala 41 za viuatilifu na kubaini kuwa leseni za uendeshaji wa maduka 59 zimeisha muda. Hivyo, maduka hayo yamesitishiwa utoaji wa huduma hadi watakapohuisha leseni za uendeshaji wa maduka hayo.

***Nitoe rai kwa wafanyabiashara wa viuatilifu nchini kuhakikisha wanafuata Sheria, taratibu na kanuni inayosimamia biashara ya viuatilifu nchini. Serikali haitasita kuchukua hatua kali za kisheria kwa mfanyabiashara atakayeuza viuatilifu visivyothibitishwa, visivyokidhi ubora au kufanya biashara ya viuatilifu bila ya***

***vibali ili kuwalinda wananchi, wanyama na mazingira.***

### 4.1.4 Usajili wa Wakulima na Urasimishaji wa Shughuli za Kilimo

102. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2025/2026 ilipanga kuendelea kurasimisha shughuli za kilimo kwa kusajili wakulima, wafanyabiashara wa mazao ya kilimo, watoa huduma za ugani, ghala na pembejeo za kilimo. Vilevile, Wizara kupitia TFRA ilipanga kuendelea kutoa hatimiliki na kadi za kielektroniki (smart card) kwa wakulima 10,000.

103. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi Machi 2026, wakulima 686,794 wamesajiliwa katika mfumo wa kielektroniki wa Ruzuku ya Pembejeo (Agricultural Inputs Subsidy System) na kufanya idadi ya wakulima waliosajiliwa kufikia 5,433,147 kati ya hao, wanawake 1,942,869 na usajili unaendelea. Kati ya waliosajiliwa, wakulima 12,833 kati ya hao wanawake 3,191 wamepewa hatimiliki na kadi za kielektroniki (smart card) kwa ajili ya kuwawezesha kupata huduma mbalimbali ikiwemo ununuzi wa pembejeo. Aidha, utoaji wa hatimiliki na kadi za kieletroniki unaendelea.

104. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha usambazaji wa mbolea kwa wakulima nchini, Wizara kupitia TFRA imesajili katika mfumo wa

kielektroniki (Agricultural Inputs Subsidy System) waagizaji (Kampuni za mbolea) 70, mawakala wa mbolea 8,785 na Vyama vya Ushirika 2,571 kuwa mawakala wa mbolea. Pia, jumla ya vituo 14,480 vya mauzo ya mbolea vimefunguliwa katika mikoa yote nchini. Kadhalika, wafanyabiashara wa mazao ya kilimo 2,452 wamesajiliwa kwa lengo la kuwatambua na kuimarisha usimamizi wa biashara za mazao.

105. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha viwango vya kitaalamu, ushirikiano na wakulima, ufuatiliaji na uwajibikaji kwa Maafisa ugani nchini unaimarishwa, Wizara imesajili watoa huduma za ugani 8,472. Kati ya hao, 6,618 ni Maafisa Ugani wa Serikali na 1,854 ni Maafisa Ugani wa sekta binafsi na usajili unaendelea.

***Nitoe rai kwa maafisa ugani wa sekta binafsi kuendelea kujisajili katika mfumo ili kutambulika na kuendelea kutoa huduma kwa wakulima wakiwa rasmi***.

106. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuratibu hifadhi ya chakula nchini na kuboresha miundombinu ya uhifadhi, Wizara imesajili ghala 2,431. Kati ya hizo, ghala 637 ni za Serikali na ghala 1,794 ni za sekta binafsi na usajili unaendelea.

### 4.1.5 Kuwekeza kwenye Ujuzi kwa Wataalam wa Ndani

107. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2025/2026, ilipanga kuwawezesha watumishi 151 kupata mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika vyuo vya ndani na nje ya nchi. Ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi Machi 2026, watumishi 583 wamepatiwa mafunzo mbalimbali ili kuendana na mahitaji ya taaluma. Kati ya hao, watumishi 71 wamejiunga na mafunzo ya muda mrefu na watumishi 512 ni wa mafunzo ya muda mfupi. Aidha, watumishi wanaohudhuria mafunzo ya muda mrefu wamegawanyika katika makundi yafuatayo:- Shahada ya uzamivu 43, Shahada ya uzamili 23, Shahada ya kwanza wawili (2) na Stashahada watatu (3).

### 4.1.6 Uwekezaji kwenye Huduma za Ugani

108. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Wizara ilipanga kununua na kusambaza vitendea kazi kwa Maafisa Ugani ikiwemo magari 100, vishikwambi 3,000 na mavazi maalum ya utambulisho 5,000; kuendelea na ujenzi wa miundombinu kwenye viwanja vya maonesho ya wakulima vya Dkt. John Samuel Malecela (Dodoma) na John Mwakangale (Mbeya); na kuanza ujenzi wa uzio katika viwanja vya Ipuli (Tabora). Aidha, Wizara ilipanga kukamilisha taratibu za uanzishaji wa Wakala wa Huduma za Ugani wa Taifa (NAESA) na kuanzisha mfumo wa huduma za ugani wa kidijiti ili

kuwezesha upatikanaji wa huduma za ugani kwa sekta binafsi.

109. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilipanga kujenga nyumba 50 za Maafisa Ugani; kuendelea kuimarisha vituo vinane (8) mahiri vya usambazaji na uhaulishaji wa teknolojia; kushirikiana na VETA na CAMARTEC kutoa mafunzo kuhusu uhaulishaji na matumizi ya teknolojia za zana za kilimo; kukarabati miundombinu ya vituo vya uhaulishaji wa teknolojia za kilimo; kujenga miundombinu ya Chuo cha Taifa cha Sukari Kidatu; kutoa mafunzo kwa wakulima 20,000; kutoa mafunzo rejea kwa Maafisa Ugani 7,000; na kugharamia mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi 1,920 wa ngazi ya Stashahada.

110. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi Machi 2026 Wizara imetekeleza yafuatayo:-

111. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima nchini, Wizara imeanza ununuzi wa vitendea kazi kwa Maafisa Ugani ambapo magari 18 kati ya 60 yamenunuliwa. Vilevile, taratibu za ununuzi wa vishikwambi na mavazi maalum ya Maafisa Ugani zinaendelea. Aidha, ujenzi wa awamu ya kwanza ya miundombinu kwenye viwanja vya maonesho vya Nanenane vya Dkt. John Samuel Malecela - Dodoma umefikia

asilimia 75 na katika viwanja vya John Mwakangale – Mbeya umefikia asilimia 12. Kukamilika kwa ujenzi wa viwanja hivyo kutawezesha kutoa mafunzo kwa wakulima na wadau wengine kwa mwaka mzima. Aidha, maboresho ya viwanja vingine yanaendelea.

112. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha utoaji wa huduma za ugani, Wizara inaendelea kukamilisha taratibu za kuanzisha Wakala ya Taifa wa Huduma za Ugani Kilimo (National Agricultural Extension Services Agency - NAESA) ambao inatarajiwa kuanza rasmi tarehe 01 Julai, 2026. Wakala huo, utawezesha kuongeza ufanisi wa huduma za ugani, kuratibu na kusimamia shughuli za ugani na kuhaulisha teknolojia kutoka kwa watafiti na wadau wengine kwenda kwa Maafisa Ugani na wakulima. Pamoja na uanzishaji wa NAESA, Wizara imeendelea kuboresha mfumo wa kutoa huduma za ugani kidijiti ambao umewawezesha wakulima kutumia simu za mkononi kupata ushauri wa kitaalam kuhusu uendelezaji wa mazao ya kilimo nchini.

113. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha vituo mahiri vya uhaulishaji wa teknolojia za kilimo vya TARI kwa kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika vituo viwili (2) vya Dkt. John Samuel Malecela - Dodoma na Mwl. Julius Kambarage Nyerere – Morogoro. ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika vituo sita (6) vya uhaulishaji na

usambazaji wa teknolojia katika viwanja vya Fatuma Mwasa - Tabora, John Mwakangale - Mbeya, Nyakabindi - Simiyu, Nyamuhongolo - Mwanza, Themi - Arusha na Ngongo – Lindi umefikia wastani wa asilimia 20. Hatua hiyo itawawezesha wakulima na watoa huduma za kilimo kupata ujuzi na maarifa kuhusu kilimo kwa kipindi cha mwaka mzima.

114. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi wa maafisa ugani ambapo ujenzi wa nyumba 29 za Maafisa Ugani katika mikoa ya Kigoma, Pwani, Tanga, Singida, Tabora, Mbeya, Kilimanjaro, Njombe, Ruvuma, Shinyanga, Arusha, Dar es Salaam, Songwe na Simiyu umekamilika. Aidha, ujenzi wa nyumba 21 umefikia wastani wa asilimia 90 na fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 34 katika mikoa 19 zimepelekwa katika Halmashauri husika ili kuanza ujenzi. Ujenzi wa nyumba hizo utawezesha upatikanaji wa huduma za ugani kwa wakati, kujenga uhusiano wa karibu na wakulima, kupunguza gharama za uendeshaji na kuongeza hamasa na ari ya kazi. Vilevile, jitihada za kuimarisha matumizi ya vituo vya Rasilimali za Kilimo vya Kata zinaendelea ikiwemo kutumika kama vituo vya zana jumuishi za kilimo na mafunzo kwa wakulima.

115. ***Mheshimiwa Spika,*** pia, Wizara kwa kushirikiana na sekta binafsi imetoa mafunzo kuhusu uhaulishaji na matumizi sahihi ya zana za kilimo kwa wasimamizi na waendesha mitambo 662 katika mikoa 17 ya Tanzania. Katika kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia, Wizara inaendelea na ukarabati wa miundombinu ya Kituo cha Mafunzo kwa Wakulima Mkindo ambapo ukarabati umefikia asilimia 55. Kadhalika, wakandarasi kwa ajili ya kuanza ukarabati wa miundombinu katika Vyuo vya Mafunzo ya Kilimo vya Igurusi na Mlingano wamekabidhiwa maeneo kwa ajili ya kuanza kazi. Pia, mkandarasi kwa ajili ya kuanza ujenzi wa bweni la kisasa la Chuo cha Taifa cha Sukari Kidatu amekabidhiwa eneo kwa ajili ya kuanza ujenzi.

116. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imetoa mafunzo kwa wakulima 23,444 kuhusu uzalishaji wa mazao ya kilimo kibiashara kupitia vituo vya mafunzo ya kilimo; na mafunzo rejea kwa Maafisa Ugani 1,753 kuhusu utoaji wa huduma za ugani kidijiti kupitia *e-kilimo*. Aidha, wanafunzi 2,075 wa ngazi ya Astashahada na Stashahada wamegharamiwa mafunzo kwa vitendo katika Vyuo vya Mafunzo ya Kilimo.

### 4.1.7 Kupima Afya ya Udongo kwa Wakulima Wadogo na Wakubwa

117. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2025/2026, Wizara ilipanga kuendelea na upimaji wa afya ya udongo na kuchora ramani za kidijiti zinazoonesha hali ya afya ya udongo; kununua na kusambaza *soil scanner* 43; na kujenga ofisi tatu (3) za usimamizi na mipango ya matumizi ya ardhi ya kilimo.

118. ***Mheshimiwa Spika***, ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, Wizara imetekeleza yafuatayo:-

119. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuwawezesha wakulima kujua aina sahihi ya mbolea ya kutumia na mazao yanayotakiwa kupandwa kwenye maeneo yao, Wizara inaendelea na upimaji wa afya ya udongo nchini. Ili kutekeleza lengo hilo, Wizara imekusanya sampuli za udongo katika eneo la kilimo lenye ukubwa wa hekta 30,261,888.47 katika mikoa 15. Hatua hii imewezesha kuongezeka kwa eneo lililochukuliwa sampuli kufikia hekta 40,134,605.80 katika mikoa 19 ya Singida, Shinyanga, Dodoma, Simiyu, Geita, Mwanza, Mara, Kagera, Kigoma, Lindi, Pwani, Mtwara, Morogoro, Tabora, Tanga, Arusha, Manyara, kilimanjaro na Ruvuma. Aidha, uchukuaji wa sampuli unaendelea katika mikoa iliyobaki ya Tanzania Bara, na ukamilishaji wa ramani za awali za afya ya

udongo unaendelea. Mchanganuo wa maeneo yaliyochukuliwa sampuli za afya ya udongo unapatikana katika **Kiambatisho Na. 3**.



*Maafisa kutoka wizara ya kilimo kwa kushirikiana na Maafisa kutoka TARI wakichukua sampuli ya udongo kwa ajili ya utafiti, katika Mkoa wa Singida*

120. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha utoaji wa huduma ya upimaji wa afya ya udongo kwa kila Halmashauri nchini, Wizara imetangaza, zabuni kwa ajili ya ununuzi wa vipima afya ya udongo (soil scanner) 43. Sambamba na upimaji wa afya ya udongo, Wizara imebaini uwepo wa tindikali katika udongo kwenye baadhi ya maeneo inayoathiri

tija na uzalishaji wa mazao ya kilimo. Hivyo, Wizara imetoa mafunzo kuhusu kurejesha afya ya udongo kwa Maafisa Ugani 185 na wakulima 18,749 katika mikoa ya Njombe, Iringa na Katavi ikiwa ni maeneo ya majaribio kupitia **Mradi wa Ruzuku Makini kwa kutumia chokaa mazao**.

121. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha miundombinu kwa ajili ya huduma za usimamizi na matumizi sahihi ya ardhi ya kilimo kwa wakulima, Wizara inaendelea na usanifu wa michoro kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za Usimamizi na Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Kilimo katika Kanda ya Ziwa (Mwanza) na Mashariki (Morogoro).

#### 4.1.8 Uendelezaji wa Kilimo cha Umwagiliaji

122. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji katika mwaka 2025/2026 ilipanga kuendelea na utekelezaji wa miradi 768 kati ya 780 iliyoanza kutekelezwa mwaka 2022/2023 hadi 2024/2025. Miradi hiyo inahusisha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika skimu mpya 60 (hekta 147,433.46); ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji katika skimu 41 (hekta 72,175); ujenzi wa mabwawa 19 (mita za ujazo 326,449,973); kuanza ujenzi wa mabwawa 28 (mita za ujazo 487,361,277); kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa

mabwawa 65; ujenzi wa skimu katika mabonde 14 ya kimkakati na kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mabonde nane (8).

123. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, ilipanga kujenga miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba matatu (3) ya Membe, Ndogowe na Chinangali; kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mashamba matatu makubwa katika mikoa ya Kigoma, Kagera na Njombe; na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa skimu 429 na kuanza ujenzi/ukarabati wa skimu 98 ambazo upembuzi na usanifu umekamilika.

124. ***Mheshimiwa Spika,*** pia, Tume ilipanga kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mabonde ya mto Ngono na Bugwema yenye jumla ya hekta 22,770; kuendelea na ujenzi wa mabwawa ya Mbakiamtuli na Ngorongo katika bonde la Rufiji yenye jumla ya mita za ujazo 57,548,653; kuanzisha mfumo wa usimamizi wa mashamba ya Mbarali Estate (ekari 6,437.5), Membe (ekari 2,500), Bugwema (ekari 7,500), Madibira (ekari 8,000) na Lumpungu (ekari 18,045); na kujenga mabwawa mawili (2) ya Dudumizi na Mambi katika shamba la Mbarali Estate.

125. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wizara ilipanga kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na kuanza ujenzi wa miradi ya umwagiliaji kwa ajili ya kutumia maji ya Ziwa Victoria na Tanganyika kwa shughuli za kilimo; kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa sita (6); kukamilisha ujenzi wa Ofisi ya Umwagiliaji ya Makao Makuu; kuendelea na ujenzi wa Ofisi za mikoa 19 na Wilaya 13 na ukarabati wa ofisi nne (4) za mikoa; kununua pikipiki 100, magari 30 na mitambo mitatu (3); na kujenga maabara moja (1) ya uhakiki wa ubora wa ujenzi katika Mkoa wa Dodoma.

126. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume ilipanga, kutoa mafunzo ya uendeshaji, usimamizi na matunzo ya miundombinu ya umwagiliaji kwa wakulima viongozi 3,000 na kusajili Vyama vya Umwagiliaji 300.

127. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imetekeleza yafuatayo:-

**Ujenzi na ukarabati wa skimu na mabwawa**

128. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume imekamilisha ujenzi wa miradi 28 ya umwagiliaji inayohusisha ujenzi wa skimu mpya 10 zenye uwezo wa kumwagilia eneo

lenye ukubwa wa hekta 10,300; ukarabati wa skimu tisa (9) zenye uwezo wa kumwagilia ukubwa wa hekta 10,760; na ujenzi wa mabwawa saba (7) yenye mita za ujazo milioni 53.2 yenye uwezo wa kumwagilia eneo lenye ukubwa wa hekta 10,141. Pia, ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika shamba la Ndogowe (hekta 2,000) na Chinangali I (hekta 88) umekamilika. Miradi iliyokamilika itanufaisha jumla ya wakulima 98,500 kwa kuwawezesha kulima kwa kipindi chote cha mwaka.

129. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Tume inaendelea na ujenzi wa miradi 118 ambapo, kati ya hiyo miradi 18 utekelezaji umefikia zaidi ya asilimia 50; miradi 52 utekelezaji upo chini ya asilimia 50 na miradi 48 ipo katika hatua za awali za utekelezaji. Orodha ya miradi ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji iliyotekelezwa imeoneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 4.**

**Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa skimu na mabwawa**

130. ***Mheshimiwa Spika***, Tume imekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa skimu 120, mabwawa 51, mabonde ya kimkakati 15 na mashamba ya pamoja matatu (3). Vilevile, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa sita (6) ya Dabalo, Buigiri, Hombolo, Kimagai, Kidete na

Ikowa umefikia wastani wa asilimia 25. Mabwawa hayo yatatumika kuzuia mafuriko katika reli ya kati na kutumika katika shughuli za kilimo cha umwagiliaji.

131. ***Mheshimiwa Spika****,* vilevile, Tume imekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa skimu mbili (2) za Mbakiamtuli na Ngorongo kati ya skimu sita (6) zilizopo katika bonde la Rufiji ambapo zabuni kwa ajili ya kuwapata wakandarasi wa ujenzi wa skimu hizo zimetangazwa. Aidha, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa skimu zilizobaki katika bonde la Rufiji pamoja na mabonde ya Manonga – Wembere, Ruhuhu, Malagarasi, Kalilankululu, Songwe na Kiru – Magara umefikia wastani wa asilimia 54.3. Kadhalika, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa skimu 389 umefikia wastani wa asilimia 36 na mabwawa 49 umefikia wastani wa asilimia 38. Orodha ya miradi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina imeoneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 5.**

132. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume imekamilisha taratibu za umiliki wa Shamba la Bugwema na kupata hatimiliki ya shamba hilo. Aidha, mkandarasi amekabidhiwa shamba kwa ajili ya kuanza ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji. Vilevile, mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa skimu katika bonde la Mto Ngono amepatikana.

133. ***Mheshimiwa Spika,*** kadhalika, Wizara kupitia Tume imeingia makubaliano na Halmashauri ya Kibondo kuhusu ujenzi, uendeshaji na usimamizi wa Shamba la Lumpungu. Aidha, mkandarasi wa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika shamba hilo amepatikana. Pia, tathmini ya shamba la Mbarali Estate imekamilika na taratibu za malipo ya fidia zinaendelea. Vilevile, Tume imehamasisha uanzishwaji wa umoja wa wakulima kwa ajili ya uendeshaji na usimamizi wa shamba la Membe.

134. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kuhakikisha kuwa wakulima wa nchi hii wananufaika na rasilimali ya maji iliyopo kwa ajili ya shughuli za kilimo ili kuongeza uzalishaji na kukuza Uchumi wao. Katika kufanikisha azma hiyo, Wizara inaendelea kushirikiana na Wizara ya Maji kuhakikisha azma ya Serikali ya kutumia maji ya Ziwa Victoria na Tanganyika kwa ajili ya shughuli za umwagiliaji inatekelezwa. Kukamilika kwa ujenzi wa mradi huo utanufaisha wakulima wa mikoa 12 ya Simiyu, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Kigoma, Mwanza, Geita, Mara, Kagera, Rukwa na Katavi, Wilaya 69, Kata 192 na Vijiji 943.

135. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa ofisi ya Makao Makuu ya Tume iliyopo Mkoa wa Dodoma - Njedengwa umefikia asilimia 98; ujenzi wa ofisi nne (4) za mikoa ya Kilimanjaro,

Kigoma, Iringa na Songwe umefikia wastani wa asilimia 10.5; na ujenzi wa ofisi 14 za wilaya za umwagiliaji katika wilaya za Chamwino (1), Mbulu (2), Ngorongoro (1), Tunduru (1), Morogoro (1), Chalinze (1), Momba (1), Musoma (1), Igunga (1), Nzega (1), Kwimba (1), Uyui (1) na Masasi (1) umefikia wastani wa asilimia 13.8. Aidha, Tume imenunua *supporting truck* 16 na *semi trailer* mbili (2) kwa ajili ya kubeba vifaa vya uchimbaji wa visima. Usanifu kwa ajili ya ujenzi wa maabara ya uhakiki wa ubora wa ujenzi katika Mkoa wa Dodoma umekamilika.

136. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume imetoa mafunzo ya uendeshaji, usimamizi na matunzo ya miundombinu ya umwagiliaji kwa wakulima 2,073 katika skimu 13. Aidha, Tume imesajili Vyama vya Umwagiliaji 99 na kufanya jumla ya vyama vilivyosajiliwa kufikia 1,013.

### 4.1.9 Uanzishaji wa Vituo vya kutoa Huduma na Ununuzi wa Zana za Kilimo

137. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Wizara ilipanga kuanzisha vituo 1,000 vya kutoa huduma ya zana za kilimo kwa wakulima; kununua trekta 10,000, *power tiller* 10,000 na mashine za kuvunia na kukaushia; na kutoa mafunzo kuhusu uendeshaji na usimamizi wa zana za kilimo kwa waendesha mitambo, wasimamizi wa vituo na watoa huduma 500.

138. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, Wizara imeanzisha vituo 79 vya kutoa huduma ya zana za kilimo kwa wakulima ambapo trekta 360 na zana zake zimesambazwa katika vituo hivyo na kuanza kutoa huduma kwa wakulima. Aidha, Wizara imenunua mashine mbili (2) zenye uwezo wa kukausha mazao ya nafaka (mahindi na mpunga) tani 10 kwa saa na kuzisimika katika mikoa ya Mbeya (Mbarali) na Tanga (Korogwe).

139. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha usimamizi na utendaji kazi wa zana za kilimo zilizosambazwa, Wizara imeweka dirisha katika mfumo wa *e - Kilimo* kwa ajili ya kufuatilia utendaji kazi wa zana za kilimo katika vituo vya kutoa huduma za zana za kilimo ili kuhakikisha kuwa zana hizo zinatumika kwa ufanisi katika shughuli za kilimo. Aidha, kupitia mfumo huo, wakulima wataweza kuomba huduma za zana za kilimo, kufanya malipo ya huduma na kutoa taarifa ya utendaji kazi wa zana za kilimo ikiwemo masaa ya kazi na ukubwa wa eneo lililohudumiwa.

140. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuleta ufanisi na uendelevu wa matumizi ya zana hizo katika vituo vilivyanzishwa na vitakavyoanzishwa, Wizara imeandaa Mwongozo wa Uendeshaji wa Vituo vya Kutoa Huduma za zana za Kilimo kwa wakulima. Mwongozo huo utatumika kama

nyenzo ya uendeshaji na usimamizi wa vituo hivyo.

**Mkutano wa Afrika wa Matumizi Endelevu ya Zana za Kilimo**

141. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhamasisha matumizi ya zana za kilimo nchini, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Chakula na Kilimo (FAO) iliratibu mkutano wa kwanza wa Afrika wa Matumizi Endelevu ya Zana za Kilimo uliofanyika Februari 3 - 6, 2026, Jijini Dar es Salaam. Pamoja na mambo mengine wakati wa Mkutano huo, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa, Dkt. Mwigulu L. Nchemba (Mb). alizindua Mkakati wa Pili wa Taifa wa Zana za Kilimo wa Mwaka 2025/2026 – 2035/2036 ambao umeweka Dira inayoonesha malengo na maeneo ya kipaumbele katika kuendeleza matumizi ya zana za kilimo nchini. Pia, Mkutano huo uliazimia mambo yafuatayo:-

a. Kuimarisha mifumo ya utoaji wa huduma za zana za kilimo ikijumuisha upatikanaji wa vipuri, matengenezo pamoja na huduma baada ya mauzo kwa kuzingatia mahitaji ya soko;

b. Kuimarisha majukwaa ya kubadilishana maarifa kwa kuunganisha taasisi za utafiti,

watekelezaji, sekta binafsi na watunga Sera ili kubadilishana uzoefu wa maamuzi ya utekelezaji na Sera; na

c. Kuimarisha ushiriki wa vijana na wanawake katika huduma za zana za kilimo kupitia maendeleo ya ujuzi yanayolenga upatikanaji wa mitaji na teknolojia zinazorahisisha kazi ili kuchangia ajira zenye staha.



*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb) akikabidhi ndege nyuki Wizara ya Kilimo*

### 4.1.10 Kuendeleza Shoroba za Kilimo na Uzalishaji

142. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo ilipanga kuendelea kuimarisha shoroba nne (4) za kuendeleza kilimo Tanzania (AGCOT) kulingana na ikolojia za kilimo.

143. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, katika mwaka 2025/ 2026, Ofisi ya Mageuzi ya Kilimo (ATO) imeendesha na kuratibu mikutano ya uhamasishaji wa uendelezaji wa shoroba mpya tatu (3) za Kati, Kaskazini na Mtwara. Lengo kuu la mikutano hiyo ni kujenga uelewa wa pamoja kwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakurugenzi wa Halmashauri, Madiwani, sekta binafsi, na wadau wengine kuhusu dhana ya Shoroba za Kilimo. Kupitia mikutano hiyo, ATO imeimarisha ushiriki wa wadau, kuboresha uratibu wa utekelezaji katika ngazi za mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, na kuhakikisha shoroba zinakuwa kichocheo cha mageuzi ya kilimo nchini.

144. ***Mheshimiwa Spika,*** pia, Wizara kupitia ATO imeandaa rasimu ya Mwongozo wa Uwekezaji, Miundombinu na Vipaumbele vya Mnyororo wa Thamani wa Mazao (Investment Blue Print) na Uwekezaji unaolenga Utunzanji

na Uhimilivu wa Mazingira (Investment Green Print). Miongozo hii inalenga kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi, washirika wa maendeleo, taasisi za fedha, ushirikishwaji wa Wizara zingine na taasisi zake.

**Uzalishaji wa Mazao kwa Mwaka 2025/2026**

145. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilipanga kuendelea kusimamia mikakati ya uzalishaji wa Mazao Asilia ya Biashara, Mazao ya Bustani, Mazao ya Chakula, Mazao ya Mafuta na mazao yenye mahitaji makubwa yanayoagizwa nje ya nchi ili kuongeza tija katika uzalishaji.

**Mazao Asilia ya Biashara**

146. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026 Wizara ilipanga kuongeza uzalishaji wa mazao asilia ya biashara ikiwemo pamba, kahawa, mkonge, korosho, tumbaku, pareto, kakao na chai kutoka jumla ya tani 1,451,694.11 zilizozalishwa mwaka 2024/2025 hadi tani 2,225,000.

147. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi Machi 2026, uzalishaji wa mazao asilia ya biashara umefikia tani 1,599,945.66 sawa na asilimia 71.9 ya lengo la kuzalisha tani 2,225,000 na ongezeko la asilimia 10.0 ikilinganishwa na tani 1,451,694,11 zilizozalishwa katika kipindi kama hicho

mwaka 2024/2025. Mchanganuo wa malengo na uzalishaji wa mazao asilia ya biashara umebainishwa katika **Jedwali Na. 5**.

**Jedwali Na. 5: Malengo na Uzalishaji wa Mazao Asilia ya Biashara (Tani) katika Mwaka 2025/2026**

| Na. | MAZAO | 2025/2026 | |
|---|---|---|---|
| | | Malengo | Uzalishaji |
| 1 | Korosho | 700,000 | 617,683.77 |
| 2 | Pamba | 400,000 | 222,014 |
| 3 | Pareto | 5,000 | 2,780* |
| 4 | Kahawa | 85,000 | 74,663.60 |
| 5 | Tumbaku | 200,000 | 185,776 |
| 6 | Chai | 40,000 | 11,631.48* |
| 7 | Mkonge | 80,000 | 64,321.77* |
| 8 | Sukari | 700,000 | 410,979.04 |
| 9 | Kakao | 15,000 | 10,096* |
| **JUMLA** | | **2,225,000** | **1,599,945.66** |

***Chanzo:*** *Wizara ya Kilimo 2026*
** Uzalishaji unaendelea*

## Zao la Pamba

148. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Pamba Tanzania ilipanga kuongeza uzalishaji wa zao la pamba kufikia tani 400,000 mwaka 2025/2026; kusambaza mbegu bora za pamba tani 28,000, chupa (acrepacks) 12,000,000 na vinyunyizi 100,000 kwa wakulima wa pamba; kununua mashine 20 za kupulizia viuatilifu; kuajiri Maafisa kilimo 2,000 kupitia programu ya BBT; kuzalisha na kusambaza kwa wakulima mbolea hai lita 12,000,000; na kununua na kusimika mtambo wa kuchakata

mbegu wenye uwezo wa kuchakata tani 15,000 kwa mwaka.

149. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi kwa kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika ilipanga kuratibu ufufuaji wa *Ginnery* mbili (2) zilizopo Mhunze na Uzogole; kushirikiana na MSD na vyama vya ushirika kuanzisha kiwanda cha kuchakata na kutengeneza pamba za hospitali na nyuzi kwa ajili ya kufungia tumbaku; kuanzisha kongani ya pamba (industrial park) katika Mkoa wa Simiyu; kuanza majadiliano na Wizara ya Nishati kuanzisha ruzuku ya umeme kwa kongani ya pamba; kuanza majadiliano na Wizara ya Fedha, Wizara ya Viwanda na Biashara na wadau wa pamba kutengeneza mfumo wa kodi (tax regime); kununua na kusimika mitambo miwili (2) ya kuzalisha nishati ya kupikia inayotokana na masalia ya miche ya pamba na mitambo minane (8) ya kusokota nyuzi za pamba na kuzalisha vikoi na mitandio. Pia, Bodi ilipanga kuboresha kituo cha mafunzo ya wakulima cha Nyakabindi.

150. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi Machi 2026, uzalishaji wa Pamba umefikia tani 222,014, sawa na asilimia 55.5 ya lengo la tani 400,000. Kutofikiwa kwa malengo ya uzalishaji kumetokana na mtawanyiko wa mvua usioridhisha katika maeneo ya uzalishaji hali iliyosababisha vitumba kudondoka. Aidha, kwa kiasi kikubwa uzalishaji

uliopatikana ulitokana na juhudi zilizofanyika za kusambaza pembejeo zenye thamani ya jumla ya Shilingi 61,825,419,000 kwa wakulima 510,919. Pembejeo hizo zinahusisha mbegu bora za pamba tani 21,051 sawa na asilimia 75.18 ya lengo la tani 28,000, chupa (acrepacks) 9,568,258 sawa na asilimia 80 ya lengo la chupa (acrepacks) 12,000,000 na vinyunyizi 80,000 sawa na asilimia 80 ya lengo la vinyunyizi 100,000. Aidha, katika kuongeza uzalishaji wa pamba hai inayozalishwa nchini, Bodi imesambaza mbolea hai lita 408,000 zenye uwezo wa kunyunyuzia hekta 10,200 kwa wakulima wa zao la pamba.

151. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi imenunua mashine 16 za kupulizia viuatilifu (self propelled boom sprayer) sawa na asilimia 80 ya lengo la kununua mashine 20. Mashine hizo zitawezesha wakulima kupunguza adha ya kunyunyuzia viuatilifu kwa kutumia vinyunyizi vya kubeba mgongoni. Vilevile, katika kuimarisha upatikanaji na utoaji wa huduma za ugani kwenye zao la pamba, Bodi kwa kushirikiana na kampuni zinazonunua pamba, imetoa ajira kwa Maafisa Ugani 761 kupitia programu ya BBT.



*Baadhi ya Vijana wa BBT ugani wakiwa na mashine ya kupulizia viuatilifu (self propelled boom sprayer) kwenye Zao la Pamba*

152. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha uongezaji thamani wa zao la pamba nchini Bodi, inaratibu upatikanaji wa eneo lenye ukubwa wa ekari 260 katika Halmashauri ya Itilima kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha kuchakata na kutengeneza pamba za hospitali na nyuzi kwa ajili ya kufungia tumbaku (cotton twine). Vilevile, tathmini ya awali ya uthaminishaji na uhakiki wa ardhi ya maeneo ya wananchi watakaolipwa fidia ili kupisha ujenzi wa kongani ya pamba (industrial park) imekamilika ambapo

jumla ya ekari 342.93 zitafidiwa kwa wananchi 190 katika Kijiji cha Nyamatara, Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi. Pia, eneo kwa ajili ya kusimika mtambo wa kuchakata mbegu za pamba limepatikana katika Halmashauri ya Igunga. Hatua hizo zinalenga kuongeza ajira kupitia uzalishaji wa zao la pamba, thamani na mauzo ya pamba iliyoongezwa thamani.

153. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi kwa kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika, imeanza taratibu za ufufuaji wa *Ginnery* ya Mhunze ambapo andiko la mradi kwa ajili ya kupata fedha za ufufuaji limewasilishwa Benki ya Ushirika Tanzania. Aidha, chama kikuu cha NYANZA kimeingia mkataba wa miaka mitatu (3) na Kampuni ya Mashati Oil Investiment kwa ajili ya kuendeleza *Ginnery* ya Uzogole. Uwepo wa *Ginnery* hizo utawawezesha wakulima wa pamba kuwa na soko la uhakika na kuongeza uzalishaji wa zao hilo.

154. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi kwa kushirikiana na *International Trade Centre-* ITC imenunua na kusambaza mashine tatu (3) kwa vikundi vya vijana na wanawake vilivyopo Halmashauri ya Ulanga. Mashine hizo zinatumika kusokota nyuzi za pamba; kutengeneza vikoi na mitandio.

**Zao la Chai**

155. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Wizara kupitia Bodi ya Chai Tanzania ilipanga kuongeza uzalishaji wa chai kavu kufikia tani 40,000; kutoa mafunzo kwa wakulima wadogo wa chai 8,000; kufufua mashamba ya chai yenye ukubwa wa hekta 56 katika Wilaya ya Kilolo; kujenga vituo sita (6) vya mizani kwenye maeneo mapya ya uzalishaji wa chai; kubadili mfumo wa uuzaji wa chai wa wakulima wadogo kutoka kuuza chai majani mabichi na kuanza kuuza chai nyeusi; kuwezesha shughuli za mnada wa chai Tanzania; kununua mashine mbili (2) za kuchakata na kuchanganya chai; kuanzisha viwanda sita (6) vya kuchakata chai kavu nyeusi na chai ya kijani; na kuendelea na majadiliano na wamiliki wa kiwanda cha Mvyulu.

156. ***Mheshimiwa Spika,*** pia, Bodi ilipanga kuwezesha upatikanaji wa hati ya kimataifa (ithibati) ya *Rain Forest Alliance* kwa wakulima wadogo wa chai; kuzalisha na kusambaza miche 2,350,000; kuanzisha maeneo mapya kwa ajili ya uzalishaji wa miche ya chai; na kujenga uzio katika ghala la kuhifadhia chai lililopo Kipawa.

157. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, uzalishaji wa chai kavu umefikia tani 11,631.48. Wizara kupitia Bodi ya Chai Tanzania inaendelea na juhudi za kuendeleza tasnia ya chai nchini, ambapo imeanzisha viwanda viwili (2) vyenye uwezo wa kuchakata tani 150 za chai kavu nyeusi kwa siku na viwanda viwili (2) vya kuchakata tani 20 za chai maalum kwa siku katika Wilaya za Kilolo na Njombe. Viwanda hivyo, vitachochea uzalishaji wa chai na kuimarisha bei ya chai ya mkulima.

158. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi imeendelea na majadiliano na wamiliki wa kiwanda cha Chai cha Lupembe na shamba lenye ukubwa wa ekari 200 katika Mkoa wa Njombe kwa ajili ya kulipa fidia ya kiwanda hicho chenye uwezo wa kuchakata tani 15 za majani mabichi kwa siku ili kurejeshwa na kuendeshwa na wakulima wadogo wa chai. Pia, imefufua mashamba ya chai yenye ukubwa wa hekta 34 katika Wilaya ya Kilolo na hekta 802 za Kampuni ya Eastern Usambara (EUTCO) katika Mkoa wa Tanga.

159. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha chai inayozalishwa nchini inakidhi viwango vinavyohitajika, Bodi imetoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha zao la chai kwa wakulima wadogo wa chai 24,183. Vilevile, imefanya tathmini kwa ajili ya ujenzi wa vituo

viwili (2) vya mizani kwenye maeneo mapya ya uzalishaji wa chai katika Wilaya ya Kilolo ili kuimarisha upimaji wa chai inayovunwa. Pia, imezalisha na kusambaza miche 246,870 ya chai katika Wilaya za Kilolo (64,870) na Mufindi (182,000).

160. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha bei ya chai kavu, Bodi ya Chai Tanzania pamoja na timu ya washauri elekezi inafanya mapitio ya mjengeko wa bei ya majani mabichi ya chai. Aidha, Bodi imeendelea kuratibu uendeshaji wa mnada wa chai unaofanyika kwa njia ya mtandao (Digital Online Tea Auction - DOTA), ambapo bei ya chai kavu imeongezeka kutoka Dola za Marekani 0.98 sawa na Shilingi 2,450 hadi kufikia Dola za Marekani 1.6 sawa na Shilingi 4,000 kwa kilo moja ya chai kavu.

161. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi imefanya tathmini na kubaini kuwa viwanda 13 vyenye jumla ya uwezo wa kuchakata chai tani 34,510 vimesitisha uchakataji wa majani mabichi ya chai kutoka kwa wakulima. Katika kuhakikisha uchakataji wa chai unaendelea, Serikali imeendelea na juhudi mbalimbali ikiwemo kuhakikisha viwanda hivyo vinaendelea na uzalishaji, kutafuta wawekezaji wapya wa viwanda vya chai na kujenga viwanda vipya. Juhudi hizo zimefanikisha kufunguliwa kwa viwanda vitano (5) kati ya 13 vilivyositisha huduma.

***Mheshimiwa Spika, nitoe rai kwa wamiliki wa viwanda vya chai nchini kuendelea kuchakata chai ya wakulima kwa kuwa Serikali inaendelea na mikakati madhubuti ya kufufua na kuendeleza zao la chai. Kwa wale ambao viwanda vyao vitakuwa bado vimesitisha uzalishaji, Serikali itapitia upya mikataba yao ya ubinafsishaji na kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa Sheria.***

**Zao la Kahawa**

162. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Kahawa Tanzania ilipanga kuongeza uzalishaji wa zao la kahawa kufikia tani 85,000; kutoa mafunzo kwa wakulima 20,000 na Maafisa Ugani 500; kuzalisha na kusambaza miche 30,000,000 ya kahawa; kuweka mfumo wa kusimamia uandaaji, usambazaji na utunzaji wa miche; kuwezesha uanzishaji wa mashamba ya kahawa yenye ukubwa wa hekta 4,000; kuchimba visima katika mashamba makubwa ya kahawa (block farm); na kujenga maabara za Tissue culture katika vituo vya TaCRI vya Maruku na Mbozi.

163. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, uzalishaji wa kahawa umefikia tani 74,663.60 sawa na asilimia 87.8 ya lengo la tani 85,000.

Uzalishaji huo umefikiwa kwa kutoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha zao la kahawa na mbinu za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa wakulima 3,360 na Maafisa Ugani 112 katika maeneo ya uzalishaji; na kuchimba visima kumi (10) katika Mkoa wa Songwe (Mbozi) kwa ajili ya umwagiliaji kwenye mashamba ya kahawa ya wakulima wadogo ili kukabiliana na athari za ukame.

164. ***Mheshimiwa Spika***, Bodi kwa kushirikiana na TARI imezalisha na kusambaza miche 27,702,090 ya kahawa kwa mpango wa ruzuku kwa wakulima katika mikoa 17 inayozalisha kahawa nchini, sawa na asilimia 92.3 ya lengo la kuzalisha miche 30,000,000. Lengo ni kuongeza maeneo mapya ya uzalishaji wa kahawa na kuondoa miche ya zamani kwenye mashamba ya muda mrefu. Vilevile, Bodi imewezesha kuanzisha wa mashamba ya kahawa yenye ukubwa wa hekta 347.4 katika mikoa ya Kigoma (hekta 118.2), Ruvuma (hekta 112), Kilimanjaro (hekta 80), Arusha (hekta 20) na Songwe (hekta 17.2). Pia, Wizara imeendelea kuimarisha bustani za kuzalisha mbegu katika vituo vya utafiti vya TARI - TaCRI kwa kuviwekea miundombinu ya umwagiliaji ili kuviwezesha kuzalisha kiasi cha mbegu kinachokidhi mahitaji ya uzalishaji wa miche.

**Zao la Korosho**

165. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Korosho Tanzania katika mwaka 2025/2026 ilipanga kuongeza uzalishaji wa korosho kufikia tani 700,000; kununua na kusambaza viuatilifu vya korosho tani 30,000 za *Sulphur* na lita 3,800,000 za viuatilifu vya maji; kutoa mafunzo kupitia mashamba darasa 30 kwa wakulima 1,000 na Maafisa Ugani 200; kuzalisha na kusambaza mbegu za korosho tani 150; kuweka mfumo wa kusimamia uandaaji, usambazaji na utunzaji wa mbegu; kuendelea na ujenzi wa viwanda vya kubangua korosho pamoja na kuongeza thamani bidhaa nyingine zitokanazo na korosho katika kongani la viwanda Maranje Wilaya ya Nanyamba; na kutengeneza mfumo wa upatikanaji wa malighafi kwa wabanguaji wadogo.

166. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha uhifadhi na ubora wa korosho, Bodi kwa kushirikiana na Vyama Vikuu vya korosho ilipanga kujenga ghala tatu (3) zenye uwezo wa kuhifadhi jumla ya tani 15,000 katika vyama vya TANECU, MAMCU na CORECU.

167. ***Mheshimiwa Spika***, ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, uzalishaji wa zao la korosho umefikia tani 617,683.77 sawa na asilimia 88.24 ya lengo la tani 700,000. Uzalishaji huo umechangiwa na

upatikanaji wa pembejeo kwa wakati zilizonunuliwa kwa fedha za ushuru wa korosho ghafi baada ya mabadiliko ya Sheria ya Tasnia ya Korosho. Wizara imenunua viuatilifu vya korosho vya *Sulphur* ya unga tani 44,177.18 na lita 2,142,874.5 na kuvisambaza kwa wakulima 549,936 kwa ajili ya kudhibiti visumbufu vya zao hilo katika maeneo ya uzalishaji. Kuongezeka kwa uzalishaji kulichangiwa na kuimarika kwa huduma bora za ugani zilizotolewa na vijana walioajiriwa kupitia mradi wa BBT.

168. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, Bodi kwa kushirikiana na TARI imetoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha zao la korosho na matumizi sahihi ya viuatilifu kupitia mashamba darasa 500 kwa wakulima 222,332 na Maafisa Ugani 2,699 katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma, Pwani, Tanga, Singida, Katavi, Kigoma, Mbeya, Njombe, Rukwa, Morogoro, Shinyanga, Tabora, Iringa, Songwe na Dodoma.

169. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha upatikanaji wa miche ya korosho, Bodi kwa kushirikiana na TARI imezalisha na kusambaza mbegu bora za korosho tani 22 zenye uwezo wa kuzalisha miche takriban 3,000,000 kwa wakulima 100,000 katika Halmashauri za Rufiji, Manispaa ya Lindi, Mtama, Nachingwea, Ruangwa, Liwale, Tunduru, Namtumbo, Manispaa ya Mtwara, Mtwara Vijijini, Chunya, Kyela,

Mbarali, Momba, Songwe, Nanyamba Mji, Tandahimba, Newala na Ludewa.

170. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhamasisha uwekezaji, upatikanaji wa masoko na uongezaji thamani wa zao la korosho, ujenzi wa kiwanda cha kubangua korosho chenye uwezo wa kubangua tani 50,000 kwa mwaka katika kongani ya viwanda iliyopo Maranje Halmashauri ya Wilaya ya Nanyamba umefikia wastani wa asilimia 55. Vilevile, ujenzi wa viwanda vitatu (3) vya kubangua korosho vyenye uwezo wa kubangua tani 230,000 kwa mwaka vinajengwa kupitia wawekezaji ambao ni Mateak Holdings (tani 100,000), Dorado Cashew Ltd (tani 100,000) na Korosho Investment (tani 30,000). Pia, Bodi imetengeneza mfumo wa upatikanaji wa malighafi kwa wabanguaji wadogo kupitia ghala zinazojengwa katika kongani ya viwanda ya Maranje ambapo wabanguaji watapata malighafi kupitia soko la awali.

171. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha uhifadhi na ubora wa korosho Chama Kikuu cha Ushirika cha TANECU kinaendelea na ujenzi wa ghala tatu (3) zenye uwezo wa kuhifadhi tani 5,000 kila moja. Ujenzi wa ghala hizo umefikia wastani wa asilimia 31. Vilevile, mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa ghala mbili (2) za Chama Kikuu cha Ushirika MAMCU zenye uwezo wa kuhifadhi tani 5,000 kila moja

katika Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara amepatikana.

**Zao la Mkonge**

172. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Mkonge Tanzania katika mwaka 2025/2026, ilipanga kuhamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa zao la mkonge kufikia tani 80,000; kutoa mafunzo ya uongezaji thamani wa mkonge; kuanzisha mashamba makubwa ya pamoja yenye ukubwa wa hekta 2,000; kuwezesha umiliki wa ardhi ya kilimo yenye ukubwa wa hekta 6,000; kuanzisha Chama Kikuu cha Ushirika cha Mkonge; kununua na kusimika mashine 10 za kuchakata mkonge (dikotiketa); kurejesha viwanda na mashamba yaliyokuwa chini ya kampuni ya Sisalana; na kuendelea na ujenzi wa kituo cha uzalishaji wa nzi chuma.

173. ***Mheshimiwa Spika***, ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, uzalishaji wa zao la mkonge umefikia tani 64,321.77 sawa na asilimia 80.4 ya lengo la tani 80,000 na uzalishaji unaendelea. Uzalishaji huo umechangiwa kwa kutoa mafunzo kuhusu uzalishaji wa mkonge na uongezaji thamani wa zao hilo kwa wadau 6,853 na Maafisa Ugani 44 katika mikoa ya Tanga, Morogoro, Pwani, Shinyanga, Simiyu, Tabora, Mara, Singida, Kilimanjaro na Arusha.

174. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, Bodi imeanzisha mashamba makubwa ya pamoja ya mkonge ya wakulima wadogo yenye ukubwa wa hekta 9,211 katika mikoa ya Morogoro (hekta 1,519 ), Pwani (hekta 343), Tanga (hekta 6,411) na Kilimanjaro (hekta 938) na imeendelea kuwezesha umiliki wa ardhi ya kilimo yenye ukubwa wa hekta 21,625.5 katika mikoa ya Tanga (hekta 16,027.50), Morogoro (hekta 3,797.50) na Arusha (hekta 1,800). Mashamba hayo yanatarajiwa kuongeza uzalishaji wa mkonge tani 120,000 ifikapo mwaka 2030.



*Shamba kubwa la pamoja la zao la mkonge lililopo Wilaya ya Handeni - Tanga*

175. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuongeza thamani na uzalishaji wa mkonge nchini, Wizara kupitia Bodi ya Mkonge Tanzania imeanzisha kiwanda kimoja (1) cha kuchakata mkonge chenye uwezo wa kuchakata tani tano (5) kwa siku katika Mkoa wa Tanga. Aidha, mzabuni kwa ajili ya kuanzisha viwanda viwili vya kuchakata mkonge katika Wilaya za Handeni na Mkinga, Mkoa wa Tanga amepatikana. Pia, Bodi imewezesha usajili wa Chama Kikuu cha Mkonge Mkoa wa Tanga (Tanga Sisal Cooperative Union Ltd) kitakacho hudumia vyama vyote vya msingi vinavyojishughulisha na zao la mkonge.

176. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea na ujenzi wa kituo cha uzalishaji wa nzi chuma (Blacksoldier flies) kwa kutumia mabaki ya mkonge (Sisal waste) ili kutengeneza protini kwa matumizi ya mifugo. Aidha, taratibu za urejeshaji wa viwanda na mashamba yaliyokuwa chini ya Kampuni ya Sisalana kwa ajili ya kuongeza uzalishaji na kuwezesha uchakataji wa mkonge zinaendelea.

**Zao la Tumbaku**

177. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Tumbaku Tanzania ilipanga kuongeza uzalishaji wa zao la tumbaku kufikia tani 250,000 mwaka 2025/2026; kutoa mafunzo kwa wakulima 5,000 na Maafisa Ugani 200

katika maeneo ya uzalishaji; kuratibu ununuzi na usambazaji wa viuatilifu lita 183,571, pakiti 1,468,568 na chupa 2,202,852; kujenga mabani 2,500 ya kukaushia tumbaku na kuanza kutumia teknolojia ya jua na umeme; kununua mitambo minne (4) ya kuchimba mabwawa na visima katika mashamba ya wakulima; kukamilisha ujenzi wa ofisi; kuratibu ujenzi wa kiwanda cha kuchakata tumbaku; na kuanzisha bandari kavu kwa ajili ya kufungasha tumbaku.

178. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, uzalishaji wa zao la tumbaku umefikia tani 185,776 sawa na asilimia 74 ya lengo la tani 250,000. Uzalishaji huo umechangiwa kwa kutoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha zao la tumbaku kwa wakulima 5,200 na Maafisa Ugani 182 katika maeneo ya uzalishaji; kununua na kusambaza kwa wakulima viuatilifu aina ya *Flumetralin* lita 130,071 *Imidacloprid* (30g/pkt) pakiti 922,213 na *Deltamethrin* (20ml/chupa) chupa 798,135 kwa ajili ya kudhibiti visumbufu vya zao la tumbaku.

179. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Bodi imejenga mabani mapya 57,282 na kukarabati mabani 2,629 kwa ajili ya kukaushia tumbaku katika mikoa ya Tabora, Shinyanga, Katavi, Ruvuma, Songwe, Mbeya, Geita, Kigoma, Singida na

Iringa; na kwa kushirikiana na TARI na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandela imefanya majaribio ya kukausha tumbaku kwa mitambo inayotumia nishati ya jua katika Halmashauri ya Manispaa ya Tabora na kubaini kuwa viwango vya ubora vya tumbaku iliyokaushwa kwa jua havitofautiani na tumbaku iliyokaushwa kwa kutumia kuni.

***Mheshimiwa Spika, ninaomba nitoe rai kwa wakulima katika maeneo ya uzalishaji wa tumbaku kutumia nishati safi ya jua kwa ajili ya kukaushia tumbaku ili kulinda mazingira.***

180. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi kwa kushirikiana na wadau wa zao la Tumbaku imewezesha ununuzi wa mitambo miwili ya kuchimba visima kwa ajili ya wakulima wa tumbaku. Pia, imechimba visima 17 katika Wilaya ya Chunya na imejenga mabwawa matano (5) katika Wilaya ya Kaliua na Urambo kwa ajili ya kuwawezesha wakulima kupata maji ya kuhudumia vitalu vya tumbaku.

181. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi inaendelea kuboresha mazingira ya kazi ambapo ujenzi wa ofisi za Kanda katika Halmashauri ya Mpanda umekamilika na katika Halmashauri ya Kaliua umefikia wastani wa asilimia 95. Vilevile, katika kuimarisha uongezaji thamani wa zao la tumbaku, ujenzi

wa jengo la kiwanda kinachomilikiwa na Kampuni ya Mkwawa Leaf chenye uwezo wa kuchakata tani 28 kwa siku katika Mkoa wa Tabora umefikia asilimia 75. Aidha, ununuzi wa mashine kwa ajili ya kiwanda hicho unaendelea.

**Zao la Pareto**

182. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia COPRA ilipanga kuongeza uzalishaji wa zao la pareto kufikia tani 5,000 mwaka 2025/2026; kutoa mafunzo kwa wakulima viongozi 19,000 na wakaguzi wa pareto 50; kupitia TARI kuzalisha mbegu bora za pareto tani mbili (2); kujenga makaushio 150; na kuanzisha kilimo cha mkataba katika zao la pareto na kuzuia usafirishaji wa unga wa pareto kwenda nje ya nchi.

183. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, uzalishaji wa zao la pareto umefikia tani 2,780 sawa na asilimia 55.6 ya lengo la tani 5,000 na uzalishaji unaendelea. Uzalishaji huo umechangiwa kwa kutoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha zao la pareto kwa wakulima viongozi 74 kupitia mashamba darasa 74 yaliyoanzishwa katika Halmashauri za Mbulu, Arusha Vijijini, Makete, Ileje, Mbeya Vijijini na Ludewa; na kwa kushirikiana na wadau imezalisha na kusambaza mbegu za

pareto tani tisa (9) kwa wakulima katika mikoa ya Mbeya, Songwe, Njombe, Iringa na Arusha.

184. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha uongezaji thamani wa pareto inayozalishwa nchini, ujenzi wa makaushio 150 ya maua ya pareto katika Halmashauri za Mbulu (25), Arusha Vijijini (10), Makete (30), Ileje (35), Mbeya Vijijini (40) na Ludewa (10) umefikia wastani wa asilimia 20 na kilimo cha mkataba katika zao la pareto kimeanzishwa ili kuzuia usafirishaji wa unga wa pareto kwenda nje ya nchi kwa lengo la kuongeza thamani na kulinda viwanda vya ndani.

**Zao la Kakao**

185. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia COPRA katika mwaka 2025/2026, ilipanga kuhamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa kakao kufikia tani 15,000; kutoa mafunzo kwa wakulima viongozi 500 na Maafisa Ugani 45; kujenga miundombinu ya usindikaji na ukaushaji katika vituo saba (7) vya ukusanyaji wa kakao; kuhamasisha uongezaji thamani wa zao la kakao; kusajili wakulima 91,000 wa kakao; kuzalisha miche 1,000,000 na kuisambaza kwa wakulima; na kuwezesha kituo cha TARI Ifakara ili kukifanya kuwa kituo mahiri cha utafiti wa zao la kakao.

186. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, uzalishaji wa zao la kakao umefikia tani 10,069 sawa na asilimia 67.31 ya lengo la tani 15,000 na uzalishaji unaendelea. Uzalishaji huo umechangiwa kwa kutoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora kwa wakulima viongozi 456 na Maafisa Ugani 42 katika maeneo ya uzalishaji. Vilevile, ujenzi wa miundombinu ya kusindika na kukausha katika vituo saba (7) vya kukusanyia kakao vilivyopo Kyela (4), Mlimba (1), Mvomero (1) na Muheza (1) umefikia wastani wa asilimia 20. Kukamilika kwa miundombinu hiyo kutasaidia kuimarisha ubora wa uongezaji thamani wa zao la kakao.

187. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha matakwa ya soko la kimataifa la Ulaya, hususan kanuni za kuzuia ukataji wa miti za Umoja wa Ulaya (EUDR) kwa zao la kakao yanazingatiwa, wakulima 29,830 wa kakao na mashamba yao ya uzalishaji yenye jumla ya ekari 88,686 wamesajiliwa katika mikoa ya Tanga, Mbeya na Morogoro. Aidha, katika kuongeza mashamba ya uzalishaji wa kakao na kufidia miche iliyozeeka katika mashamba ya muda mrefu, TARI imezalisha na kusambaza miche 240,044 ya kakao kwa wakulima katika maeneo ya uzalishaji. Aidha, kituo cha TARI Ifakara kimekuwa kituo mahiri cha utafiti wa zao la kakao ambapo vinasaba 293 vya kakao

vimekusanywa na kuhifadhiwa katika kituo hicho.

**Mazao ya Bustani**

188. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia COPRA kwa kushirikiana na wadau katika mwaka 2025/2026 ilipanga kuongeza uzalishaji wa mazao ya bustani kufikia tani 9,000,000; na kutoa mafunzo kwa Maafisa Ugani 1,500 na wakulima 5,000 katika maeneo ya uzalishaji. Ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, uzalishaji wa mazao ya bustani umefikia tani 9,781,236.74 mwaka 2024/2025 sawa na asilimia 108.68 ya lengo la kuzalisha tani 9,000,000; na mafunzo rejea kuhusu kilimo bora cha mazao ya bustani yametolewa kwa Maafisa Ugani 542 na wakulima 1,626 katika maeneo ya uzalishaji.

**Mazao ya Bustani yenye Kipaumbele**

**Zao la Parachichi**

189. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2025/2026 ilipanga kuhamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa parachichi zinazouzwa nje ya nchi kufikia tani 40,000; kutoa mafunzo kwa wakulima 9,500 na Maafisa Ugani 200; kununua na kusambaza viuatilifu lita 3,000 za viuakuvu na lita 1,000 aina ya *Copper sulphate*; kuhamasisha

wakulima kujiunga na Vyama vya Ushirika wa parachichi; kuandaa na kusambaza kwa wakulima mwongozo wa viwango vya uzalishaji wa parachichi na mazao ya viungo; na kutunga kanuni za kusimamia mnyororo wa thamani wa zao la parachichi.

190. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilipanga pia, kuviwezesha viwanda vya uchakataji na utengenezaji wa bidhaa zitokanazo na parachichi; kusimamia mauzo ya parachichi; kujenga vituo 100 vya kukusanyia parachichi; kujenga vituo vitatu (3) vya kupanga madaraja na kufungasha parachichi; kuzalisha na kusambaza miche ya parachichi 2,100,000; na kuweka mfumo wa kusimamia uandaaji, usambazaji na utunzaji wa miche; na kuendelea kuwawezesha wakulima wadogo kupata miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya parachichi.

191. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, uzalishaji wa zao la parachichi ulifikia tani 201,354 katika mwaka 2024/2025. Kati ya hizo, parachichi zinazouzwa nje ya nchi ni tani 37,871 sawa na asilimia 94.7 ya lengo la kuzalisha tani 40,000 ya parachichi zinazouzwa nje ya nchi. Uzalishaji huo umechangiwa kwa kutoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha zao la parachichi kwa wakulima 527 na Maafisa Ugani 50; kuandaa na kusambaza Mwongozo kuhusu Viwango vya Uzalishaji Endelevu wa zao la Parachichi  na Mazao ya

Viungo kwa wakulima 213; kutunga Kanuni za kusimamia mnyororo wa thamani wa zao la parachichi kwa kutambua wavunaji, kusajili wanunuzi, mawakala, kusimamia bei elekezi na kuweka madaraja ya matunda ya parachichi.

192. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TPHPA imetangaza zabuni kwa ajili ya ununuzi wa viuatilifu lita 3,000 za viuakuvu na lita 1,000 za *Copper sulphate* kwa ajili ya kudhibiti visumbufu katika zao la parachichi. Aidha, Tume ya Maendeleo ya Ushirika imehamasisha wakulima 54 wa parachichi wa Halmashauri ya Makete kuanzisha Chama cha Ushirika cha MANG'OTO AMCOS na wakulima 95 wa Wilaya ya Wanging'ombe kuanzisha chama cha Ulembwe AMCOS. Vyama hivyo vitasaidia kuongeza ushindani katika soko la parachichi na kuwezesha wakulima kuuza nje ya nchi.



*Ufungashaji wa Parachichi kwa ajili ya kusafirisha nje ya nchi katika kiwanda cha Seasons Orchard - Njombe*

193. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha uongezaji thamani wa zao la parachichi, ujenzi wa vituo nane (8) vya kukusanyia parachichi katika Mkoa wa Mbeya Halmashauri za Rungwe (6) na Busokelo (2) umefikia wastani wa asilimia 20. Vilevile, imesaini mikataba na mafundi na wasambazaji wa vifaa vya ujenzi kwa ajili ya ujenzi wa vituo 12 vya ukusanyaji wa parachichi katika mikoa ya Iringa vinne (4), Rukwa kimoja (1), Ruvuma viwili (2) na Njombe vitano (5). Aidha, katika kuongeza maeneo ya uzalishaji wa parachichi, Wizara imesambaza miche ya parachichi 349,000 katika mikoa ya Mbeya, Songwe, Iringa na Njombe kwa mpango wa ruzuku na usambazaji unaendelea. Vilevile, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imechimba visima vitatu (3) kwa ajili ya kuwawezesha wakulima wadogo kupata maji ya umwagiliaji katika maeneo yanayolima parachichi.

**Zao la Viazi mviringo**

194. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara katika mwaka 2025/2026, ilipanga kuongeza uzalishaji wa zao la viazi mviringo kufikia tani 2,570,061; kukarabati vitalu nyumba vinne (4); kujenga vitalu nyumba vitatu (3) katika vituo vya utafiti; kutoa mafunzo kwa wakulima wawezeshaji 500; na kuandaa na kusambaza mwongozo wa uzalishaji na uuzaji wa viazi mviringo.

195. ***Mheshimiwa Spika***, ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa uzalishaji wa viazi mviringo umefikia tani 2,961,414.82 sawa na asilimia 115 ya lengo la tani 2,570,061. Aidha, Wizara imefanya tathmini ya gharama kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa vitalu nyumba katika vituo vya utafiti vya Igeri (Njombe), Tengeru (Arusha), Uyole (Mbeya) na Nkundi (Rukwa) kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa mbegu bora za viazi mviringo. Vilevile, mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora na himilivu cha zao la viazi mviringo na uzalishaji wa mbegu bora za viazi kwa wakulima wawezeshaji 350 yametolewa katika mikoa ya Mbeya, Njombe, Morogoro, Tanga, Arusha, Kilimanjaro na Manyara. Pia, rasimu ya Mkakati wa Kuendeleza zao la Viazi mviringo nchini imeandaliwa.

## Mazao yenye Mahitaji Makubwa

196. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu uzalishaji wa mazao yenye mahitaji makubwa ambayo ni ngano, miwa na mazao ya mafuta yanayoagizwa kutoka nje ya nchi.

### Zao la Ngano

197. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2025/2026, ilipanga kuongeza uzalishaji wa zao la ngano kufikia tani 300,000; kusambaza mbegu za ngano tani 1,000 kwa wakulima;

kuanzisha vituo maalum vya kuzalisha mbegu za ngano; kuendelea na majaribio ya aina 82 za mbegu mpya za ngano; na kutoa mafunzo ya uzalishaji wa mbegu za kuazimia ubora (QDS) kwa wakulima 500.

198. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TARI ilipanga kufanya utafiti wa mbegu za ngano zenye kukidhi sifa ya mahitaji ya soko; kuhamasisha Vyama vya Ushirika kuanzisha mashamba makubwa ya ngano na viwanda vidogo vya kuchakata ngano; na kuwezesha upatikanaji wa mitaji kwa wakulima watakaoendesha mashamba hayo kupitia dirisha za *equity* na *guarantee scheme* litakaloanzishwa katika Benki ya Ushirika Tanzania.

199. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa uzalishaji wa zao la ngano ulifikia tani 115,826 mwaka 2024/2025. Aidha, tani 500 za mbegu bora za ngano zimesambazwa kwa wakulima katika maeneo ya uzalishaji kupitia mpango wa ruzuku; na mbegu za ngano aina tatu (3) zimewasilishwa TOSCI kwa ajili ya majaribio ya utambuzi na umahiri.

200. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia TARI imeendelea kufanya majaribio ya aina 82 ya mbegu mpya za ngano na imeendelea kufanya tathmini ya mashamba kwa ajili ya kuzalisha mbegu za ngano. Pia, Wizara kupitia

TOSCI imetoa mafunzo ya uzalishaji wa mbegu za kuazimia ubora (QDS) kwa wakulima 415 ili kuwezesha uzalishaji wa mbegu za ngano nchini.

201. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika imehamasisha Vyama vya Ushirika 14 kuanzisha mashamba makubwa ya ngano na viwanda vidogo vya kuchakata ngano katika mikoa ya Manyara, Kilimanjaro na Njombe. Aidha, Benki ya Ushirika Tanzania imeanzisha dirisha za *equity* na *guarantee scheme* kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa mitaji yenye riba nafuu kwa wakulima.

**Zao la Miwa na Uzalishaji wa Sukari**

202. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Sukari Tanzania katika mwaka 2025/ 2026, ilipanga kuongeza uzalishaji wa zao la miwa kutoka tani 4,713,907.89 zilizozalisha sukari tani 431,736.74 mwaka 2024/2025 hadi tani 7,000,000 za miwa zitakazozalisha sukari tani 700,000; kusimamia upanuzi wa kiwanda cha sukari cha Mtibwa na mashamba ya miwa ya kiwanda yaliyopo Dakawa yenye ukubwa wa hekta 12,000; kusimamia upanuzi wa mashamba yenye ukubwa wa hekta 13,000 ya kiwanda cha sukari Kagera na kusimamia utekelezaji wa mradi wa upanuzi wa kiwanda cha sukari cha Kilombero K4.

203. ***Mheshimiwa Spika*** vilevile, ilipanga kusimamia uanzishaji wa vitalu vya kuzalisha miche ya miwa kwenye eneo lenye ukubwa wa hekta 100 katika bonde la Kilombero; kuratibu uanzishaji wa viwanda vya sukari vya Rai Group na Lake Agro; TARI kuanzisha kitalu cha miche ya miwa kwenye eneo la ukubwa wa ekari 10; na kuzalisha mbegu za miwa tani 10.

204. ***Mheshimiwa Spika***, ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, uzalishaji wa zao la miwa umefikia tani 4,351,673.1 zilizozalisha sukari tani 410,979.04 sawa na asilimia 62 na 59 ya lengo la kuzalisha miwa tani 7,000,000 na sukari tani 700,000, mtawalia. Uzalishaji huo umetokana na upanuzi wa kiwanda cha sukari cha Mtibwa na mashamba ya miwa ya kiwanda yaliyopo Dakawa yenye ukubwa wa hekta 12,000 ambapo upanuzi umefikia wastani wa asilimia 54. Aidha, upanuzi wa mashamba yenye ukubwa wa hekta 13,000 ya kiwanda cha sukari Kagera umefikia wastani wa asilimia 96; na upanuzi wa kiwanda cha sukari cha Kilombero K4 umekamilika. Upanuzi huo utaongeza uzalishaji wa miwa kutoka tani 600,000 hadi tani 1,500,000 kwa mwaka.

205. ***Mheshimiwa Spika***, kitalu cha miche ya miwa kwa ajili ya wakulima wadogo kimeanzishwa kwenye eneo lenye ukubwa wa hekta 100 katika bonde la Kilombero. Aidha, Wizara kupitia Bodi imeratibu uanzishaji wa

viwanda vya sukari vya Lake Agro Ltd - Pwani, Rai group - Kigoma na Golden Sugar Mill – Kagera. Aidha, vitalu A na B venye ukubwa wa hekta 20 na hekta 170, mtawalia vinaendelea na uzalishaji.

206. ***Mheshimiwa Spika***, pia, Wizara kupitia Bodi imeratibu uwekezaji wa uzalishaji wa bidhaa zitokanazo na sukari kwa kusajili ujenzi wa distillery ya Mara Nile – Pwani, upanuzi wa Illovo distillery katika kiwanda cha Kilombero na kiwanda cha TPC Ltd – Moshi ili kuongeza uzalishaji wa bidhaa zitokanazo na sukari; na imezalisha mbegu za miwa tani 210 katika Mikoa ya Pwani, Kagera na Morogoro.



*Kiwanda cha sukari cha Kilombero K4 - Morogoro*

**Mazao ya Mafuta**

207. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilipanga kuongeza uzalishaji wa mazao ya mafuta kufikia tani 2,200,000 mwaka 2025/2026; kuwezesha uchakataji wa mafuta yanayotokana na alizeti na chikichi kwa kuviwezesha viwanda vidogo; kuwawezesha wakulima wakubwa wa alizeti kwa kuwapatia mashamba makubwa ya pamoja; kuendelea kushauriana na Wizara ya Fedha kuweka sera za fedha ikiwemo kuongeza ushuru kwenye mafuta ya kula yanayotoka nje ya nchi; kusambaza mbegu bora za alizeti tani 2,150 kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku; kuzalisha na kusambaza miche ya chikichi 10,000,000 kwa wakulima; na kuzalisha na kusambaza mbegu bora za karanga tani 20.1 na mbegu za ufuta tani 40.

208. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa uzalishaji wa mazao ya mafuta ulifikia tani 2,248,046.24 mwaka 2024/2025 na kuchangia uzalishaji wa mafuta ya kula nchini kufikia tani 305,906. Uzalishaji huo ni pungufu kwa asilimia 58 ya mahitaji ya mafuta ya kula ya tani 731,974 kwa mwaka. Aidha, mbegu bora za alizeti tani 741 zimesambazwa kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku; miche ya chikichi 4,491 imezalishwa na kusambazwa kwa wakulima katika maeneo ya uzalishaji; na mbegu bora za karanga tani

24.3 na mbegu za ufuta tani 24.56 zimezalishwa na kusambazwa kwa wakulima katika maeneo ya uzalishaji. Kadhalika, Wizara imekamilisha Kanuni za Usimamizi wa Mafuta ya Kula ambazo zinalenga kuchagiza uzalishaji wa ndani na nchi kujitosheleza kwa mafuta ya kula ifikapo mwaka 2030.

## 4.2 Kuongeza Ajira zenye Staha na Ushiriki wa Vijana na Wanawake kwenye Kilimo

### 4.2.1 Kuwezesha Upatikanaji wa Ardhi ya Kilimo na Uanzishaji wa Mashamba Makubwa ya Pamoja (BBT – Mashamba)

209. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Wizara ilipanga kutambua, kupima na kutwaa mashamba yenye ukubwa wa hekta 80,000; kuanza uwekezaji katika shamba la Mapogoro – Chunya (Mbeya) katika eneo la ekari 20,000; kujenga ghala nane (8) zenye uwezo wa kuhifadhi tani 1,000; kujenga chumba cha ubaridi chenye uwezo wa kuhifadhi tani 1,000; kujenga uzio wa umeme kuzunguka shamba la Mlazo/Ndogowe; na kununua mitambo ya kuandaa mashamba.

210. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, Wizara imetambua maeneo yenye ukubwa wa hekta 7,019 katika mikoa ya Pwani (Kisarawe, Rufiji, Mkuranga na Kibaha) na Tanga (Mkinga)

kwa ajili ya kuanzisha mashamba makubwa ya pamoja. Vilevile, katika kuimarisha miundombinu katika mashamba makubwa ya pamoja, ujenzi wa barabara zenye urefu wa km 20 katika shamba la Mapogoro – Chunya (Mbeya) umefanyika kupitia TARURA na zabuni kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji na nyumba za shambani imetangazwa. Aidha, zabuni kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa ujenzi wa uzio wa umeme wenye urefu wa km 27 kuzunguka shamba la Mlazo/Ndogowe imetangazwa. Pia, Wizara imenunua trekta nane (8), *trailer* sita (6), mitambo miwili (2) ya kuchimba visima, *Bulldozer* tatu (3), *Excavator* mbili (2), *Wheelloader* tatu (3), *Motorgrader* tatu (3) na *Planter* sita (6) kwa ajili ya shughuli za mashamba ya Chinangali, Ndogowe na Mapogolo.

211. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha ubora na uhifadhi wa mazao yanayolimwa na vijana na wanawake wa BBT, zabuni kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa ujenzi wa ghala zenye uwezo wa kuhifadhi tani 1,000 katika mashamba ya pamoja ya vijana ya Chinangali (ghala 4) na Mlazo/Ndogowe (ghala 4) imetangazwa. Vilevile, zabuni kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa ujenzi wa chumba cha ubaridi (cold room) chenye uwezo wa kuhifadhi tani 1,000 za mazao ya kilimo katika shamba la Chinangali imetangazwa.

### 4.2.2 Kuwezesha Uendelezaji wa Programu ya BBT Ngazi ya Halmashauri

212. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Wizara ilipanga kuendelea kutekeleza mradi wa BBT katika Halmashauri 20 zitakazotenga maeneo yasiyopungua ukubwa wa hekta 200 kwa kila Halmashauri; kutoa mafunzo ya kilimo biashara kwa vijana na wanawake; na kuanzisha mashamba ya tumbaku yenye ukubwa wa ekari 150 katika Halmashauri za Uyui na Chunya.

213. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, katika kutekeleza Programu ya BBT ngazi ya Halmashauri hadi Machi 2026, Halmashauri 18 zimetenga maeneo ya kilimo kwa ajili ya vijana kuanzisha mashamba ya pamoja. Halmashauri hizo ni Chemba, Ikungi, Bahi, Kaliua, Manyoni, Madaba, Kibaha, Kilolo, Mpanda, Muleba, Kisarawe, Njombe Musoma, Kakonko, Chunya, Njombe Mji, Geita Mji na Missenyi. Kadhalika, Bodi ya Tumbaku imeanzisha mashamba ya tumbaku katika Halmashauri za Uyui na Chunya kwa ajili ya kutoa mafunzo ya zao la tumbaku kwa vijana na wanawake.

214. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha vijana na wanawake wanapata elimu ya kilimo biashara, Halmashauri za Muleba na Kaliua zimedahili vijana na wanawake 582 kwa ajili ya

kupata mafunzo ya kilimo biashara yanayoendana na shughuli za kilimo zinazofanyika katika Halmshauri hizo.

### 4.2.3 Kuwezesha Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji kwa Wakulima wadogo (BBT visima)

215. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ilipanga kuchimba visima 500 vya umwagiliaji vitakavyomwagilia eneo lenye ukubwa wa hekta 30,393.39 katika Halmashauri 178 nchini ambavyo vitanufaisha wakulima 58,903.

216. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kuwezesha kilimo cha umwagiliaji kwa wakulima wadogo, ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, visima 345 vya umwagiliaji vyenye uwezo wa kumwagilia hekta 6,052 vimechimbwa katika mikoa 15 na kunufaisha takriban wakulima 12,545. Pia, Tume imenunua *surface pump* za umwagiliaji 1,000 na zitasambazwa kwa vikundi 740 vya wakulima wanawake na vijana kutoka kwenye maeneo ya pembezoni mwa Ziwa Victoria na Tanganyika. Orodha ya visima vilivyochimbwa umeainishwa katika **Kiambatisho Na. 6**. Aidha, uchimbaji wa visima unaendelea katika mikoa mingine.

217. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imenunua seti 1,250 za pampu, jenereta na mipira ambapo seti 250 zimesambazwa kwa wakulima na seti 1,000 zitaendelea kusambazwa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji kwa wakulima katika mikoa yenye vyanzo vya uhakika wa maji. Jumla ya wakulima 2,694 katika mikoa saba (7) ya Mara (468), Mwanza (398), Kagera (634), Ruvuma (483), Simiyu (74), Geita (292) na Tanga (345) wamenufaika. Matumizi ya vifaa hivyo yataongeza eneo linalomwagiliwa kwa hekta 19,200 au ekari 48,000.

### 4.2.4 Kuwezesha Upatikanaji wa Mikopo kwa Vijana na Wanawake (BBT mitaji)

218. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilipanga kuiwezesha AGITF kiasi cha Shilingi Bilioni 6 kwa ajili ya kuwapatia mikopo vijana na wanawake; na kutenga Dola za Marekani Milioni 35 kwa kipindi cha miaka mitano (5) kupitia dirisha za *guarantee scheme*, *direct lending* na *equity fund* kwa ajili ya uongezaji thamani wa mazao ya kimkakati.

219. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, dirisha maalumu kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa mitaji kupitia *guarantee scheme, direct lending* na *equity fund* limeanzishwa na kutoa mikopo yenye thamani ya Shilingi Bilioni 5.5 kwa riba nafuu isiyozidi asilimia saba (7%).

Mikopo hiyo, imenufaisha wakulima katika mnyororo wa thamani wa kilimo. Vilevile, AGITF imeweka kiasi cha Shilingi Bilioni 3.5 kwenye dirisha la *guarantee scheme* litakalowezesha kutoa mikopo yenye thamani ya Shilingi Bilioni 7. Aidha, Kiasi cha Dola za Marekani milioni 35 zimetolewa kama *Guarantee Scheme* na Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa taasisi za fedha zitakazokopesha vijana na wanawake mikopo yenye thamani ya zaidi ya Dola za Marekani Milioni 70.

### 4.2.5 Kuwezesha Vijana na Wanawake Kuongeza Thamani ya Mazao

220. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilipanga kutekeleza mradi wa BBT kwa vijana na wanawake 200 kwa kuwapatia mafunzo ya kuongeza thamani ya zao la mkonge ili waweze kuzalisha bidhaa zitokanazo na zao hilo.

221. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, mafunzo atamizi kuhusu uongezaji thamani wa zao la mkonge yametolewa kwa vijana na wanawake 352 (wanawake 305 na wanaume 47) kupitia programu ya BBT Zanzibar na Mkoa wa Tanga. Pia, vijana na wanawake hao wamewezeshwa mashine 20 na tani tisa (9) za mkonge kwa ajili ya kutengeneza bidhaa. Vilevile, Bodi ya Korosho Tanzania imenunua mashine 100 za kubangua korosho na

kuwapatia vijana na wanawake 2,800 ili kuongeza thamani ya zao la korosho.

### 4.2.6 Kuwezesha Vijana na Wanawake kutoa Huduma za Ugani (BBT Ugani)

222. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilipanga kuendelea kutekeleza Mpango wa Ugani (BBT – Agricultural Extension Enterpreneurship Scheme) kwa ajili ya kuwatengenezea ajira vijana na wanawake 500, kuimarisha utoaji wa huduma za ugani na kukuza ujuzi wa vijana wahitimu wa vyuo vya kilimo kwa kutoa huduma za ugani kwa wakulima; na kutekeleza Programu ya BBT – Miche kwa kuwawezesha vijana na wanawake kuzalisha miche ya mazao.

223. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, vijana na wanawake 1,434 wameajiriwa kwa ajili ya kutoa huduma za ugani. Kati ya hao, Bodi ya Pamba Tanzania imeajiri vijana 761; Bodi ya Korosho Tanzania imeajiri vijana 511; Bodi ya Kahawa Tanzania imeajiri vijana 112 na COPRA imeajiri vijana 50 kwa ajili ya zao la parachichi. Hatua hiyo, imesaidia kuimarisha utoaji wa huduma za ugani na kukuza ujuzi kwa vijana wahitimu wa vyuo vya kilimo kwa ajili ya kutoa huduma za ugani kwa wakulima.

***Kilimo sasa ni fursa ya ajira kwa vijana na wanawake inayolenga kuchochea ubunifu, kuleta utajiri na kulisha Taifa kwa ujumla. Hii inasadifu shairi maarufu tulilokuwa tukilisoma shuleni la baba aliyekuwa akitoa wosia kwa watoto wake katika dakika za mwisho za uhai wake "kama mnataka mali mtaipata shambani"***

## 4.3 Kuimarisha Usalama wa Chakula na Lishe

### 4.3.1 Uwekezaji kwenye Miundombinu ya Uhifadhi ili kufikia Uwezo wa Kuhifadhi tani 3,000,000 ifikapo Mwaka 2030

224. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha uhifadhi wa mazao nchini, Wizara kupitia NFRA ilipanga kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya uhifadhi yenye uwezo wa kuhifadhi tani 165,000 kupitia mradi wa kuongeza uhifadhi wa nafaka; kuanza ujenzi wa miumbombinu yenye uwezo wa kuhifadhi tani 300,000; kukarabati ghala 46; kununua vifaa kwa ajili ya ghala 28; na kuanza ujenzi wa miundombinu ya uhifadhi wa mazao ya kilimo yenye uwezo wa kuhifadhi tani 30,000.

225. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi Machi 2026, mkandarasi amepatikana kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa Mradi wa Kuongeza Uwezo wa Hifadhi unaojumuisha vihenge na ghala zenye uwezo wa kuhifadhi tani 165,000 katika Kanda za Songea,

Makambako, Songwe, Shinyanga na Dodoma. Vilevile, wakandarasi wamekabidhiwa maeneo kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu yenye uwezo wa kuhifadhi tani 85,000 katika Kanda za Arusha, Sumbawanga, Dodoma, Shinyanga na Kipawa. Kukamilika kwa miradi hiyo kutaongeza uwezo wa Wakala wa kuhifadhi chakula kutoka tani 776,000 hadi tani 861,000. Aidha, zabuni kwa ajili ya kupata wakandarasi wa ukarabati wa ghala 20 imetangazwa. Pia, zabuni kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ghala 28 zilizojengwa katika Mkoa wa Ruvuma imetangazwa.

### 4.3.2 Kuiongezea NFRA Uwezo wa Kununua Mazao ya Wakulima ili Kuongeza Hifadhi

226. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha usalama wa chakula nchini, Wizara kupitia NFRA katika mwaka 2025/202,6 ilipanga kununua tani 1,140,000 za nafaka; na kuuza chakula ndani na nje ya nchi pindi kitakapohitajika.

227. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, NFRA imenunua tani 135,290.394 za nafaka kwa lengo la kuimarisha usalama wa chakula nchini na kufanya hifadhi ya akiba ya chakula ya Taifa kufikia tani 553,077.376; na imeuza tani 95,872.887 za nafaka (mpunga tani 33,865.024, mahindi tani 55,867.957, mbaazi tani 5,652.479 na dengu tani 487.428).



*Mh.Daniel Chongolo, Waziri wa Kilimo (kulia) akikagua ghala la kuhifadhia chakula linalopatikana Kipawa- Dar es Salaam, ghala hilo ni mali ya Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa Bw. Andrew Komba*

### 4.3.3 Kuhamasisha Matumizi ya Mazao yaliyoongezewa Virutubishi ili Kukabiliana na Matatizo ya Lishe Nchini

228. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Wizara ilipanga kuendelea kutekeleza Mpango Kazi wa Lishe katika Kilimo (Nutrition Sensitive Agriculture Action Plan – NSAAP) ili

kukabiliana na matatizo ya lishe yanayohusisha udumavu, ukondefu na upungufu wa wekundu wa damu; kuzalisha na kusambaza vipando vya viazi lishe 3,290,000; na kutoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora kwa wakulima wawezeshaji 2,500 na wazalishaji wa mbegu za viazi lishe 100.

229. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, Wizara kupitia TARI imezalisha vipando vya viazi lishe 25,401 na kuvisambaza katika mikoa ya Tabora, Kigoma, Singida, Katavi na Mwanza na uzalishaji unaendelea. Vilevile, TARI imetoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora kwa wakulima wawezeshaji 206 na wazalishaji wa mbegu bora za viazi lishe 1,054 katika Wilaya za Kakonko, Kasulu, Kibondo, Buhigwe, Uvinza, Tanganyika, Mpanda, Nsimbo, Mlele, Nkasi, Sikonge, Manispaa ya Tabora, Kaliua, Uyui, Urambo, Nzega, Itigi, Manyoni, Manispaa ya Singida na Ikungi.

230. ***Mheshimiwa Spika,*** TARI imefanya utambuzi wa virutubisho kwa sampuli 69 za mazao ya mpunga, ngano, mahindi, maharage, kunde, mbaazi, soya, karanga, ufuta na alizeti ili kubaini muundo unaopatikana wa virutubisho kwa ajili ya kuongeza uelewa wa masuala ya lishe kwa watumiaji. Vilevile, imebuni *prototype* ambayo inatumika kukoboa nafaka ikiwemo mahindi, mtama, ngano, uwele na ulezi

ambayo itawezesha wakulima kuchakata nafaka bila kuathiri virutubishi vilivyomo kwenye nafaka hizo.

## 4.4 Kuimarisha Upatikanaji wa Masoko, Mitaji na Mauzo ya Mazao Nje ya Nchi

### 4.4.1 Kujenga Miundombinu ya Masoko ya Mazao ya Kilimo kwa ajili ya Wakulima katika Halmashauri mbalimbali Nchini

**Masoko ya Kimkakati**

231. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea kuimarisha miundombinu ya masoko ya mazao ya kilimo, Wizara ilipanga kuendelea na ujenzi wa masoko matano (5) ya kimkakati. Ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, ujenzi wa masoko matano (5) ya kimkakati katika Halmashauri za Manispaa ya Kahama (Busoka), Ngara (Kabanga), Kyerwa (Nkwenda na Murongo) na Tarime (Sirari) umefikia wastani wa asilimia 81.

232. ***Mheshimiwa Spika,*** hatua ya ujenzi iliyofikiwa kwa kila soko ni kama ifuatavyo: - Soko la Nkwenda (asilimia 87), Kabanga (asilimia 85), Sirari (asilimia 83), Busoka (asilimia 75) na Murongo (asilimia 70). Kukamilika kwa ujenzi wa masoko hayo kutawezesha wakulima na wadau wengine kufanya biashara ya mazao ya kilimo katika mipaka ya nchi za Uganda, Kenya, Rwanda na Burundi.

**Vituo vya Masoko (Market Sheds)**

233. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Wizara ilipanga kuendelea na ujenzi wa vituo saba (7) vya masoko; kuanza ujenzi wa vituo vitatu (3) vya masoko (market sheds); na kuanzisha masoko manne (4) ya mazao ya kilimo kwenye mipaka ya Rusumo, Namanga, Kasumulo na Holili.

234. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, ujenzi wa vituo sita (6) vya masoko (market sheds) umefikia wastani wa asilimia 43.67. Vituo hivyo vya masoko ni Kibakwe (Mpwapwa) asilimia 98, Ushirika (Nzega Mji) asilimia 63, Endashangwet (Karatu) asilimia 42, Losirwa (Monduli) asilimia 37, Rombo (Mamsera) asilimia 20 na Hai (Masama Mula) asilimia 2. Kukamilika kwa ujenzi wa vituo hivyo, kutawezesha wakulima kukusanya na kuuza mazao yao sehemu rasmi zinazotambulika na mamlaka husika. Aidha, Wizara inaendelea na taratibu za kubainisha maeneo kwa ajili ya kuanzisha masoko manne (4) ya mazao ya kilimo kwenye mipaka ya Rusumo, Namanga, Kasumulo na Holili.

### 4.4.2 Kuimarisha Uongezaji Thamani kwa Kushirikisha Sekta Binafsi

235. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Wizara ilipanga kuendelea na ujenzi wa vituo jumuishi viwili (2); kujenga miundombinu ya kukaushia, kuchakata na kuhifadhi muhogo na tangawizi; kulipa fidia ya viwanda na ghala katika maeneo ya Mzizima (Dar es Salaam) na Isaka (Shinyanga); na CPB kununua tani 78,897 za nafaka na mazao mchanganyiko.

236. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, Wizara kupitia Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB) imenunua tani 5,020.15 za nafaka. Kati ya hizo, tani 1,386.57 zimechakatwa na uchakataji unaendelea; na ujenzi wa vituo jumuishi vya kuchambua, kuhifadhi na kuchakata mazao ya bustani katika mikoa ya Iringa (Mufindi) na Mbeya (Rungwe) umefikia wastani wa asilimia 15.

237. ***Mheshimiwa Spika,*** zabuni kwa ajili ya ununuzi wa mashine ya kukaanga kahawa yenye uwezo wa kukaanga kilo 60 kwa siku imetangazwa; na mafunzo kuhusu uongezaji thamani wa mazao ya zabibu na korosho yametolewa kwa wakulima 250 na Maafisa Ugani 932 katika maeneo ya uzalishaji.

### 4.4.3 Kuongeza Mauzo ya Mazao ya Kilimo Ndani na Nje ya Nchi

238. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Wizara ilipanga kuongeza mauzo ya mazao nje ya nchi kutoka Dola za Marekani Bilioni 3.54 mwaka 2023/2024 hadi takriban Dola za Marekani Bilioni 4; TPHPA, kukamilisha mchakato wa ufunguzi wa masoko mapya 15; COPRA kuandaa na kusambaza miongozo kuhusu uuzaji, ununuzi, usindikaji, uhifadhi, usafirishaji na uingizaji wa mazao; kuandaa viwango vya uzalishaji wa mazao; kutoa mafunzo kuhusu viwango vya ubora wa mazao ya bustani kwa wakulima viongozi 4,500; kuwajengea uwezo wadau 5,350 kuhusu taratibu za usafirishaji wa mazao ya kilimo; na kuimarisha mifumo ya ununuzi na uuzaji wa mazao ya kilimo.

239. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kusimamia mauzo ya mazao ya kilimo nje ya nchi na kuwezesha kuongeza thamani ya mauzo hayo kutoka Dola za Marekani Bilion 3.54 mwaka 2023/2024 hadi Dola za Marekani Bilioni 3.73 mwaka 2024/2025. Aidha, kupita mifumo rasmi ya kidigiti imewezesha uuzaji wa mazao ya kakao, choroko, dengu, mbaazi, soya na ufuta kuongeza kutoka tani 268,757.77 zenye thamani ya Shilingi Bilioni 896.91

mwaka 2024 hadi tani 713,618.72 zenye thamani ya Shilingi Trilioni 1.40 mwaka 2025.

240. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, taratibu za ufunguzi wa masoko mapya 15 katika nchi 14 zipo katika hatua ya tathmini ya visumbufu hatarishi (Pest Risk Analysis - PRA) kwa masoko ya China (Vanilla na Nanasi), India (Vanila na Nanasi), Indonesia (Karafuu), Singapore (Karafuu), Israel (Parachichi), Malaysia (Parachichi), Canada (Pilipili Manga), Uturuki (Nanasi), Brazil (Nanasi), USA (Kakao), Afrika Kusini (Ndizi), Zambia (Viazi mviringo), Pakistan (Tumbaku) na Iraq (Tumbaku). Ufunguzi wa masoko hayo utawezesha nchi yetu kuongeza mauzo ya mazao ya kilimo katika nchi hizo na hivyo kuongeza ajira na kukuza uchumi.

241. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha mauzo ya mazao nje ya nchi yanaendelea kuongezeka na kwa kuzingatia mahitaji makubwa ya zao la parachichi katika masoko ya Uingereza na Marekani, Wizara kupitia TPHPA imeanza kutekeleza operesheni maalum inayolenga kudhibiti kisumbufu cha kikarantini aina ya Nondo wa Matunda katika zao la parachichi. Lengo la operesheni hiyo inayotekelezwa katika mikoa ya Njombe, Iringa na Mbeya itaiwezesha Tanzania kukidhi kigezo muhimu na pekee kilichobaki ili kufungua masoko ya parachichi katika nchi za Uingereza na Marekani.

242. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha wakulima wanazalisha mazao yanayokidhi mahitaji ya soko, Wizara kupitia COPRA imeandaa na kusambaza miongozo ya uzalishaji wa mazao ya ufuta, mbaazi, dengu, choroko, soya na maharage. Aidha, COPRA imeandaa na kusambaza Miongozo ya Uuzaji na Ununuzi wa Mazao jamii ya mikunde, viungo, kakao na parachichi. Pia, imeandaa viwango vya uzalishaji wa mazao ya ufuta, mikunde (mbaazi, dengu, choroko, soya na maharage), viungo (mdalasini, iliki, pilipili manga na karafuu), kakao, parachichi na vitunguu maji.

243. ***Mheshimiwa Spika,*** COPRA imetoa mafunzo kuhusu viwango vya uzalishaji na ubora wa mazao ya ufuta na mikunde kwa Maafisa Ugani 3,214 katika mikoa ya Mtwara (693), Lindi (691), Ruvuma (418), Morogogo (353), Kilimanjaro (153), Tanga (150), Arusha (133), Rukwa (109), Pwani (102), Katavi (94), Singida (77),Manyara (73), Dodoma (60), Kigoma (49), Simiyu (27), Mwanza (13), Shinyanga (8), Mara (6) Tabora (4) na Geita (1). Aidha, imewajengea uwezo wadau 503 kuhusu kanuni za kilimo cha mkataba, udhibiti ubora, usajili, utoaji wa vibali na taratibu za usafirishaji wa mazao ya kilimo ndani na nje ya nchi.

### 4.4.4 Kuimarisha Upatikanaji wa Mitaji

244. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Wizara kupitia AGITF ilipanga kuanzisha dirisha la dhamana na mitaji kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji wa mitaji yenye riba nafuu kwa wakulima katika Benki ya Ushirika Tanzania; kuendelea kushirikiana na taasisi za fedha katika kuimarisha utoaji wa mikopo yenye riba nafuu kwenye sekta ya kilimo; TADB kuongeza idadi ya taasisi za fedha zinazotumia mfuko wa dhamana wa TADB kutoka taasisi 19 hadi 21; na kuendelea na ujenzi wa ofisi ya AGITF Makao Makuu katika Mkoa wa Dodoma.

245. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, Wizara kupitia AGITF imetoa mikopo yenye riba nafuu yenye thamani ya Shilingi Milioni 100 kwa wakulima na Bilioni 5 zimepelekwa Benki ya Ushirika Tanzania kwa ajili ya kukopesha wakulima kupitia vyama vya ushirika; imeanzisha dirisha la dhamana na mitaji kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji wa mitaji yenye riba nafuu kwa wakulima katika Benki ya Ushirika Tanzania; na ujenzi wa jengo la Ofisi ya AGITF Makao Makuu katika Mkoa wa Dodoma umefikia asilimia 65.

246. ***Mheshimiwa Spika,*** TADB imeongeza idadi ya taasisi za fedha zinazotumia mfuko wa dhamana kutoka taasisi 19 hadi 22. Ongezeko hilo limewezesha upatikanaji wa mikopo yenye riba nafuu katika shughuli za kilimo.

### 4.4.5 Kuziwezesha Maabara za Serikali ziweze kufikia Viwango vya Ubora vinavyotakiwa Kimataifa

247. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TPHPA ilipanga kuanza ujenzi wa maabara ya kisasa katika Mkoa wa Njombe kwa ajili ya kupima ubora wa mazao; kuendelea kuimarisha maabara ya TPHPA Makao Makuu kwa kununua na kufunga vifaa vya kisasa vya maabara; TOSCI kukamilisha ukarabati wa maabara ya Makao Makuu na maabara ya kupima ubora wa mbegu iliyopo katika Mkoa wa Arusha; TARI kukamilisha ujenzi na ununuzi wa vifaa vya maabara ya magonjwa ya mimea na maabara ya kuzalisha miche kwa njia ya chupa katika kituo cha TARI Maruku; kununua vifaa vya maabara katika vituo vya TARI; na kukamilisha upatikanaji wa ithibati ya maabara ya udongo.

248. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, ukarabati wa maabara ya Taifa ya Mbegu iliyopo TOSCI Makao Makuu katika Mkoa wa Morogoro umefikia asilimia 92. Kukamilika

kwa maabara hiyo kutaongeza uwezo wa kuthibiti ubora wa mbegu kwa kutumia teknolojia za kisasa na kuendelea kulinda taswira ya nchi katika viwango vya ubora wa mbegu kimataifa na kufungua fursa mpya kwa uwekezaji katika uzalishaji na biashara ya mbegu. Vilevile, Wizara imeimarisha maabara ya TPHPA makao makuu kwa kukarabati, kununua na kufunga vifaa vya kisasa pamoja na kuwezesha upatikanaji wa ithibati ya kimataifa.

249. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza uzalishaji wa miche itakayosambazwa kwa wakulima, ujenzi wa maabara ya kuzalisha miche kwa njia ya chupa katika kituo cha utafiti cha TARI Maruku umefikia asilimia 30; na ujenzi wa maabara ya kudhibiti visumbufu vya mimea (patholojia) katika Kituo cha Utafiti cha TARI Naliendele umefikia asilimia 67. Vilevile, ili kuimarisha ubora wa mazao, mshauri elekezi wa ujenzi wa maabara ya TPHPA kwa ajili ya kupima ubora wa mazao katika Mkoa wa Njombe amepatikana.

## 4.5 Kuimarisha Maendeleo ya Ushirika

### 4.5.1 Kuimarisha Mifumo ya Kidijiti kwenye Vyama vya Ushirika na Mamlaka za Usimamizi

250. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Wizara kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania ilipanga kuunganisha Mfumo wa MUVU na mifumo mingine ya TEHAMA; na kukagua mifumo ya TEHAMA inayotumiwa na Vyama vya Ushirika kwa lengo la kutathimini ufanisi wake.

251. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, Tume imetengeneza *Portal* inayoonesha muhtasari (*Dashboard)* wa takwimu za kiushirika kupitia kiungo www.csmis.ushirika.go.tz/home. *Portal* hiyo inawezesha wananchi kupata taarifa za ushirika zikiwemo za usajili wa vyama, idadi ya wanachama, SACCOS, AMCOS, Vyama vya Upili na ukaguzi wa Vyama vya Ushirika. Vilevile, Tume imesajili vyama 6,545 vyenye jumla ya wanachama 3,357,366 katika Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika – MUVU kwa ajili ya kurahisisha utoaji wa huduma na usimamizi.

252. ***Mheshimiwa Spika,*** pia, imeunganisha mfumo wa MUVU na mifumo ya Wizara na Taasisi zingine za Serikali kupitia Mfumo Mkuu

wa Serikali wa GovESB kwa ajili ya kurahisisha upatikanaji wa taarifa, kuondoa udurufu wa mifumo na kupunguza gharama za uendeshaji. Mifumo ambayo imeunganishwa ni pamoja na mfumo wa Wizara (e-Kilimo na Bodi ya Sukari (CANE GROWERS MIS), Mifumo ya eGA (GoveESB, ERMS, mGov, GMS), Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF Online Self Services), Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (NaPA), Wizara ya Fedha (GePG), Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEECMIS) na Soko la Bidhaa Tanzania (OTS). Mifumo mingine ni pamoja na SCULT (SOMA), ELCT ND SACCOS (Core Banking System), Rotai (Mkulima Hub) na Climbing Up (Shamba bora).

### 4.5.2 Kuimarisha Usimamizi na Udhibiti wa Vyama vya Ushirika

253. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ilipanga kuendelea kuratibu na kusimamia utambuzi na uthaminishaji wa mali za Vyama vya Ushirika 5,973 na kuandaa Mpango wa Matumizi na Uendelezaji mali hizo; kuandaa kitabu kitakachoonesha fursa za uwekezaji zilizopo kwenye Vyama vya Ushirika; kufanya ufuatiliaji wa mali za Vyama vya Ushirika vilivyofutwa ikiwemo Chama Kikuu cha Ushirika cha Tanga (TARECU) na Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania.

254. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, utambuzi na uthaminishaji wa mali za kudumu za Vyama vya Ushirika unaendela kutekelezwa kupitia Kampuni ya World Map chini ya uratibu wa Shirikisho la Vyama vya Ushirika. Aidha, jumla ya Vyama vya Ushirika 5,934 katika mikoa ya Katavi (50), Mara (279), Geita (258), Mwanza (318), Simiyu (348), Njombe (206), Ruvuma (220), Pwani (184), Dar es Salaam (285), Morogoro (161), Arusha (158), Singida (134), Tanga (200), Lindi (182), Dodoma (99), Tabora (440), Manyara (119), Kagera (345), Mbeya (254), Kilimanjaro (215), Songwe (257), Shinyanga (229), Simiyu (348), Mtwara (433) na Kigoma (212) vimefanyiwa uhakiki na uthaminishaji wa mali zao. Mali hizo ni ardhi, majengo, mitambo, mashine, mifumo ya TEHAMA na samani za ofisi.

255. ***Mheshimiwa Spika,*** pia, rasimu ya Mpango wa Matumizi na Uendelezaji wa Mali zinazomilikiwa na Vyama vya Ushirika pamoja na kitabu cha kuonesha fursa zilizopo kwenye Vyama vya Ushirika imeandaliwa na itakamilishwa baada ya utambuzi na uthaminishaji wa mali za Vyama vya Ushirika kukamilika. Vilevile, Tume imefanya ufuatiliaji wa mali za TARECU LTD na kubaini kuwa baadhi ya mali hazijauzwa ikiwemo ghala (6) na majengo (2) Pia, ufuatiliaji wa mali za Shirikisho la Vyama vya Ushirika (TFC) unaendelea.

### 4.5.3 Kuhamasisha Vyama vya Ushirika Kujiendesha Kibiashara na Kuviwezesha kupata Mitaji

256. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa kushirikiana na Benki ya Ushirika Tanzania ilipanga kuendelea kuwezesha Vyama vya Ushirika kuingia katika mfumo rasmi wa kifedha kwa kuhamasisha Vyama Vikuu kuwa mawakala wa Benki na kufungua matawi; kusimamia Chama Kikuu cha Tandahimba na Newala (TANECU) kujenga kiwanda kipya cha kubangua korosho chenye uwezo wa kubangua tani 3,500; kufufua kiwanda cha kuchakata pamba cha Manawa na kulipa fidia za hisa za Serikali; na kufufua viwanda vya kuchakata pamba vya Buyagu na Magu.

257. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ilipanga kusimamia Chama Kikuu cha Ushirika cha Kahama (KACU) kujenga kiwanda cha kukamua mafuta ya kula; kusimamia Chama Kikuu cha Tabora (WETCU) kujenga kiwanda cha kutengeneza nyuzi za kusukia tumbaku; kuendelea kuimarisha mifumo rasmi na jumuishi ya biashara na masoko ya mazao katika Vyama vya Ushirika; na kuhamasisha Vyama vya Ushirika kuendelea kuuza mazao ya kilimo kupitia mifumo rasmi.

258. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi Machi 2026, Wizara kupitia Tume imehamasisha Vyama Vikuu vya Ushirika na SACCOS kubwa 52 kuwa mawakala wa Benki ya Ushirika Tanzania. Aidha, Vyama vya Ushirika 6,545 vimehamasishwa kuendelea kuwekeza katika Benki ya Ushirika Tanzania. Uhamasishaji huo umewezesha Vyama 1,540 kuwekeza kiasi cha Shilingi Bilioni 19 katika Benki ya Ushirika Tanzania. Pia, matawi manne (4) ya Benki ya Ushirika yaliyonzishwa katika mikoa ya Dodoma, Kilimanjaro, Tabora na Mtwara yanaendelea na utoaji wa huduma.

259. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhamasisha Vyama vya Ushirika kuongeza thamani ya mazao, Tume imeendelea kuratibu ujenzi wa kiwanda cha kubangua korosho cha TANECU chenye uwezo wa kubangua tani 3,500 kwa mwaka katika Wilaya ya Tandahimba. Vilevile, Tume inaendelea na ufufuaji wa kiwanda cha Magu ambapo utekelezaji umefikia asilimia 52. Pia, tathmini ya ufufuaji wa kiwanda cha Manawa imefanyika ambapo gharama ya ufufuaji wa kiwanda hicho ni Shilingi Bilioni 3.5 ambayo inahusisha fidia za hisa za wawekezaji ili kimilikiwe na ushirika. Baada ya kukamilisha malipo ya fidia, Chama Kikuu cha NYANZA kitaendelea kuratibu ufufuaji wa kiwanda hicho. Kadhalika, ufufuaji wa kiwanda

cha Buyagu umepangwa kufanyika baada ya ufufuaji wa Kiwanda cha Magu kukamilika.

260. ***Mheshimiwa Spika***, ujenzi wa kiwanda cha Chama Kikuu cha KACU chenye uwezo wa kuchakata mafuta tani 10,800 kwa mwaka umefikia asilimia 90. Pia, eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 12,000 katika Wilaya ya Nzega kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza nyuzi za kusukia tumbaku limepatikana. Mradi huo utatekelezwa kupitia TCJE.

261. ***Mheshimiwa Spika***, Tume kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuhamasisha Vyama vya Ushirika kuuza mazao kupitia mifumo rasmi ikiwemo mfumo wa Soko la Bidhaa Tanzania (TMX) ambapo hadi Machi 2026, umewezesha kuuza kilo 1,501,744,164 za mazao zenye thamani ya Shilingi 3,740,335,430,188. Hatua hiyo, imeongeza uwazi, kuimarisha ushiriki wa wanachama katika maamuzi ya kibiashara, kupunguza biashara isiyo rasmi na kuongeza mapato.

### 4.5.4 Kuhamasisha Ushirika kwenye Sekta Mbalimbali na Makundi Maalum

262. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume katika mwaka 2025/2026, ilipanga kuhamasisha vikundi 105 vinavyotekeleza shughuli za kiuchumi katika Sekta ya Kilimo, Mifugo,

Uvuvi, Madini, Viwanda na Fedha ili kuunda Vyama vya Ushirika; kuratibu uanzishwaji wa Kampuni ya Bima ya Ushirika; kuhamasisha Vyama vya Ushirika kujiunga na Bima mbalimbali; kuhamasisha wanaushirika kujiunga na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii; kuandaa Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Ushirika; na kuanzisha SACCOS kwenye AMCOS.

263. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi Machi 2026, Wizara kupitia Tume imehamasisha vikundi 25 vya vijana vyenye jumla ya wanachama 1,307 kuanzisha Vyama vya Ushirika 25 vikiwemo vya kilimo (12), mifugo (4), uvuvi (3), madini (1), viwanda (2) na fedha (3) katika mikoa ya Dar es Salaam, Tabora, Dodoma, Mwanza, Pwani na Arusha Aidha, Tume kupitia Shirikisho la Vyama vya Ushirika (TFC) imeratibu uanzishwaji wa Kampuni ya Bima ya Ushirika na taratibu kwa ajili ya kupata leseni ya uendeshaji kutoka TIRA zinaendelea.

264. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume kwa kushirikiana na Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania inaendelea kuratibu upatikanaji wa bima ya afya, bima ya mazao na hifadhi ya kinga ya jamii. Katika kuhakikisha upatikanaji wa bima katika zao la tumbaku, jumla ya wakulima 32,822 wamesajiliwa katika Halmashauri za Uyui, Nzega, Urambo na Manispaa ya Tabora. Kadhalika, Tume inaendelea na majadiliano na

NSSF kwa lengo la kuingia makubaliano rasmi ya kuwezesha vyama vya ushirika kupata mafao mbalimbali ya hifadhi ya jamii. Pia, rasimu ya Mpango Kabambe wa Maendeleo ya Ushirika imeandaliwa ili kuwezesha utekelezaji wa Dira 2050 katika maeneo yanayohusu ushirika.

265. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume imehamasisha Vyama Vikuu vya *Kagera Cooperative Union - KCU*, *Karagwe District Cooperative Union - KDCU*, Lindi Mwambao, *Arusha Cooperative Union - ACU,* Mirambo na Juhudi AMCOS kuanzisha SACCOS kwa lengo la kuongeza mitaji na kuwawezesha wanachama kupata mikopo yenye riba nafuu.

## 4.6 Kuimarisha Matumizi ya Mifumo ya TEHAMA Katika Uendelezaji wa Sekta ya Kilimo

### 4.6.1 Kuwekeza kwenye Matumizi ya Mifumo ya Kidijiti katika Sekta ya Kilimo

266. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Wizara ilipanga kuendelea kuimarisha mfumo wa *e – Kilimo* kwa kuendelea kujenga moduli ya taarifa za kilimo na taarifa za mifumo ya kijiografia; kuboresha mawasiliano na njia ya kubadilishana taarifa na wadau wa kilimo; kuanzisha maktaba ya kidijiti (e-library) kwa ajili ya kutunza kumbukumbu za kilimo; kuendelea kutoa huduma za ugani kwa wakulima kidijiti;

TPHPA kuanzisha moduli ya kufuatilia mazao; na kuanzisha *e-phyto.*

267. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wizara kupitia COPRA ilipanga kuendelea kusajili ghala, masoko, vituo vya ukaguzi wa mazao na wafanyabiashara wa mazao ya kilimo; AGITF kuboresha mfumo wa kidijiti kwa ajili ya usimamizi wa mikopo; na kuendelea kununua vifaa vya TEHAMA kulingana na teknolojia mpya na za kisasa.

268. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi Machi 2026 Wizara imekamilisha ujenzi wa moduli ya mbolea, ghala na mashamba ya wakulima; kuendelea kujenga na kufanya majaribio ya moduli ya taarifa za kilimo na kijiografia zinazopatikana kwa lugha nyepesi; imeboresha mawasiliano na njia ya kubadilishana taarifa za wadau wa kilimo (agriculture data digitalization value chain) kwa kuunganisha mfumo wa *e – kilimo* na mifumo mbalimbali ikiwemo TFRA kwa taarifa za usajili wa wakulima, TMA kwa takwimu za hali ya hewa, TRA kwa ajili ya masuala ya kodi na namba za utambulisho za mlipakodi. Vilevile, Wizara inaendelea na uunganishaji wa mfumo wa NIDA kwa ajili ya utambulisho wa mkulima.

269. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha mfumo wa *e – phyto* kwa ajili ya kuwezesha ubadilishanaji wa vyeti vya usafi wa mimea na *traceability* ili

kuwezesha ufuatiliaji wa viuatilifu vinavyoingia nchini na mazao ya kilimo ambayo hayajakidhi vigezo katika soko la kimataifa. Pia, imetoa mafunzo kuhusu ufuatiliaji wa vigezo vya kuingiza na kusafirisha mazao ya kilimo nje ya nchi kwa wakaguzi na Maafisa TEHAMA 70 katika moduli hizo.

270. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, kupitia mfumo wa *Crop Stock Dynamic System* - CSDS imesajili ghala 637 na kufanya jumla ya ghala zilizosajiliwa kufikia 2,431; imesajili masoko 20 na kufanya jumla ya masoko yaliyosajiliwa kufikia 398; imesajili vituo vya ukaguzi vitano (5) na kufanya jumla ya vituo vilivyosajiliwa kufikia 160 na imesajili wafanyabiashara wa mazao ya kilimo 1,798 na kufanya jumla ya wafanyabiashara waliosajiliwa kufikia 2,414.

271. ***Mheshimiwa Spika***, Kituo cha Huduma kwa Wateja (Kilimo Call Center) kimetoa huduma kwa wadau 9,837 ikiwemo uzalishaji na utunzaji wa mazao na matumizi sahihi ya pembejeo; taarifa za bei za mazao na masoko na matumizi sahihi ya zana za kilimo; na imeimarisha mawasiliano ya ugani kwa kujenga moduli ya kuwawezesha wakulima kupata huduma za ugani kilimo kutoka kwa maafisa ugani waliopo karibu yao.

### 4.6.2 Kuimarisha Mifumo ya Kidijiti itakayowezesha Upatikanaji wa Taarifa Sahihi kwa Wakati

272. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Wizara ilipanga kuendelea kuboresha mfumo wa *e – Kilimo* wa Wizara kwa kuunganisha na mifumo mingine ya Serikali; na kuanzisha kituo cha teknolojia za kilimo cha TEHAMA (AgriTech Hub).

273. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi Machi 2026, Wizara imeunganisha mfumo wa *e – Kilimo* na mfumo wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) kwa ajili ya taarifa za ruzuku, Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC) kwa ajili ya kupata taarifa za wakulima kupitia ushirika wa mazao, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) kwa takwimu za hali ya hewa na mfumo wa HCMIS (Utumishi) kwa uhakiki wa Maafisa Ugani.

274. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, imeunganisha na mfumo wa Serikali wa mGov kwa huduma ya jumbe fupi (Bulk SMS), mfumo wa TRA wa namba za utambulisho za mlipakodi (TIN) na mfumo wa forodha (TANCIS) kwa sehemu ya vibali vya biashara (Import and Export), mfumo wa BRELA pamoja na mfumo wa malipo wa Serikali (GePG).

## MAENEO MENGINE MUHIMU YALIYOTEKELEZWA NA WIZARA

### Kuongeza Matumizi ya Teknolojia na Mbinu za Kilimo Kinachohimili Mabadiliko ya Tabianchi

275. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, hususan kwa wakulima wa nyanda kame, Wizara kupitia TARI ilipanga kujenga uwezo wa kituo cha TARI - Hombolo kuwa kituo mahiri cha tafiti za mazao ya nyanda kame na mabadiliko ya Tabianchi; kuendelea kujenga Ofisi na miundombinu ya kisasa; kuendelea na utafiti wa zao la Tende; kuendelea na utekelezaji wa Mpango wa Sekta wa Usimamizi na Utunzaji wa Mazingira pamoja na Mpango wa Sekta wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi.

276. ***Mheshimiwa Spika,*** pia, ilipanga kuendelea kufanya tathmini ya athari ya mazingira na jamii kwenye mashamba makubwa 10; kuandaa Mipango ya Usimamizi wa Mazingira; kutoa mafunzo kuhusu utunzaji na usimamizi wa mazingira, mbinu na teknolojia za kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi ili kuwa na kilimo endelevu na himilivu kwa wakulima 800 katika mikoa ya Dodoma, Singida, Manyara na Tanga.

277. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi Machi 2026, Wizara imegundua na kutoa mbegu himilivu aina 54 za mazao ya choroko (mungbean), maharage, mbogamboga, mpunga, karanga, mtama na muhogo kwa lengo la kuongeza uhimilivu na uzalishaji wa mazao katika maeneo mbalimbali ya nchi kulingana na ikolojia husika.

278. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imekiwezesha kituo cha TARI – Hombolo kuwa Kituo Mahiri cha Utafiti wa Mazao ya Nyanda Kame na Teknolojia za Uhimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi ikiwemo kujenga kitalu nyumba (screen house) na miundombinu ya umwagiliaji. Kutokana na jitihada hizo, kituo kimeendelea kufanya utafiti wa mbegu bora za zao la tende kwa kuanzisha mashamba darasa manne (4) ya zao hilo na kusambaza miche 1,166 kwa wakulima 53 katika Vijiji vya Mita, Hombolo, Mvumi na Chalinze Nyama.

279. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha Wizara na wadau wa kilimo, wanatekeleza majukumu kwa kuzingatia sheria ya mazingira ya mwaka 2004, na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ambayo yana athiri utekelezaji wa shughuli za kilimo, Wizara imeandaa mpango wa pili wa usimaizi wa mazingira wa sekta ya kilimo ili kutekeleza Dira ya Taifa 2050

inayotuelekeza kuzingatia utunzaji wa mazingira kwa kilimo endelevu.

280. ***Mheshimiwa Spika,*** pia, Wizara imeendelea kuratibu tathmini ya athari ya mazingira na jamii katika miradi inayoendelea 24. Kadhalika, Wizara imeendela kutoa mafunzo kuhusu uhifadhi na usimamizi wa mazingira na kilimo himilivu kwa wanufaika 23,403 wakiwemo wakulima, maafisa ugani, maafisa mipango, maafisa mazingira, maendeleo ya jamii, watafiti, wasimamizi wa mashamba ya mbegu, wakaguzi na wasambazaji wa mbegu katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Geita, Iringa, Katavi, Kigoma, Mwanza, Morogoro, Mtwara, Njombe, Pwani, Shinyanga, Tabora na Tanga. **Kiambatisho Na. 7**. Orodha ya miradi iliyofanyiwa Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii.

**Masuala ya Jinsia**

281. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Wizara ilipanga kuendelea kuhakikisha uzingatiaji wa masuala ya jinsia katika kilimo cha mazao mbalimbali; kukamilisha mwongozo wa ujumuishaji wa masuala ya jinsia katika mnyororo wa thamani wa kilimo; kuendelea kuhakikisha kuwa masuala ya jinsia yanazingatiwa katika utoaji wa pembejeo za kilimo; kutoa mafunzo kupitia vikundi vya wakulima katika mashamba darasa; na

kuendelea kutekeleza shughuli kwa kuzingatia usawa wa jinsia.

282. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, Wizara imekamilisha Mwongozo wa Ujumuishaji wa Masuala ya Jinsia katika Mnyororo wa Thamani wa Kilimo. Vilevile, imetoa mafunzo kuhusu jinsia na ukatili wa kijinsia kwa wadau wa kilimo 2,751 (wanawake 1,146 na wanaume 1,605) katika mikoa ya Tanga, Mbeya, Tabora, Iringa, Arusha, Kilimanjaro pamoja na taasisi za TARI, ASA na TOSCI; na imeendelea kuhakikisha ujumuishwaji wa jinsia unapewa kipaumbele katika utekelezaji wa shughuli za kilimo.

283. ***Mheshimiwa Spika,*** pia, maafisa ugani 1,877 wamepatiwa mafunzo ya kilimo himilivu ambapo kati ya hao 573 ni wanawake. Vilevile, wakulima 18,749 wameshiriki katika mradi wa ruzuku makini (majaribio ya pembejeo na ushauri wa kushusha kemikali ya udongo) na kuwajengea uelewa kuhusu mbinu za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi katika mikoa ya Katavi, Iringa, Mwanza, Shinyanga, Geita na Njombe kati ya hao wanawake 8,002.

284. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeanzisha madawati tisa (9) ya jinsia katika ngazi ya Wizara makao makuu na taasisi zilizo chini ya Wizara (NiRC, TARI, TOSCI na ASA). Pia,

imefanya utambuzi wa watoa huduma 251 katika mikoa 18 iliyojumuisha Wilaya 37 kwa ajili ya waathirika wa masuala ya ukatili wa kijinsia katika maeneo yote ya utekelezaji wa Miradi iliyopo chini ya Wizara ya Kilimo.

**Afya na Ustawi wa Watumishi**

285. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Wizara ilipanga kuendelea kutoa huduma ya lishe na dawa kwa watumishi tisa (9) wanaoishi na VVU na UKIMWI; kuhamisha watumishi kushiriki michezo mbalimbali ili kupunguza athari za Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara; kuratibu vikao vinne (4) vya waelimisha rika; kutoa elimu ya VVU, UKIMWI, Afya ya Akili na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza; kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi kwa kuwapatia vitendea kazi, motisha na stahiki zao kwa mujibu wa Sheria, Kanuni, miongozo na taratibu; na kuwapatia nafasi za watumishi kujiendeleza kitaaluma.

286. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, Wizara imeendelea kutoa huduma ya lishe na dawa kwa watumishi wanaoishi na VVU na UKIMWI; imehamasisha watumishi 347 kushiriki michezo mbalimbali ili kupunguza athari za Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza kwa

ajili ya kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara; imeratibu vikao viwili (2) vya waelimisha rika kwa lengo la kubadilishana taarifa na kutathmini hali ya utekelezaji wa afua za VVU, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza mahala pa kazi katika Utumishi wa Umma; imetoa elimu ya VVU, UKIMWI, Afya ya Akili na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza kwa watumishi 428 kwa kushirikiana na Wizara ya Afya.

287. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha utendaji kazi wa watumishi kwa kuwapatia watumishi 640 kompyuta mpakato, magari 55 yamenunuliwa kwa ajili ya shughuli za ofisi sambamba na kutoa motisha na stahiki zao kwa mujibu wa sheria, taratibu, kanuni na miongozo.

# 5 MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2026/ 2027

288. ***Mheshimiwa Spika***, takwimu za Benki ya Dunia za mwaka 2023 zinaonesha kuwa wastani wa Shilingi 9,540 zinahitajika ili kukidhi kiwango cha kipimo cha maisha kwa siku kwa mwananchi mmoja mmoja ambapo ni sawa na Shilingi 3,482,100 kwa mwaka. Aidha, takwimu za Ofisi ya Taifa ya Takwimu zinaonesha kuwa kipato cha mtanzania kwa mwaka ni wastani wa Shilingi 3,000,000

ambacho kimechochewa na jitihada za Serikali tangu uhuru kupitia Sekta ya Kilimo.

289. ***Mheshimiwa Spika***, katika kufikia kiwango cha kipimo cha maisha kwa siku kinachohitajika kwa mwananchi mmoja mmoja kwa kuzingatia takwimu za Benki ya Dunia za mwaka 2023, Mpango na Bajeti ya Wizara ya Kilimo katika mwaka 2026/2027 umebeba maono mapana ya Serikali kupitia kilimo ambayo ni msingi na dira itakayoiwezesha Tanzania kufikia hadhi ya nchi ya kipato cha kati cha juu ifikapo mwaka 2050.

290. ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango na Bajeti ya Wizara ya Kilimo ya mwaka 2026/2027 umezingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa (2050); Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/2027 – 2030/2031); Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/2027; Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2025 - 2030; Hotuba ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa wakati wa Ufunguzi wa Bunge la 13 tarehe 14 Novemba, 2025 Jijini Dodoma; Sera ya Taifa ya Kilimo ya mwaka 2013; Sera ya Taifa ya Umwagiliaji ya mwaka 2010; Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya mwaka 2002; na Mpango Kabambe wa Mageuzi ya Kilimo 2050 (Tanzania Agriculture Master Plan 2050) itakayotekelezwa kupitia Agenda

10/30 na Mpango Mkakati wa Wizara ya Kilimo wa mwaka 2026/2027 - 2030/2031.

291. ***Mheshimiwa Spika,*** pia, umezingatia Agenda za Kikanda na Kimataifa ikiwemo Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) na Azimio la Kampala kuhusu Programu ya Kuendeleza Kilimo Barani Afrika (CAADP 2026 - 2035); Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2026/2027; Maoni na Ushauri wa Kamati za Kudumu za Bunge; Maoni ya Baraza la Rais la Ushauri wa Kilimo na wadau wa maendeleo; masuala mtambuka ya jinsia, mazingira, lishe, mabadiliko ya tabianchi, vijana na kutokomeza ajira kwa watoto katika Sekta ya Kilimo, Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza, VVU na UKIMWI.

292. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara itaendelea kutekeleza vipaumbele sita (6), ambavyo ni: Kuongenza Tija na Uzalishaji; Kuchangia Kuongeza Ajira zenye Staha na Ushiriki wa Vijana na Wanawake Kwenye Kilimo; Kuimarisha Usalama wa Chakula na Lishe; Kuimarisha Upatikanaji wa Mitaji, Masoko na Mauzo ya Mazao Nje ya Nchi; Kuimarisha Maendeleo ya Ushirika; na Kuimarisha Matumizi ya Mifumo ya TEHAMA katika Uendelezaji wa Sekta ya Kilimo.

293. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha kuwa vipaumbele vilivyopangwa vinafikiwa, Wizara imepanga kutekeleza mikakati 30 kama ifuatavyo:-

**i. Kuongeza Tija na Uzalishaji;**

294. ***Mheshimiwa Spika***, mikakati itakayozingatiwa katika eneo hili ni pamoja na:-

a) Utafiti wa Kilimo;
b) Uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora na miche;
c) Kutoa ruzuku ya mbolea, mbegu na viuatilifu;
d) Usajili wa wakulima na urasimishaji wa shughuli za kilimo;
e) Kuimarisha huduma za ugani;
f) Kuanzisha mashamba makubwa ya pamoja na kupima afya ya udongo;
g) Uendelezaji wa kilimo cha umwagiliaji; na
h) Uanzishaji wa vituo vya kutoa huduma za zana za kilimo.

### ii. Kuchangia Kuongeza Ajira zenye Staha na Ushiriki wa Vijana na Wanawake kwenye Kilimo

295. ***Mheshimiwa Spika***, kwa kuzingatia changamoto ya upatikanaji wa ajira hususan kwa vijana na wanawake, Wizara imepanga kutekeleza mikakati ifuatayo:-

a) Kuwezesha uendelezaji wa programu ya BBT ngazi ya Halmashauri;
b) Kuwezesha ujenzi wa miuondombinu ya umwagiliaji kwa wakulima wadogo (BBT visima);
c) Kuwezesha upatikanaji wa mikopo kwa vijana na wanawake (BBT mitaji);
d) Kuwezesha vijana na wanawake kuzalisha miche (BBT miche);
e) Kuwezesha vijana na wanawake kuongeza thamani ya mazao; na
f) Kuwezesha vijana na wanawake kutoa huduma za ugani (BBT Ugani).

### iii. Kuimarisha Usalama wa Chakula na Lishe

296. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara itaendelea kuimarisha hifadhi ya chakula ili kuwezesha nchi kuendelea kujitosheleza katika usalama wa chakula na lishe. Katika eneo hili, mikakati itakayotekelezwa ni pamoja na:-

a) Uwekezaji kwenye Miundombinu ya Uhifadhi ili Kufikia Uwezo wa Kuhifadhi tani 3,000,000 ifikapo Mwaka 2030
b) Kuiongezea NFRA uwezo wa kununua mazao ya wakulima ili kuongeza hifadhi ya chakula; na
c) Kuhamasisha matumizi ya mazao yaliyoongezewa virutubishi ndani ya nchi ili kukabiliana na matatizo ya lishe nchini.

**iv. Kuimarisha Upatikanaji wa Mitaji, Masoko na Mauzo ya Mazao Nje ya Nchi**

297. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha wananchi wananufaika zaidi na shughuli za kilimo, Wizara imepanga kutekeleza mikakati inayolenga kuimarisha kipato cha wananchi na kuondoa umaskini. Mikakati hiyo ni pamoja na:-

a) Kujenga miundombinu ya masoko ya mazao ya kilimo katika Halmashauri mbalimbali;
b) Kuimarisha uongezaji thamani kwa kushirikisha Sekta Binafsi;
c) Kuongeza mauzo ya mazao ya kilimo ndani na nje ya nchi;
d) Kuimarisha upatikanaji wa mitaji; na

e) Kuziwezesha maabara za Serikali kufikia viwango vya ubora unaotakiwa kimataifa.

### v. Kuimarisha Maendeleo ya Ushirika

298. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara imepanga kutekeleza mikakati ifuatayo ili kuimarisha maendeleo ya ushirika nchini:-

a) Kuimarisha ukaguzi na usimamizi wa uendeshaji wa vyama vya ushirika;
b) Kuimarisha ushirika kwenye sekta mbalimbali na makundi maalum; na
c) Kuhamasisha vyama vya ushirika kujiendesha kibiashara.

### vi. Kuimarisha Matumizi ya Mifumo ya TEHAMA katika Uendelezaji wa Sekta ya Kilimo

299. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika shughuli za kilimo, Wizara imepanga kutekeleza mikakati ifuatayo:-

a) Kuimarisha mifumo ya kidijiti itakayowezesha upatikanaji wa taarifa sahihi kwa wakati; na

b) Kuwekeza kwenye matumizi ya mifumo ya kidijiti katika Sekta ya Kilimo.

## KAZI ZITAKAZOTEKELEZWA KWA KUZINGATIA VIPAUMBELE VYA MWAKA 2026/2027

### 5.1 Kuongeza Tija na Uzalishaji

#### 5.1.1 Utafiti wa Kilimo

300. ***Mheshimiwa Spika,*** utafiti ni msingi wa ukuaji wa Sekta ya Kilimo unaowezesha ugunduzi na matumizi ya teknolojia za kisasa ikiwemo mbegu bora, matumizi ya udongo na maji, udhibiti wa visumbufu vya mimea na mazao na kuongeza thamani ya mazao ili kuongeza uzalishaji na tija.

301. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha matokeo ya tafiti yanamnufaisha mkulima wa kitanzania na kuendeleza teknolojia za kilimo kwa mwaka 2026/2027, Wizara kupitia TARI itakamilisha ugunduzi na kusajili aina 73 za mbegu bora za mazao ya kimkakati ya nafaka, jamii ya mikunde, biashara, mizizi, matunda na mafuta kwa lengo la kuongeza aina mpya za mbegu zinazoendana na mahitaji ya soko. Vilevile, itaendelea na ugunduzi wa teknolojia 20 za kanuni za kilimo bora kwa mazao ya nafaka, jamii ya mikunde, biashara, mizizi, matunda na mafuta kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa mazao, kuongeza ufanisi wa

matumizi ya rasilimali na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

302. ***Mheshimiwa Spika,*** TARI itaendelea na tafiti 28 za teknolojia za afya ya udongo kwa mazao ya kimkakati ya nafaka, jamii ya mikunde, biashara, mizizi, matunda na mafuta. Kukamilika kwa tafiti hizo kutawezesha mapendekezo ya matumizi sahihi ya mbolea. Vilevile, itakamilisha uchambuzi wa sampuli 34 za udongo zilizokusanywa kwa ajili ya utafiti wa afya ya udongo ili kubaini kiwango sahihi cha uwekaji wa mbolea ya kupandia na kukuzia kwa tumbaku ya mvuke katika wilaya za Uyui, Kaliua, Uvinza, Kasulu, Tanganyika, Chunya, Namtumbo, Kahama, Mbogwe na Serengeti. Aidha, TARI itapokea sampuli za udongo 2,300 na sampuli 200 za mbolea kutoka kwa wadau kwa ajili ya kuzichambua na kushauri matumizi sahihi.

303. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha uzalishaji wa mbegu za utafiti, Wizara kupitia TARI itazalisha mbegu tani 1,870.5 za mazao ya nafaka, mikunde, mafuta na mazao ya bustani. Kati ya hizo, mbegu mama ni tani 53.12, mbegu za awali tani 343.3, mbegu za msingi tani 831.1 na mbegu zilizothibitishwa tani 642.98. Vilevile, itakusanya na kutunza nasaba 2,325 za mbegu za asili za mazao ya mahindi (132), mpunga (70), kunde (20), mbaazi (6) maharage (86), mbegu za mazao ya

miti (11), ufuta (600), karanga (750), mtama (150), njugumawe (100), muhogo (200) na viazi vitamu (200).

304. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha matokeo ya utafiti yanawafikia wakulima, TARI itahaulisha teknolojia 381 zinazojumuisha teknolojia za mbegu bora (139); kanuni za kilimo bora (175); afya ya udongo (9); teknolojia za kuongeza thamani ya mazao (24) na teknolojia za kudhibiti wadudu, magonjwa na viuatilifu vya visumbufu vya mimea (34).

305. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha miundombinu ya utafiti nchini, TARI itaendelea na ujenzi wa maabara za kuzalisha miche kwa njia ya chupa (tissue culture lab) katika vituo vya TARI Maruku na TARI Tengeru. Vilevile, itakarabati maabara ya TARI Mikocheni na kununua vifaa kwa ajili ya maabara ya kituo cha TARI Mlingano. Aidha, itajenga maabara mbili (2) za kuzalisha mbegu katika vituo vya TARI Ilonga na TARI Selian pamoja na kuendelea na ujenzi wa maabara ya kudhibiti visumbufu vya mimea katika kituo cha TARI Naliendele.

306. ***Mheshimiwa Spika,*** TARI itaendelea na ujenzi wa kituo cha *Bioscience* katika Mkoa wa Morogoro kwa ajili ya kutoa huduma za kisasa za kisayansi katika utafiti wa mbegu, wadudu, magonjwa, uhimilivu wa athari za

mabadiliko ya tabianchi, udongo, uhandisi wa kibaolojia (Bio - engineering) na kanzidata za taarifa za kibaolojia (Bioinformatics). Vilevile, itaendelea na ujenzi wa Benki ya mbegu katika kituo cha TARI Selian, ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu (Njedengwa, Dodoma) na ujenzi wa nyumba tatu (3) za watumishi, jiko na hosteli katika Kituo cha Utafiti wa Kahawa cha Mwayaya (Buhigwe).

307. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kulinda mashamba ya utafiti wa mbegu dhidi ya uvamizi. TARI itaendelea na ujenzi wa uzio katika mashamba ya utafiti wa mbegu katika vituo vya TARI Uyole, TARI Kifyulilo, TARI Dakawa, TARI Hombolo, TARI Maruku, TARI Ifakara, TARI Kihinga, TARI Mlingano, TARI Ukiriguru na TARI Tumbi. Aidha, italipa fidia kwa wananchi watakaohamishwa katika kituo cha TARI Uyole ili kupisha ujenzi wa uzio. Pia, itaendelea na taratibu za upatikanaji wa hatimiliki katika vituo 17 na mashamba ya majaribio 18.

308. ***Mheshimiwa Spika,*** TARI itaendelea kukarabati nyumba 49 za watumishi katika vituo vya TARI Ilonga (24), TARI Mlingano (15) na TARI Tumbi (10) na ukarabati wa ofisi nne (4) katika vituo vya TARI Ilonga (3) na Tumbi (1). Aidha, itaendelea na ujenzi wa ofisi moja (1) katika kituo cha TARI Hombolo na ofisi ya TARI makao makuu Njedengwa - Dodoma.

309. ***Mheshimiwa Spika,*** TARI itaendelea na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji itakayomwagilia eneo lenye ukubwa wa hekta 2,160.9 katika vituo 17 vya TARI Selian (145), TARI Kihinga (150), TARI Ilonga (215), TARI Hombolo (70), TARI Kifyulilo (26.5), TARI Dakawa (50), TARI Uyole (920), TARI Kibaha (20), TARI Maruku (32), TARI Tengeru (50), TARI Ifakara (36.4), TARI Tumbi (60), TARI Naliendele (37), TARI Mikocheni (60), TARI Ukiriguru (247), TARI Mlingano (20) na TARI Uyole – Isimani (22).

310. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha uhifadhi wa mbegu za utafiti zinazozalishwa, Wizara kupitia TARI itaendelea na ujenzi wa ghala 11 zenye uwezo wa kuhifadhi tani 415 kila moja katika vituo vya TARI Tumbi - Tabora, TARI Selian - Arusha, TARI Hombolo - Dodoma, TARI Dakawa - Morogoro, TARI Naliendele - Mtwara, TARI Uyole - Mbeya, TARI Kifyulilo - Iringa, TARI Ifakara - Morogoro, TARI Ilonga - Morogoro, TARI Ukiriguru - Mwanza na TARI Maruku – Kagera.

311. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia TARI, imepanga kununua na kusimika mashine ya kukaanga kahawa yenye uwezo wa kukaanga kilo 60 kwa siku katika Kituo cha Utafiti wa Kahawa cha Mwayaya (Buhigwe). Aidha, itanunua zana za kilimo 15 kwa ajili ya shughuli za kilimo. Kati ya hizo, mashine za

kuvunia mazao (2), kunyunyizia dawa (2), kupandia (2), trekta (3), *harrow* (2), *plough* (2) na *trailer* (2). Pia, itanunua magari (2), pikipiki (3) na mashine za *seed treatment*, *cold rooms facilities* na *seed graders.* Ununuzi wa vitendea kazi hivyo utaimarisha utendaji kazi katika vituo vya utafiti.

### 5.1.2 Uzalishaji na Usambazaji wa Mbegu Bora na Miche

**Uzalishaji wa Mbegu**

312. ***Mheshimiwa Spika***, mahitaji ya mbegu bora nchini kwa mwaka ni tani 127,650. Katika mwaka 2026/2027, Wizara kwa kushirikiana na Sekta Binafsi imepanga kuongeza upatikanaji wa mbegu bora kutoka tani 79,214.48 mwaka 2025/2026 hadi tani 127,650. Vilevile, Wizara itaongeza uzalishaji wa mbegu bora ndani ya nchi kutoka tani 47,702.45 mwaka 2025/2026 hadi tani 105,000 mwaka 2026/2027.

313. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha upatikanaji wa mbegu bora nchini, ASA itazalisha mbegu bora tani 27,219 kupitia kilimo cha mkataba kwa kampuni na wakulima kwenye eneo lenye ukubwa wa hekta 12,470 katika mashamba ya mbegu ya ASA. Kati ya hizo, ufuta tani 490, mahindi tani 17,632, mpunga tani 5,108, maharage tani 412,

choroko tani 110, mbaazi tani 160, mtama tani 300, alizeti tani 1,907 na ngano tani 1,100.

**Miundombinu ya Uzalishaji Mbegu**

314. ***Mheshimiwa Spika***, ASA itafungua mashamba mapya ya uzalishaji wa mbegu yenye ukubwa wa hekta 1,900 katika mashamba ya mbegu ya Mbozi (hekta 600), Msimba (hekta 500) na Luhafwe (hekta 800). Vilevile, ASA itaendelea na ujenzi wa ghala tano (5) zenye uwezo wa kuhifadhi mbegu tani 1,800 kila moja katika mashamba ya mbegu ya Msimba, Msungura, Dabaga, Namtumbo na Mbozi.

315. ***Mheshimiwa Spika***, ili kulinda mashamba ya mbegu dhidi ya uvamizi, ASA itaendelea na ujenzi wa uzio katika mashamba ya mbegu ya Namtumbo (km 33.3), Mwele (km 14), Kilangali (km 23), Luhafwe (km 13), Msungura (km 5), Mbozi (km 40), Dabaga (km 22), Bugaga (km 10) na Arusha (km 17).

316. ***Mheshimiwa Spika***, ASA itaendelea na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika eneo lenye ukubwa wa hekta 3,000 katika mashamba ya mbegu ya Msimba (200), Mbozi (500), Namtumbo (1,000), Msungura (100), Arusha (240), Kilimi (160) na Luhafwe (800). Vilevile, itaendelea na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya mbegu yenye ukubwa wa hekta 700 ya

Mbozi (100), Namtumbo (400), Arusha (100) na Msimba (100).

317. ***Mheshimiwa Spika***, ASA itajenga makaushio matatu (3) ya mbegu katika mashamba ya mbegu ya Namtumbo, Luhafwe na Igunga. Vilevile, itakarabati ofisi mbili (2) katika mashamba ya mbegu ya Mwele na Mbozi. Pia, itajenga nyumba 29 za watumishi katika mashamba ya mbegu ya Namtumbo (3), Bugaga (3), Arusha (3), Kilangali (3), Mbozi (3), Msimba (3), Dabaga (3), Mwele (3) na Kilimi (5) ili kuimarisha utendaji kazi wa watumishi katika mashamba ya mbegu.

**Uthibiti wa Ubora wa Mbegu**

318. ***Mheshimiwa Spika***, msingi wa mapinduzi ya kilimo unaanza na mbegu bora ambapo hubeba hatma ya mavuno yetu na kiini cha tija na usalama wa chakula na nchi kwa ujumla. Serikali imekuwa ikipokea malalamiko kutoka kwa baadhi ya wakulima kuhusu uwepo wa mbegu zisizo na ubora za mazao mbalimbali kutoka kwa wafanyabiashara wasio waaminifu.

319. ***Mheshimiwa Spika***, katika kukabiliana na changamoto iliyopo ya uuzaji wa mbegu zisizo na ubora, jambo ambalo ni hujuma ya wazi dhidi ya mkulima, Wizara katika mwaka 2026/2027, itatoa mafunzo kwa vitendo

(Demonstration) kwa wakulima na wauzaji wa mbegu yatakayolenga kuwawezesha kutofautisha mbegu zisizo na ubora na mbegu bora.

***Nitoe wito kwa wafanyabiashara wasio waaminifu wanaouza mbegu zisizo na ubora kufahamu kuwa mkono wa sheria hautawaacha salama. Niwasihi wakulima wa nchi hii kuwa macho na kuhakikisha wananunua mbegu bora kutoka kwa mawakala waliosajiliwa na kukagua kwa makini nembo za uthibiti ubora kwenye vifungashio na siyo vinginevyo.***

320. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha uthibiti wa ubora wa mbegu nchini, TOSCI itanunua mtambo wa kuchapisha lebo zinazotumika katika vifungashio vya mbegu kwa lengo la kuongeza ufanisi na kujenga uwezo wa utoaji wa lebo za kuthibiti ubora, kuepuka vihatarishi vya kiusalama na kuhakikisha upatikanaji wa mbegu bora kwa wakulima kwa wakati. Vilevile, itanunua maeneo kwa ajili ya ujenzi wa maabara za mbegu katika mikoa ya Dodoma, Geita na Mbeya.

321. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia TOSCI, itanunua vifaa vya kisasa kwa ajili ya Maabara ya Taifa ya Mbegu yenye uwezo wa kufanya uchambuzi wa kikemikali na lishe, vifaa vya ofisi na magari sita (6). Vilevile,

itanunua na kusimika Mtambo wa kuchapisha lebo za ubora zitakazotumika katika vifungashio vya mbegu na kutoa lebo za ubora wa mbegu 45,000,000. Pia, itaendelea na ukarabati wa maabara ya Kanda ya Kaskazini (Arusha) pamoja na ujenzi wa maabara tatu (3) katika Kanda ya Magharibi (Tabora), Kusini (Mtwara) na Kanda ya Ziwa (Mwanza).

322. ***Mheshimiwa Spika***, TOSCI itaendelea na ukaguzi wa mashamba 1,669 ya mbegu yenye ukubwa wa hekta 26,600, miche 20,000,000, maduka 2,800 na ghala za kuhifadhi mbegu 167. Vilevile, itatoa mafunzo kwa wakaguzi wa mbegu walioidhinishwa 115 katika ngazi ya Halmashauri, wakulima 890 wa mbegu katika Mfumo wa Ubora wa Mbegu Uliobainishwa na Mkulima (UMBEGU-QDS), na wafanyabiashara wa mbegu 6,500. Pia, itakusanya sampuli za mbegu 4,820 kwa ajili ya majaribio ya ubora wa mbegu ili kuongeza mbegu zilizothibitishwa ubora.

323. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha upatikanaji wa aina mpya za mbegu nchini na kumwezesha mkulima kuwa na chaguo la aina za mbegu, TOSCI itafanya majaribio ya utambuzi wa aina mpya za mbegu 80, majaribio ya umahiri wa aina mpya za mbegu 30, majaribio ya uhalisia wa mbegu zilizopo katika uzalishaji 250, pamoja na tafiti za kiuchunguzi juu ya mahitaji ya mbegu nchini.

324. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha upatikanaji wa takwimu na taarifa za mbegu bora nchini, TOSCI itaboresha Mfumo wa *TOSCI Online Application Services* (TOAS) ili kuwawezesha wakulima na wadau wengine wa tasnia ya mbegu nchini kupata taarifa za mbegu bora kwa urahisi na kwa wakati.

**Uzalishaji wa Vipando**

325. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha miche inazalishwa na kusambazwa kwa wakulima, Wizara itaimarisha ufuatiliaji na usimamizi wa miche kwa lengo la kuhakikisha miche hiyo inawafikia wakulima kwa wakati ili kuongeza uzalishaji na tija katika mazao ya kilimo. Pia, itahamasisha vikundi vya vijana na wanawake kushiriki katika uzalishaji wa miche ambao utachangia upatikanaji wa ajira na kupunguza upotevu wa miche.

326. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2026/2027, Wizara kwa kushirikiana na sekta binafsi itazalisha miche 46,603,721 ya mazao ya kakao (559,500), karafuu (508,563), parachichi (1,727,400), chikichi (2,000,000), korosho (5,000,000), kahawa (30,000,000), migomba (750,758), zabibu (700,000), miembe (17,500), michungwa (20,000), minazi (111,000), mkonge (3,500,000), tufaha (600,000), iliki (109,000) na chai (1,000,000). Pia, TARI

itazalisha na kusambaza vipando vya viazi lishe 3,400,000 na pingili za muhogo 5,670,000.

### 5.1.3 Utoaji wa Ruzuku ya Mbolea, Mbegu na Viuatilifu

#### a) Upatikanaji wa mbolea

327. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara kupitia Mamlaka ya Mbolea Tanzania (TFRA) imepanga kuratibu upatikanaji wa mbolea nchini kufikia tani 1,500,000 za mbolea. Kati ya hizo, TFC itanunua na kusambaza mbolea tani 220,500 ikiwemo tani 150,000 kwa ajili ya mazao ya chakula, tani 70,000 kwa ajili ya zao la tumbaku na tani 500 kwa ajili ya zao la chai. Pia, itasimika mitambo ya kuchanganya mbolea (Bulk Blending Facilities) katika Mkoa wa Dar es Salaam yenye uwezo wa kuchanganya tani 300,000 kwa mwaka kwa ajili ya mazao ya parachichi, chai na mazao mengine kulingana na mahitaji ya wakulima na hali ya afya ya udongo kwenye maeneo mbalimbali.

328. ***Mheshimiwa Spika,*** TFC itanunua na kusambaza tani 50,000 za mbolea kutoka kwa wazalishaji wa ndani ili kuviwezesha viwanda vya ndani kuongeza uzalishaji na kupunguza utegemezi wa uagizaji mbolea kutoka nje ya nchi. Pia, itanunua malori

matano (5) yenye uwezo wa kubeba mbolea tani 30 kila moja ili kuwezesha usambazaji wa mbolea.

329. ***Mheshimiwa Spika,*** TFC itaanzisha kiwanda cha kutengeneza chokaa mazao chenye uwezo wa kuzalisha tani 250,000 hadi 500,000 kwa mwaka katika eneo lenye ukubwa wa hekta 39 Kata ya Mzizima, Halmashauri ya Jiji la Tanga, Mkoa wa Tanga. Vilevile, itajenga ghala mbili (2) zenye uwezo wa kuhifadhi tani 5,000 za mbolea kila moja katika mikoa ya Tanga (Tanga Jiji) na Ruvuma (Tunduru).

330. ***Mheshimiwa Spika,*** TFC itakarabati ghala nne (4) za kuhifadhi mbolea zenye uwezo wa kuhifadhi tani 55,000 zilizopo katika mikoa ya Mbeya (15,000), Mwanza (5,000), Tabora (20,000) na Rukwa (15,000). Pia, itaendelea kutafuta mbia kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha mbolea aina ya *Triple Super Phosphate* – TSP, *Single Super Phosphate* – SSP, MAP, Urea na DAP kwa kutumia madini ya makaa ya mawe na *phosphate* katika Mkoa wa Songwe.

**b) Ruzuku ya Mbegu**

331. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara kupitia COPRA imepanga kusambaza mbegu bora za alizeti tani 120 na tani 480 za mazao ya mikunde na mafuta

ikiwemo ufuta 100, choroko 100, dengu 100, soya 20 na mbaazi 160 kwa mpango wa ruzuku kwa lengo la kuwawezesha wakulima kupata mbegu bora kwa bei nafuu na kuongeza tija na uzalishaji. Mpango huu unalenga kuwafikia wakulima 139,000 katika maeneo ya uzalishaji nchini.

### c) Upatikanaji wa Viuatilifu na Udhibiti wa Visumbufu vya Mazao na Mimea

332. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA) katika mwaka 2026/2027, itaendelea kuimarisha matumizi sahihi ya viuatilifu ili kudhibiti magonjwa na wadudu waharibifu wa mazao na mimea na hivyo kuwezesha usalama wa chakula pamoja na kukuza soko la bidhaa za kilimo ndani na nje ya nchi. Katika kufanikisha hayo Wizara itatekeleza yafuatayo:-

333. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha uzalishaji wa mazao ya kilimo unaongezeka na kupunguza upotevu wa mazao kabla ya kuvuna, Wizara kupitia TPHPA, itanunua na kusambaza lita 100,000 za viuatilifu kwa ajili ya udhibiti wa milipuko ya visumbufu vya mimea na mazao na kwa kutumia wadudu rafiki. Aidha, katika maeneo yasiyofikika kwa urahisi na yenye athari za milipuko ya visumbufu vya mimea na mazao, TPHPA

itadhibiti visumbufu hivyo kwa kutumia teknolojia mbalimbali ikiwemo udhibiti kwa njia ya anga ambapo itatumia ndege ya kilimo na ndege nyuki za kunyunyizia viuatilifu.

334. ***Mheshimiwa Spika,*** TPHPA itazalisha aina 10 za wadudu rafiki kwa ajili ya udhibiti wa visumbufu kwenye mazao ya muhogo, mahindi na baadhi ya mazao ya bustani. Vilevile, itasajili wafanyabiashara wa viuatilifu nchini ili kupunguza viuatilifu feki. Aidha, itaendelea na ukarabati wa Ofisi ya Makao Makuu, Ofisi tatu (3) za Kanda za Magharibi, Nyanda za Juu Kusini na Mashariki ili kupeleka huduma karibu na wananchi. Pia, itaanza ujenzi wa maabara ya ubora wa mazao katika Mkoa wa Njombe ili kuimarisha uchunguzi na udhibiti wa visumbufu vya mazao na kuongeza upatikanaji wa masoko ya kimataifa.

335. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha mazao yanayouzwa nje na ndani ya nchi yanakidhi viwango ili kulinda afya ya mlaji, mazingira na kukuza biashara, TPHPA itakagua tani 1,500,000 za mazao na mimea. Aidha, itapima viwango vya mabaki ya viuatilifu (Maximum Residual Limits – MRLs) kwa mazao ya chakula. Pia, itatoa mafunzo kwa wakulima 9,000, wafanyabiashara wa pembejeo za kilimo 252 na Maafisa Ugani 6,748 kuhusu utambuzi, ufuatiliaji na mbinu bora za

kudhibiti visumbufu vamizi kwa lengo la kuongeza tija.

336. ***Mheshimiwa Spika,*** TPHPA itafanya majaribio 1,000 ya ufanisi wa kibaiolojia wa viuatilifu vipya kwa ajili ya usajili. Vilevile, itaendelea na ukaguzi wa maduka ya pembejeo za kilimo na ghala za kuhifadhi viuatilifu 4,000 kwa ajili ya kudhibiti ubora wa viuatilifu. Aidha, ili kuhakikisha katika mipaka yote tunakuwa na vituo kwa ajili ya kutoa huduma kwa wafanyabiashara na kulinda afya ya mimea, TPHPA itafungua ofisi za ukaguzi wa mazao na mimea katika vituo 14 vya mipakani katika Kanda ya Ziwa, Kaskazini, Magharibi, Nyanda za Juu Kusini, Mashariki na Kusini.

337. ***Mheshimiwa Spika,*** TARI itaendelea na tafiti 18 za visumbufu vya mimea (magonjwa na wadudu) kwa mazao ya korosho, mitende, miwa, maharage, viazi mviringo, soya, mbogamboga, ngano, pamba, kahawa, minazi na miti ya miyombo ili kudhibiti visumbufu na kuongeza tija katika uzalishaji.

### 5.1.4 Usajili wa Wakulima na Urasimishaji wa Shughuli za Kilimo

338. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kurahisisha upatikanaji wa huduma za kilimo kidijiti, Wizara katika mwaka 2026/2027, itaendelea na usajili wa wakulima, wafanyabiashara wa

mazao ya kilimo, watoa huduma za ugani, ghala na pembejeo za kilimo. Vilevile, kupitia TFRA itaendelea kutoa hatimiliki na kadi za kielektroniki (smart card) kwa wakulima 10,000 kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa huduma mbalimbali ikiwemo kununua pembejeo za kilimo.

### 5.1.5 Kuimarisha Huduma za Ugani

### Vitendea Kazi na Miundombinu ya Kujifunzia

339. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha utoaji wa huduma za ugani nchini, Wizara katika mwaka 2026/2027, imepanga kununua na kusambaza vitendea kazi kwa Maafisa Ugani ikiwemo magari 107, pikipiki 1,000 na mavazi maalum ya utambulisho 2,021. Vilevile, katika kuimarisha uhaulishaji wa teknolojia za kilimo kwa wakulima ili kuongeza tija na uzalishaji, Wizara itaendelea na ujenzi wa miundombinu katika viwanja vya maonesho ya wakulima ya Nanenane vya Dkt. John Samuel Malecela (Dodoma) na John Mwakangale (Mbeya).

340. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TARI itaendelea kuimarisha vituo sita (6) mahiri vya usambazaji na uhaulishaji wa teknolojia kwa kuviwekea miundombinu ya umwagiliaji katika viwanja vya maonesho ya nanenane vya Nyakabindi, Themi, Nyamuhongolo,

Fatuma Mwasa, Ngongo na John Mwakangale. Lengo ni kuwezesha utoaji wa huduma na uhaulishaji wa teknolojia za kilimo mwaka mzima.

341. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia, Wizara itaendelea kukarabati miundombinu ya vituo vinne (4) vya uhaulishaji wa teknolojia za kilimo vya MATI Mtwara, Mlingano, Igurusi na Ichenga. Vilevile, itaendelea na ukarabati wa vituo vinne (4) vya Rasilimali za Kilimo vya Kata katika mikoa ya Dodoma, Singida, Tanga na Tabora. Pia, itajenga mabwawa matano (5) katika Vyuo vya Mafunzo ya Wakulima vya MATI – Ilonga, MATI Tumbi, MATI Ukiriguru, MATI Igurusi na MATI Uyole kwa ajili ya kuvuna maji ya mvua kwa lengo la kutoa mafunzo ya kilimo kinachokabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

342. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha huduma za ugani zinasogezwa karibu na wakulima, Wizara itakamilisha ujenzi wa nyumba 55 za Maafisa Ugani katika mikoa 19 nchini. Vilevile, itaendelea na ujenzi na ukarabati wa vituo vitano (5) vya Rasilimali za Kilimo vya Kata (Ward Resource Centres – WARC's) ili kuwezesha wakulima kupata mafunzo na huduma za kilimo katika vituo hivyo.

343. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea na ujenzi wa miundombinu ya Chuo cha Taifa cha Sukari Kidatu ili kuwa kituo mahiri cha tasnia ya sukari katika ukanda wa SADC na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Lengo ni kuzalisha wataalamu mahiri katika tasnia ya sukari ili kuongeza tija na uzalishaji katika tasnia ya sukari nchini.

**Mafunzo ya Kilimo**

344. ***Mheshimiwa Spika,*** ukombozi wa kweli wa mkulima haupatikani kwa kutoa vitendea kazi pekee, bali kwa kupatiwa mafunzo ili kukuza ujuzi na maarifa. Wizara katika mwaka 2026/2027, itaendesha programu za uhaulishaji teknolojia za kilimo ikiwemo kutoa mafunzo ya kanuni za kilimo bora, uendeshaji na usimamizi wa matumizi endelevu ya zana za kilimo, kilimo biashara na teknolojia himilivu kwa wakulima 1,200,000. Vilevile, itagharamia mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi 2,320 wa ngazi ya Astashahada na Stashahada kupitia vituo vya kuhaulisha teknolojia za kilimo kwa ajili ya kuwajengea wanafunzi umahiri kwenye mnyororo wa uzalishaji na usimamizi wa mazao mahsusi.

345. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na kiongozi mahiri Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania itaendelea kutekeleza azma ya kumuinua mkulima kupitia mafunzo ambayo yatatolewa na maafisa ugani. Ili kufikia lengo hilo Wizara itaendelea kutoa mafunzo rejea kwa Maafisa Ugani 1,200 ili kuendana na mahitaji na mabadiliko ya teknolojia ambazo watazifikisha kwa wakulima.

### 5.1.6 Kuanzisha Mashamba Makubwa ya Pamoja na Kupima Afya ya Udongo

346. ***Mheshimiwa Spika***, wengi wetu tunatambua kuwa ardhi ni mali na asili ya utajiri wetu na hatuwezi kuupata utajiri huo kwa kiwango chake kwa kuendeleza uzalishaji katika mashamba madogo. Ni lazima ardhi tuifanye iseme kwa lugha ya mafanikio kupitia mashamba makubwa. katika mwaka 2026/2027, Wizara itakamilisha uchoraji wa ramani za kidijiti zinazoonesha hali ya afya ya udongo nchini na kutoa mapendekezo ya matumizi sahihi ya pembejeo za kilimo katika maeneo yote yanayotumika kwa kilimo katika ngazi za vijiji. Vilevile, Wizara itatambua, itapima na itawezesha umiliki wa mashamba yenye ukubwa wa ekari 80,000 kwa ajili ya uwekezaji wa kilimo biashara kwa mazao ya kimkakati ya chikichi na ngano.

347. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara itanunua na kusambaza *soil scanner* 43 kwa ajili ya kupima afya ya udongo katika Halmashauri 43 ili kuhakikisha matumizi sahihi ya pembejeo za

kilimo kwa wakulima. Aidha, Wizara itaendelea na ujenzi wa ofisi mbili (2) za usimamizi na mipango ya matumizi ya ardhi ya kilimo katika Kanda ya Ziwa (Mwanza) na Mashariki (Morogoro) kwa ajili ya kusogeza huduma karibu na wakulima.

### 5.1.7 Uendelezaji wa Kilimo cha Umwagiliaji

348. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itaendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji katika miradi 118 kama ifuatavyo: -

i. Ujenzi wa skimu 55 za umwagiliaji zenye jumla ya hekta 124,626;
ii. Ujenzi wa mabwawa 23 yenye mita za ujazo 100,629,958;
iii. Ukarabati wa skimu 39 za umwagiliaji zenye jumla ya hekta 106,480; na
iv. Ufungaji wa miundombinu ya umwagiliaji katika shamba la Chinangali awamu ya pili lenye ukubwa wa hekta 620.8.

349. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Tume itaendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa skimu za umwagiliaji 389, mabwawa 49 na mabonde ya kimkakati saba (7) yenye ukubwa takriban hekta 168,796.

350. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itaendelea na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika shamba la Bugwema lenye jumla ya hekta 3,000. Vilevile, Tume itaanza ujenzi wa mabwawa ya Mbakiamtuli na Ngorongo katika bonde la Rufiji yenye jumla ya mita za ujazo 57,548,653 zitakazomwagilia eneo lenye jumla ya hekta 64,800; na kuanza ujenzi wa skimu katika Bonde la mto Ngono lenye jumla ya hekta 20,470.

351. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kushirikiana na Wizara ya Maji kuhakikisha mradi wa kutumia maji ya Ziwa Victoria na Tanganyika (mradi wa Gridi ya Taifa ya Umwagiliaji) kwa ajili ya umwagiliaji unatekelezwa. Mradi wa Gridi ya Taifa ya umwagiliaji utanufaisha wakulima wa mikoa ya Simiyu, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Kigoma, Mwanza, Geita, Mara, Kagera, Rukwa na Katavi, Wilaya 69, Kata 192 na Vijiji 943.

352. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha uendelevu wa miradi ya umwagiliaji, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itaendelea kuimarisha usimamizi wa miundombinu ya umwagiliaji kwa kusajili vyama vya umwagiliaji 100; kutoa mafunzo ya uendeshaji na utunzaji wa miundombinu ya umwagiliaji kwa

wakulima 5,000; itaingia mikataba na vyama vya umwagiliaji 500 kuhusu uendeshaji, usimamizi na matunzo ya miundombinu; na kutoa mafunzo ya ukusanyaji wa ada ya huduma za umwagiliaji kwa vyama vya umwagiliaji 500.

### 5.1.8 Uanzishaji wa Vituo vya kutoa Huduma na Ununuzi wa Zana za Kilimo

353. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara itaanzisha vituo 100 vya kutoa huduma ya zana za kilimo kati ya vituo 1,000 vinavyotarajiwa kuanzishwa ifikapo mwaka 2030. Aidha, Wizara itanunua trekta 500, *power tiller* 200 na mashine 50 za kuvuna na kukausha nafaka kwa ajili ya shughuli za kilimo. Vilevile, itaanzisha Kituo cha Zana za Kilimo cha Taifa (National Mechanization Centre) ambacho kitakuwa na zana zote za msingi kwa ajili ya kusafisha na kusawazisha mashamba, uchimbaji wa visima na mabwawa na kutoa mafunzo.

### Uzalishaji wa Mazao kwa Mwaka 2026/2027

354. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara itaendelea kusimamia na kutekeleza mikakati ya uzalishaji wa mazao ya kilimo kulingana na mahitaji ili kuongeza tija katika uzalishaji. Mazao hayo yanahusisha Mazao Asilia ya Biashara, Mazao ya Bustani,

Mazao ya Chakula, Mazao ya Mafuta na mazao yenye mahitaji makubwa yanayoagizwa nje ya nchi.

**Mazao Asilia ya Biashara**

355. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kuhamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa mazao asilia ya biashara ikiwemo pamba, kahawa, mkonge, korosho, tumbaku, pareto, kakao na chai kutoka jumla ya tani 1,599,945.66 mwaka 2025/2026 hadi tani 2,118,000 mwaka 2026/2027 kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 6**.

**Jedwali Na. 6: Malengo ya Uzalishaji wa Mazao Asilia ya Biashara (Tani) katika Mwaka 2026/2027**

| **Na.** | **Mazao** | **2025/2026** | **2026/2027** |
|---|---|---|---|
| | | **Uzalishaji** | **Malengo** |
| 1 | Korosho | 617,683.77 | 750,000 |
| 2 | Pamba | 222,014 | 400,000 |
| 3 | Pareto | 2,780* | 3,000 |
| 4 | Kahawa | 74,663.60 | 85,000 |
| 5 | Tumbaku | 185,776 | 205,000 |
| 6 | Chai | 11,631.48* | 30,000 |
| 7 | Mkonge | 64,321.77* | 80,000 |
| 8 | Sukari | 410,979.04 | 550,000 |
| 9 | Kakao | 10,096* | 15,000 |
| **Jumla** | | **1,599,945.66** | **2,118,000** |

* *Uzalishaji unaendelea*

356. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kufikia malengo hayo, mikakati ya uzalishaji kwa kila zao ni kama ifuatavyo:-

**Zao la Pamba**

357. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Pamba Tanzania itaendelea kuhamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa zao la pamba kutoka tani 222,014 mwaka 2025/2026 hadi tani 400,000 mwaka 2026/2027. Uzalishaji huo utafikiwa kwa kusambaza mbegu bora za pamba tani 18,000, chupa (acrepacks) 10,000,000 navinyunyizi 20,000. Vilevile, Bodi kwa kushirikiana na wadau itazalisha na kusambaza mbolea hai lita 7,200,000 zenye uwezo wa kunyunyuzia hekta 360,000 pamoja na kuimarisha huduma za ushauri wa kitaalamu katika maeneo ya uzalishaji.

358. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Pamba itaandaa mradi maalum wa *Complete Cotton Village* kwa kuhamasisha vyama vya ushirika vinne (4) katika uongezaji thamani wa zao la pamba katika Mkoa wa Simiyu. Vilevile, itanunua na kusimika mtambo wa kuchakata mbegu wenye uwezo wa kuchakata tani 15,000 kwa mwaka ili kupunguza gharama na kuongeza uendelevu wa upatikanaji wa mbegu. Aidha, Bodi itaendelea kutafuta mbia wa kuanzisha kiwanda cha kuchakata na kutengeneza pamba za hospitali na nyuzi kwa ajili ya kufungia tumbaku (cotton twine) katika Mkoa wa Simiyu. Hatua hiyo itasaidia kupunguza matumizi ya fedha za kigeni kutokana na uagizaji wa vifaa tiba vinavyotokana na pamba.

359. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kuratibu ujenzi wa kongani ya pamba (industrial park) kwenye eneo la ekari 1,000 katika Mkoa wa Mwanza. Aidha, itaanzisha mashamba makubwa ya pamoja ya pamba yenye ukubwa wa ekari 20,000 kwa ajili ya vijana na wanawake katika mikoa ya Simiyu, Singida na Kigoma. Vilevile, itaendelea kuboresha vituo vya mafunzo ya wakulima katika mikoa ya Simiyu - Nyakabindi na Tabora - Igunga ili kuviwezesha kutoa huduma za zana za kilimo.

360. ***Mheshimiwa Spika,*** Aidha, itanunua na kusimika mitambo miwili (2) ya kuzalisha nishati ya kupikia inayotokana na masalia ya mashina ya pamba na mitambo nane (8) ya kusokota nyuzi za pamba na kuzalisha vikoi na mitandio. Pia, Bodi kwa kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika itaendelea kuratibu ufufuaji wa *Ginnery* mbili (2) zilizopo Mhunze na Uzogole.

**Zao la Chai**

361. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha tasnia ya chai nchini, Wizara kupitia Bodi ya Chai Tanzania itahamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa chai kavu kutoka tani 11,631.48 mwaka 2025/2026 hadi tani 30,000 mwaka 2026/2027. Vilevile, katika kuimarisha masoko na uongezaji thamani wa zao la chai, Bodi kwa kushirikiana na wadau wa sekta

binafsi itaratibu uanzishwaji wa viwanda vitatu (3) vya kuchakata na kuchanganya chai. Aidha, Bodi itatoa mafunzo kuhusu matumizi ya mifumo ya kilimo mtandao kwa wakulima 15,000 wa zao la chai katika mikoa ya Iringa, Mbeya na Njombe.

362. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi ya Chai itaendelea kuratibu uendeshaji wa mnada wa chai wa Dar es Salaam na kuwezesha mnada huo kufanyika kwa njia ya mtandao ili kupata masoko mapya ya kimataifa na kuimarisha bei ya chai kavu. Vilevile, itawezesha utekelezaji na usimamizi wa viwango endelevu vya hiari (Voluntary Sustainability Standards – VSS) na uthibitishaji wa mazingira, jamii na utawala bora (Enviromental Social and Governance – ESG) ikiwemo ajira zenye staha na hifadhi za bioanuai katika mashamba ya chai kwa wakulima wa chai 4,040 wa Mufindi na Lupembe.

**Zao la Kahawa**

363. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara kupitia Bodi ya Kahawa Tanzania itahamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa zao la kahawa kutoka tani 74,663.60 mwaka 2025/2026 hadi tani 85,000. Vilevile, itatoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha zao la kahawa na mbinu za kukabiliana na mabadiliko ya

tabianchi kwa wakulima 2,300 na Maafisa Ugani 217 kwenye maeneo ya uzalishaji. Pia, itaweka mfumo wa kusimamia uandaaji, usambazaji na utunzaji wa miche inayozalishwa.

364. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza uzalishaji wa zao la kahawa, Bodi ya Kahawa kwa kushirikiana na TARI itazalisha na kusambaza miche ya kahawa 30,000,000. Vilevile, itawezesha uanzishaji wa mashamba mapya ya kahawa yenye ukubwa wa hekta 4,000 katika Halmashauri 54 zinazozalisha kahawa.

365. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi itanunua na kusimika mashine nne (4) za kumenya kahawa kwa ajili ya vyama vya ushirika vilivyopo katika wilaya za Mbinga na Mbozi kwa lengo la kuongeza thamani ya zao la kahawa. Kadhalika, itachimba visima 10 katika mashamba makubwa ya kahawa (block farm) katika maeneo ya uzalishaji ili kuwezesha wakulima kupata maji ya uhakika kwa ajili ya umwagiliaji.

**Zao la Korosho**

366. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027 Wizara kupitia Bodi ya Korosho Tanzania, itahamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa korosho kutoka tani 617,683.77 mwaka 2025/2026 hadi tani 750,000. Lengo hilo litafikiwa kwa kuendelea kutoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha zao la korosho kwa

wakulima 2,000 katika maeneo ya uzalishaji. Vilevile, Bodi itanunua na kusambaza viuatilifu vya *Sulphur* ya unga tani 30,000 na viuatilifu vya maji lita 1,500,000 kwa ajili ya udhibiti wa visumbufu vya zao la korosho.

367. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi ya Korosho, itaanzisha mashamba ya pamoja ya korosho yenye ukubwa wa hekta 3,520 katika mikoa ya Pwani (2,600), Singida (120), Lindi (200), Katavi (200) na Mbeya (400). Kadhalika, itaendelea na ujenzi wa miundombinu ikiwemo, kuchimba visima - 5, kujenga zahanati - 1, jengo la utawala - 1, nyumba - 5 na ghala - 1 katika kongani la viwanda la Maranje.

368. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha upatikanaji wa miche ya korosho, Bodi kwa kushirikiana na TARI na sekta binafsi itazalisha na kusambaza miche ya korosho 5,000,000. Vilevile, itawatambua na kuwasajili wazalishaji 3,000 wa miche ya korosho na kuendelea kuhuisha kanzidata ya wakulima wa korosho.

369. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhamasisha uwekezaji na upatikanaji wa masoko ya zao la korosho, Bodi itanunua vifaa na mashine za viwandani katika kongani la viwanda la Maranje. Vilevile, itaendelea na ujenzi wa viwanda vitatu (3) vya kubangua korosho vyenye uwezo wa kubangua tani 230,000 kwa mwaka vitavyojengwa kupitia wawekezaji wa Kampuni ya Mateak Holding LTD (tani

100,000), Dorado Cashew Ltd. (tani 100,000) na Korosho Investment (tani 30,000) .

370. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi itaendelea na ujenzi wa ghala nne (4) zenye uwezo wa kuhifadhi tani 38,000 katika Halmashauri za Mkinga (tani 10,000), Tunduru (tani 10,000), Mkuranga (tani 10,000) na Mtwara (tani 8,000). Vilevile, itahamasisha Vyama Vikuu vya Ushirika vya TANECU, MAMCU na CORECU kuendelea na ujenzi wa ghala tatu (3) zenye uwezo wa kuhifadhi jumla ya tani 15,000 za korosho kwa lengo la kuongeza thamani ya zao la korosho.

**Zao la Mkonge**

371. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Mkonge Tanzania itahamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa zao la mkonge kutoka tani 64,321.77 mwaka 2025/2026 hadi tani 80,000 mwaka 2026/2027. Vilevile, itasambaza miche ya mkonge 3,500,000 kwa wakulima. Aidha, Bodi kwa kushirikiana na TARI itatoa mafunzo kuhusu uzalishaji wa mkonge na uongezaji thamani wa zao hilo kwa wadau 200 na Maafisa Ugani 50.

372. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhamasisha uongezaji thamani wa zao la mkonge, Bodi itaendelea na ununuzi na usimikaji wa mashine 10 za kuchakata mkonge (dikotiketa) zenye uwezo wa kuchakata tani mbili (2) kwa siku katika

mikoa ya Tanga (6), Morogoro (2), Shinyanga (1) na Tabora (1). Aidha, itakamilisha ujenzi wa vituo viwili (2) vya kuchakata zao la mkonge katika Wilaya ya Mkinga na Handeni.

373. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi ya Mkonge itaanzisha vituo 13 vya ukusanyaji na uuzaji wa mkonge kwa ajili ya wakulima wadogo na kuweka miundombinu ya uongezaji thamani *(brushing & baling)* katika mikoa ya Singida, Pwani na Tanga ili kuimarisha upatikanaji wa masoko ya zao la mkonge.

374. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi itakamilisha ujenzi wa ghala, ofisi na miundombinu ya maji taka katika viwanda vya Taula na Kibaranga vilivyopo katika Halmashauri za Wilaya za Handeni na Muheza. Pia, itakamilisha malipo ya mashine saba (7) za kuchakata mkonge zinazomilikiwa na Kampuni ya Sisalana katika mashamba matano (5) ya Hale (1), Magoma (2), Magunga (1), Ngombezi (1) na Mwelya (2).

**Zao la Tumbaku**

375. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Tumbaku Tanzania itaendelea kuhamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa zao la tumbaku kutoka tani 185,776 mwaka 2025/2026 hadi tani 200,000 mwaka 2026/ 2027 kulingana na mikataba kati ya wakulima na makampuni ya tumbaku. Vilevile,

itahamasisha na kutoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha zao la tumbaku kwa wakulima 8,000 na Maafisa Ugani 250 kutoka kwenye kampuni za tumbaku, Vyama vya Ushirika na Halmashauri za Wilaya katika maeneo ya uzalishaji. Aidha, itaanzisha shamba darasa moja (1) lenye ukubwa hekta 40 katika Halmashauri ya Chunya, Mkoa wa Mbeya.

376. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi itakamilisha ujenzi wa ofisi katika Halmashauri za Kaliua na Manispaa ya Songea na kununua magari mawili (2) kwa ajili ya kuratibu na kuwezesha utekelezaji wa shughuli za Bodi. Aidha, itajenga Ofisi mbili (2) za Kanda katika mikoa ya Tabora (Sikonge) na Kigoma (Kasulu) na kununua vifaa vya ofisi. Kukamilika kwa shughuli hizo, kutawezesha Bodi kuimarisha utekelezaji wa majukumu yake.

377. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza thamani ya zao la tumbaku, Bodi kwa kushirikiana na wadau itasimamia ujenzi wa mabani 750 ya tumbaku kwa ajili ya kukaushia tumbaku katika mikoa ya Tabora, Shinyanga, Katavi, Kigoma, Mbeya, Songwe, Geita, Kagera, Singida, Ruvuma na Iringa. Vilevile, itanunua na kusimika makaushio matatu (3) ya tumbaku (Curing hubs) yanayotumia nishati ya jua na itajenga ghala moja (1) la kuhifadhia tumbaku katika Mkoa wa Morogoro.

378. ***Mheshimiwa Spika,*** Pia, Bodi kwa kushirikiana na wadau itaendeleza jitihada za kuhamasisha upandaji wa miti kwa kila mkulima, matumizi ya matawi ya miti badala ya magogo pamoja na nishati mbadala ya kukaushia tumbaku ikiwemo majani tembo na makaa ya mawe ili kupunguza ukataji wa miti na kuendeleza jitihada za uhifadhi wa mazingira.

379. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi kwa kushirikiana na *Tumbaku Cooperative Joint Enterprise* (TCJE) itaratibu ununuzi na usambazaji wa viuatilifu aina ya *Flumetralin* lita 142,857.14 *Imidacloprid* (30g/pkt) pakiti 1,142,857.14 na *Deltamethrin* (20ml/chupa) chupa 1,714,285.71 kwa ajili ya kudhibiti visumbufu vya zao la tumbaku.

**Zao la Pareto**

380. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA), itaendelea kuhamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa zao la pareto kutoka tani 2,780 mwaka 2025/2026 hadi tani 3,000 mwaka 2026/2027. Vilevile, itatoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha zao la pareto kwa wakulima viongozi 450 na wakaguzi wa pareto 50 kupitia mashamba darasa 100 yatakayoanzishwa katika maeneo

ya uzalishaji kwa kushirikiana na wadau wa zao la pareto.

381. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha ubora wa pareto inayozalishwa nchini inakidhi viwango vya kimataifa, Wizara kupitia COPRA itaendelea na ujenzi wa makaushio 150 ya maua ya pareto katika Halmashauri za Makete (30), Ileje (35), Mbeya Vijijini (40), Ludewa (10), Mbulu (25) na Arusha Vijijini (10). Vilevile, itaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika uongezaji thamani ya zao la pareto ili kuongeza mauzo nje ya nchi. Kadhalika, COPRA itasajili wakulima 20,000 wa zao la pareto kwa kuchukua taarifa zao na majira ya nukta ya mashamba yao kwa lengo la kuwatambua na kuwapa huduma stahiki.

382. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha upatikanaji wa mbegu za pareto kwa wakati kwa wakulima, COPRA na TARI kwa kushirikiana na wadau itazalisha na kusambaza mbegu za pareto tani tano (5) katika maeneo ya uzalishaji.

**Zao la Kakao**

383. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara kupitia COPRA itahamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa kakao kutoka tani 10,096 mwaka 2025/2026 hadi tani 15,000. Uzalishaji huo utafikiwa kwa

kutoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha zao la kakao kwa wakulima viongozi 500 na Maafisa Ugani 45 katika Halmashauri za Kyela, Rungwe, Busokelo, Mlimba na Mvomero. Vilevile, COPRA kwa kushirikiana na TARI itazalisha na kusambaza miche 559,500 ya kakao kwa wakulima katika mikoa ya Tanga, Kigoma, Kagera na Morogoro.

384. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha uongezaji thamani na kuhakikisha kakao inafikia viwango vya soko la kimataifa, COPRA itaendelea na ujenzi wa miundombinu ya usindikaji na ukaushaji katika vituo saba (7) vya ukusanyaji wa kakao vya Mlimba (1), Kyela (4), Mvomero (1) na Muheza (1) kwa ajili ya uongezaji thamani wa zao la kakao. Tume ya Maendeleo ya Ushirika itahamasisha chama kikuu cha KYECU kuanzisha kiwanda cha kusindika kakao.

**Mazao ya Bustani**

385. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara kupitia COPRA na kwa kushirikiana na wadau itaendelea kuhamasisha na kusimamia utekelezaji wa mikakati ya kuendeleza mazao ya bustani itakayowezesha kuongeza uzalishaji wa mazao hayo kutoka tani 9,781,236.74 mwaka 2024/2025 hadi tani 10,000,000. Uzalishaji huo utafikiwa kwa kutoa mafunzo rejea kuhusu kilimo bora cha mazao ya

bustani kwa Maafisa Ugani 1,500 na wakulima 4,000 katika maeneo ya uzalishaji.

386. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara itaendelea na ujenzi wa vituo jumuishi viwili (2) vya kuchambua, kufungasha na kuhifadhi mazao ya bustani katika Halmashauri za Mufindi (Iringa) na Rungwe (Mbeya) ili kuongeza thamani na kukidhi viwango vya soko la ndani na nje ya nchi.

387. ***Mheshimiwa Spika,*** mazao ya bustani yameendelea kuwa sehemu muhimu katika kuchochea ajira kwa vijana na wanawake, kuongeza kipato kwa mkulima na kukuza uchumi wa nchi. Serikali inaendelea kuweka mikakati madhubuti ili kuendeleza mazao hayo yakiwemo:-

**Zao la Parachichi**

388. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na fursa kubwa iliyopo ya soko la parachichi ndani na nje ya nchi, Wizara katika mwaka 2026/2027 itahamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa zao la parachichi kutoka tani 201,354 mwaka 2024/2025 hadi tani 235,000. Kati ya hizo, parachichi zinazouzwa nje ya nchi zinatarajiwa kufikia tani 40,000. Uzalishaji huo utafikiwa kwa Wizara kutoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha zao la parachichi

kwa wakulima 9,500 na Maafisa Ugani 500 katika maeneo ya uzalishaji.

389. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha wakulima wanaongeza mashamba ya parachichi ili kuongeza uzalishaji na kipato, Wizara kupitia TARI na COPRA kwa kushirikiana na wadau itaviwezesha vikundi vya vijana na wanawake kuzalisha na kusambaza miche ya parachichi 1,727,400 kwa mpango wa ruzuku. Hatua hiyo si tu inalenga kuongeza uzalishaji wa parachichi bali ni nia ya dhati ya kuwawezesha vijana kupata ajira zenye staha kupitia kilimo. Aidha, Wizara itaweka mfumo wa kusimamia uandaaji, usambazaji na utunzaji wa miche ya parachichi.

390. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha uongezaji thamani na upatikanaji wa masoko ya zao la parachichi, Wizara kupitia COPRA itaendelea na ujenzi wa vituo 20 vya kukusanyia parachichi katika mikoa ya Mbeya nane (8), Iringa vinne (4), Rukwa kimoja (1), Ruvuma viwili (2) na Njombe vitano (5). Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na wadau itaendelea kuhamasisha uzalishaji wa mafuta ya parachichi katika viwanda vya ndani kwa kuwa hadi sasa kuna viwanda vya kati na vikubwa nane (8) vya kuzalisha mafuta ya parachichi.

**Zao la Viazi Mviringo**

391. ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na umuhimu mkubwa wa zao la viazi mviringo katika kuchangia usalama wa chakula nchini na chanzo kikubwa cha kipato kwa wananchi. Wizara katika mwaka 2026/2027, imepanga kuongeza uzalishaji wa zao la viazi mviringo kutoka tani 2,961,414.82 mwaka 2024/2025 hadi tani 3,000,000. Katika kufikia lengo hilo, Wizara kwa kushirikiana na wadau itatoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora na himilivu cha zao la viazi mviringo kwa wakulima 5,000.

392. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia TARI kwa kushirikiana na wadau itatoa mafunzo kuhusu uzalishaji wa mbegu bora za viazi mviringo kwa wakulima wawezeshaji 500 katika mikoa ya Mbeya, Njombe, Morogoro, Tanga, Arusha, Kilimanjaro na Manyara. Vilevile, Wizara itakamilisha uandaaji wa Mkakati wa Kuendeleza Zao la Viazi Mviringo wenye lengo la kuimarisha uzalishaji wa kibiashara wa zao hilo. Kadhalika, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara itaendelea kutoa elimu kwa wadau wa tasnia ya viazi mviringo kuhusu ufungashaji unaozingatia vipimo kwa mujibu wa sheria zilizopo ili kumlinda mkulima.

393. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha uzalishaji wa mbegu bora za viazi mviringo, Wizara kupitia TARI itajenga vitalu nyumba viwili (2) katika vituo vya utafiti vya Igeri (Njombe) na Uyole (Mbeya) na kukarabati kitalu nyumba kimoja (1) katika kituo cha TARI Tengeru (Arusha).

**Zao la Tufaha (Apples)**

394. ***Mheshimiwa Spika***, kwa muda mrefu nchi yetu imekuwa ikitegemea matunda ya tufaha kutoka nje ya nchi licha ya uwepo wa fursa ya kutosha ya uzalishaji wa zao hilo hususan katika maeneo ya Kanda ya Kaskazini, Kati na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini yanayofaa kwa uzalishaji wa tufaha zinazokidhi viwango vya ubora wa kimataifa. Hadi Machi 2026, takriban tani 1,481.98 za tufaha ziliingizwa kutoka nje ya nchi. Hali hiyo, inaonesha mahitaji ya zao hilo ni makubwa ndani ya nchi.

395. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2026/2027, Wizara imepanga kuhamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa zao hilo ili kukidhi mahitaji. Kilimo hiki, si tu alama ya mabadiliko ya kifikra bali ni chanzo kipya cha kukuza uchumi wa mkulima mmoja mmoja hususan vijana na wanawake, kuliingizia Taifa fedha za kigeni na kupunguza utegemezi wa bidhaa hiyo kutoka nje ya nchi.

396. ***Mheshimiwa Spika,*** katika safari hii ya kipekee, Wizara kupitia TARI na COPRA itazalisha na kusambaza miche 600,000 ya tufaha kwa wakulima katika maeneo ya uzalishaji. Aidha, itatoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha zao la tufaha kwa wakulima 2,400 na Maafisa ugani 50 katika maeneo ya uzalishaji. Vilevile, Wizara kupitia COPRA itasajili wakulima 8,261 wa zao la tufaha kwa lengo la kuwatambua na kurahisisha utoaji wa huduma.

397. ***Mheshimiwa Spika,*** jitihada hizo ni kielelezo cha dhamira ya dhati ya kuhakikisha tunatumia fursa zilizopo kuzalisha tufaha ndani ya nchi yetu.

> ***Nitoe wito kwa vijana, wanawake na wawekezaji kuchangamkia kilimo cha tufaha na fursa zilizopo katika mnyororo wake mzima. Tufaha si tu tunda linalotumika kuonesha upendo pekee, bali ni biashara yenye tija na faida ya muda mrefu na ni urithi tunaoweza kuuacha kwa vizazi vijavyo.***

## Mazao yenye Mahitaji Makubwa

398. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kupunguza matumizi ya fedha za kigeni zinazotumika kuagiza mazao na bidhaa za ngano, sukari na mafuta ya kula kutoka nje ya nchi, Wizara itaendelea kuhamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa mazao hayo kwa kuweka na kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo kununua ardhi yenye ukubwa usiopungua ekari 80,000 kwa ajili ya kuanzisha mashamba makubwa ya pamoja kwa mazao ya ngano, alizeti na chikichi na kuwapatia wakulima wakubwa na wadogo ili kuongeza uzalishaji. Aidha, mikakati kwa kila zao ni kama ifuatavyo:-

## Zao la Ngano

399. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara imepanga kuongeza uzalishaji wa zao la ngano kutoka tani 115,826 mwaka 2024/2025 hadi tani 200,000. Lengo hilo litafikiwa kwa kusambaza mbegu za ngano tani 700 kwa wakulima kupitia mpango wa ruzuku na kuanzisha vituo maalum vya kuzalisha mbegu za ngano katika mashamba makubwa ya pamoja. Vilevile, COPRA itatoa mafunzo ya mbinu za kilimo bora cha ngano kwa wakulima 2,000 na maafisa ugani 100 kwenye mikoa ya uzalishaji.

400. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kupata mbegu zinazostahimili hali ya joto kwa lengo la kuongeza uzalishaji, TARI itaendelea na majaribio ya aina 82 za mbegu mpya za ngano katika mikoa ya Morogoro na Tanga. Pia, TARI itaendelea na tafiti za mbegu za ngano zenye kukidhi sifa ya mahitaji ya soko na tija katika uzalishaji. Vilevile, katika kuhakikisha upatikanaji wa mbegu za ngano, TOSCI itatoa mafunzo ya uzalishaji wa mbegu za kuazimia ubora (QDS) kwa wakulima 500 katika Wilaya za Nkasi, Babati, Hanang, Songwe, Mbinga, Siha na Makete. Kadhalika, Wizara kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika itaendelea kuhamasisha vyama vya ushirika kuanzisha mashamba makubwa ya ngano na viwanda vidogo vya kuchakata ngano.

**Zao la Miwa na Uzalishaji wa Sukari**

401. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara kupitia Bodi ya Sukari Tanzania itaongeza uzalishaji wa zao la miwa kutoka tani 4,351,673.1 zilizozalisha sukari tani 410,979.04 mwaka 2025/2026 hadi tani 5,500,000 za miwa zitakazozalisha sukari tani 550,000. Vilevile, Wizara kupitia TARI itaanzisha shamba la kuzalisha mbegu za miwa lenye ukubwa wa ekari 10 katika Halmashauri ya Kilosa ambalo litakuwa na uwezo wa kuzalisha jumla ya tani 400 za mbegu za miwa. Pia, itazalisha mbegu

za miwa tani 200 kutoka kwenye shamba la ekari 5 la Mvomero.

402. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi kwa kushirikiana na TARI itaanzisha vitalu vya kuzalisha miche ya miwa kwenye eneo lenye ukubwa wa hekta 100 katika bonde la Kilombero kwa ajili ya wakulima wadogo wa miwa.

403. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza uwekezaji katika zao la miwa, Wizara kupitia Bodi ya Sukari itaandaa maeneo kwa ajili ya uwekezaji wa kilimo cha miwa nchini ikihusisha eneo la Bonde la Mto Pangani (Korogwe, Muheza, Handeni na Pangani) lenye hekta 146,704.6 na kwenye sehemu ya Bonde la Wembere (Tabora) lenye hekta 15,218 lililopo katika Wilaya za Uyui na Igunga kwa ajili ya uzalishaji wa sukari.

404. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara itaendelea kuratibu uanzishaji wa viwanda viwili (2) vya sukari katika mikoa ya Pwani na Kigoma. Kadhalika, itaratibu uwekezaji wa kujenga viwanda vitatu (3) katika Mkoa wa Tanga ambapo kimoja ni kwa ajili ya sukari ya viwandani na viwili (2) ni kwa ajili ya sukari ya kawaida itakayotumika kama malighafi ya kuzalisha sukari ya viwandani.

**Mazao ya Mafuta**

405. ***Mheshimiwa Spika,*** mahitaji ya mafuta ya kula nchini ni takriban tani 731,974 ikilinganishwa na uzalishaji wa tani 305,906 kwa mwaka. Uzalishaji huo ni pungufu kwa tani 426,068 ambapo huilazimu nchi kutumia fedha nyingi za kigeni kuagiza mafuta ya kula nje ya nchi kwa ajili ya kufidia pengo hilo.

406. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kupunguza utegemezi wa mafuta ya kula kutoka nje ya nchi, Wizara katika mwaka 2026/2027, itahamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa mazao ya mafuta kutoka tani 2,248,046.24 mwaka 2024/2025 hadi tani 2,300,000 kwa kutoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha mazao ya mafuta kwa wakulima katika maeneo ya uzalishaji. Vilevile, itaanzisha mashamba makubwa ya pamoja yenye ukubwa wa hekta 48,000 kwa ajili ya zao la chikichi na alizeti katika mikoa ya Kigoma, Morogoro, Singida na Dodoma.

407. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itasambaza mbegu bora za alizeti tani 120 kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku pamoja na kuzalisha na kusambaza miche ya chikichi 2,000,000 kwa wakulima katika maeneo ya uzalishaji. Kadhalika, itaratibu upatikanaji na usambazaji wa mbegu bora za karanga tani 20.1 na mbegu za ufuta tani 100. Wizara itakamilisha na

kuanza utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Mafuta ya Kula (National Edible Oil Strategy), wenye lengo la kuongeza uzalishaji na kujitosheleza kwa mafuta ya kula nchini.

### 5.2 Kuchangia Kuongeza Ajira zenye Staha na Ushiriki wa Vijana na Wanawake kwenye Kilimo

408. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kutekeleza kipaumbele cha kuchangia kuongeza ajira zenye staha kwa vijana na wanawake kufikia 3,000,000 ifikapo mwaka 2030. Ajira hizo zitatokana na utekelezaji wa programu ya BBT katika miradi ya mashamba makubwa katika maeneo walipo vijana na wanawake ngazi ya Halmashauri; kuendelea kuwezesha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji kwa wakulima wadogo (BBT visima); upatikanaji wa mikopo kwa vijana na wanawake (BBT mitaji); na kuongeza thamani ya mazao na kutoa huduma za ugani (BBT Ugani).

#### 5.2.1 Kuwezesha Uendelezaji wa Programu ya BBT Ngazi ya Halmashauri

409. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kutekeleza Programu ya BBT katika Halmashauri 20 zilizotenga maeneo yasiyopungua ukubwa wa ekari 200 katika mikoa ya Dodoma, Singida, Tabora, Njombe, Mbeya, Iringa, Pwani, Mara,

Katavi, Rukwa, Kagera na Geita. Vilevile, Wizara itawajengea uwezo vijana 2,000 watakaochaguliwa na Halmashauri zao kuhusu kilimo biashara kupitia program ya BBT kwenye vyuo na vituo vya mafunzo ya kilimo. Wizara itaanza ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji, barabara na hifadhi ya mazao ya kilimo katika shamba la Mapogolo Wilaya ya Chunya.

410. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji na uhifadhi katika mashamba ya Ndogowe na Chinangali katika Wilaya ya Chamwino. Vilevile, itaendelea kufungua mashamba na kuweka miundombinu muhimu ya uzalishaji katika mashamba 20 ya Halmashauri. Kadhalika, upembuzi yakinifu utafanyika kwa ajili ya kuweka miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba makubwa ya pamoja matano (5) yaliyopo katika mikoa ya Tabora, Singida, Mbeya na Dodoma.

411. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaratibu utekelezaji wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (TAM) katika mashamba matano (5) ya pamoja. Vilevile, itajenga ghala nane (8), chumba cha ubaridi, uzio na kuweka miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya BBT Ndogowe na Chinangali. Pia, wizara imepanga kusafisha ekari 1,800 katika shamba la BBT Ndogowe.

### 5.2.2 Kuwezesha Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji kwa Wakulima Wadogo (BBT Visima)

412. ***Mheshimiwa Spika,*** kilimo cha umwagiliaji ni nguzo muhimu katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Ili kuendeleza kilimo cha umwagiliaji nchini, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji katika mwaka 2026/2027, itachimba visima 846 vya umwagiliaji katika mikoa 25 nchini kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji na kufunga mifumo ya umwagiliaji katika Halmashauri 178 nchini; na itanunua *surface pump* za umwagiliaji 1,000 kwa ajili ya makundi ya wanawake na vijana kutoka kwenye maeneo ya pembezoni mwa Ziwa Victoria na Tanganyika.

### 5.2.3 Kuwezesha Upatikanaji wa Mikopo kwa Vijana na Wanawake (BBT Mitaji)

413. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Mfuko wa Dhamana wa Pembejeo za Kilimo (AGITF) itawezesha upatikanaji wa mikopo yenye riba nafuu ya Shilingi Bilioni 5 kwa vijana na wanawake. Vilevile, itaweka kiasi cha Dola za Marekani Milioni 35 kwenye Benki za biashara kwa ajili ya *guarantee scheme* zitakazowezesha vijana na wanawake kupata

mikopo yenye riba nafuu mara mbili au zaidi ya fedha hizo.

### 5.2.4 Kuwezesha Vijana na Wanawake Kuongeza Thamani ya Mazao

414. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Mkonge itaendelea kutoa mafunzo ya kuongeza thamani ya zao la mkonge kwa vijana na wanawake 200 ili waweze kuzalisha bidhaa zitokanazo na zao hilo; na Bodi ya Korosho Tanzania itanunua mashine 100 za kubangua korosho na kuwapatia vijana na wanawake ili kuongeza thamani ya zao la korosho.

### 5.2.5 Kuwezesha Vijana na Wanawake kutoa Huduma za Ugani (BBT Ugani)

415. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha utoaji wa huduma za ugani na kukuza ujuzi wa vijana wahitimu wa vyuo vya mafunzo ya kilimo kwa kutoa huduma za ugani kwa wakulima, Wizara kupitia Bodi za mazao kwa kushirikiana na Chuo Kikuu Cha Sokoine cha Kilimo na sekta binafsi itaendelea kutekeleza Mpango wa Ugani (BBT – Agricultural Extension Enterpreneurship Scheme) kuzalisha ajira kwa vijana na wanawake 1,700. Vilevile, kupitia Bodi za mazao, vijana na wanawake watahamasishwa kushiriki katika uzalishaji wa miche ya mazao mbalimbali kulingana na mahitaji.

## 5.3 Kuimarisha Usalama wa Chakula na Lishe

416. ***Mheshimiwa Spika,*** usalama wa chakula na lishe nchini ni nguzo muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu katika nyanja za uchumi, kijamii na kisiasa. Katika mwaka 2026/2027, Wizara itaendelea kuwekeza katika miundombinu ya uhifadhi wa chakula, kuiongezea NFRA uwezo wa kununua mazao pamoja na kuhamasisha matumizi ya mazao yaliyoongezewa virutubishi ili kukabiliana na matatizo ya lishe nchini.

### 5.3.1 Uwekezaji kwenye Miundombinu ya Uhifadhi ili Kufikia Uwezo wa Kuhifadhi tani 3,000,000 ifikapo Mwaka 2030

417. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha uwezo wa kuhifadhi, kupunguza upotevu wa mazao ya kilimo baada ya kuvuna na kuimarisha usalama wa chakula, Wizara kupitia NFRA itaendelea na ujenzi wa miundombinu ya uhifadhi yenye uwezo wa kuhifadhi tani 165,000 kupitia Mradi wa Kuongeza Uhifadhi wa Nafaka katika Kanda za Songea, Makambako, Dodoma, Shinyanga na Songwe. Vilevile, itaendelea na ujenzi wa miundombinu yenye uwezo wa kuhifadhi tani 85,000 na kuanza ujenzi wa miundombinu yenye uwezo wa kuhifadhi tani 65,000 katika Kanda za Arusha, Sumbawanga,

Songea, Makambako, Songwe, Kipawa, Shinyanga na Dodoma. Kukamilika kwa miradi hiyo kutaongeza uwezo wa hifadhi na kufanya Taifa kuwa kitovu cha chakula katika Bara la Afrika.

418. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itakarabati ghala 46 katika mikoa ya Shinyanga, Geita, Kigoma, Tabora, Rukwa, Katavi, Mwanza, Manyara na Songwe. Vilevile, itanunua vifaa kwa ajili ya ghala 79 katika mikoa ya Ruvuma, Iringa, Geita, Morogoro, Katavi, Rukwa, Songwe, Manyara, Tabora, Kigoma, Dodoma, Mtwara na Mwanza ili kuongeza uwezo wa hifadhi.

### 5.3.2 Kuiongezea NFRA Uwezo wa Kununua Mazao ya Wakulima ili Kuongeza Hifadhi

419. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha hifadhi ya mazao nchini kwa mwaka 2026/2027, Wizara kupitia NFRA, itaendelea kununua nafaka kutoka kwa wakulima kwa lengo la kuhakikisha usalama wa chakula na upatikanaji wa bei ya uhakika kwa wakulima inaendelea kuimarishwa.

### 5.3.3 Kuhamasisha Matumizi ya Mazao yaliyoongezewa Virutubishi (Biofortified) ili Kukabiliana na Matatizo ya Lishe Nchini

420. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara itaendelea kutekeleza Mpango Kazi wa Lishe katika Kilimo (Nutrition Sensitive Agriculture Action Plan – NSAAP) ili kukabiliana na matatizo ya lishe yanayohusisha udumavu, ukondefu na upungufu wa wekundu wa damu. Vilevile, Wizara kupitia TARI itazalisha na kusambaza vipando vya viazi lishe 3,400,000 kwa lengo la kuhamasisha matumizi katika mikoa ya Mwanza, Geita, Tabora, Katavi, Kigoma, Shinyanga, Simiyu, Kagera na Mara.

421. ***Mheshimiwa Spika,*** TARI itatoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora kwa wakulima wawezeshaji 2,518 na wazalishaji wa mbegu za viazi lishe 100 katika Halmashauri za Bukombe, Geita, Misungwi, Misenyi na Bukoba. Pia, itaandaa fomula ya kutengeneza unga lishe wenye mchanganyiko wa ngano, mahindi ya provitamini A, maharage yenye madini ya chuma na *zinc*. Unga huo utasaidia kuimarisha lishe nchini.

422. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itatoa mafunzo kwa Maafisa Ugani 200 na wakulima viongozi 1,000 katika mikoa ya Njombe, Mbeya na Ruvuma kuhusu ukadiriaji wa mazao ya chakula yakiwemo nafaka, mikunde na mizizi kwa ajili ya hifadhi katika

ngazi ya kaya. Vilevile, itatoa mafunzo kuhusu ujumuishaji na utekelezaji wa mipango ya lishe katika kilimo kwa Maafisa Ugani (250), Maafisa Lishe (12) na Maafisa Mipango (10) katika mikoa ya Lindi na Mtwara. Pia, itatoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora kwa wakulima wawezeshaji 2,518 na wazalishaji wa mbegu 100 katika Halmashauri za Bukombe, Geita, Misungwi, Misenyi na Bukoba.

## 5.4 Kuimarisha Upatikanaji wa Masoko, Mitaji na Uongezaji Thamani

423. ***Mheshimiwa Spika,*** dhamira ya Serikali si tu kuona wakulima wanazalisha mazao ya kutosha, bali ni kuhakikisha kuwa jasho lao linalindwa kupitia mifumo thabiti ya masoko na mitaji kwa kuimarisha mazingira wezeshi na kuweka mifumo itakayowezesha mauzo ya mazao ya kilimo kwa bei ya soko. Hivyo, Serikali ya Awamu ya Sita inajenga daraja kati ya wazalishaji na walaji ambalo litawezesha upatikanaji wa mitaji yenye riba nafuu hususan kwa wakulima wadogo.

424. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara kwa kushirikiana na wadau itaendelea kuimarisha upatikanaji wa masoko, mitaji na uongezaji thamani kwa kutekeleza mikakati ifuatayo:-

### 5.4.1 Kujenga Miundombinu ya Masoko ya Mazao ya Kilimo

425. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha miundombinu ya masoko ya mazao ya kilimo, Wizara itakamilisha ujenzi wa masoko matano (5) ya kimkakati katika Halmashauri za Manispaa ya Kahama (Busoka), Ngara (Kabanga), Kyerwa (Nkwenda na Murongo) na Tarime (Sirari). Ujenzi wa masoko hayo utawezesha kuendeleza biashara ya mazao ya kilimo katika mipaka ya nchi za Uganda, Kenya, Rwanda na Burundi.

426. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imepanga kujenga masoko matano (5) kwenye maeneo ya mipakani na maeneo ya kimkakati katika Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Kanda ya Ziwa na Kanda ya Mashariki ambayo ni malango muhimu ya biashara kati ya Tanzania na nchi za jirani ambapo shughuli nyingi za kiuchumi na kijamii zinafanyika.

427. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea na ujenzi wa vituo vya masoko (market sheds) vya Endashangwet (Karatu), Kibakwe (Mpwapwa), Losirwa (Monduli), Ushirika (Nzega Mji), Mamsera (Rombo), Mula (Hai), Kigoma (Kibondo), Moshi (Himo), Halmashauri ya Wilaya ya Singida (Merya) na Manispaa ya Mpanda (Mpanda hoteli). Ujenzi wa vituo hivyo, utawezesha wakulima kukusanya na kuuza mazao sehemu rasmi zinazotambulika na mamlaka husika.

### 5.4.2 Kuongeza Mauzo ya Mazao ya Kilimo Ndani na Nje ya Nchi

428. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza mauzo ya mazao ya kilimo ndani na nje ya nchi, Wizara katika mwaka 2026/2027, itaendelea kushirikiana na sekta binafsi kuimarisha biashara ya mazao ya kilimo kwa kusimamia mikakati ya uzalishaji na kuongeza mauzo ya mazao nje ya nchi kutoka Dola za Marekani Bilioni 3.54 mwaka 2023/2024 hadi takriban Dola za Marekani Bilioni 4 mwaka 2026/2027. Vilevile, Wizara itakamilisha taratibu za ufunguzi wa masoko mapya 15 katika nchi 14 kwa ajili ya mazao ya nafaka, bustani, mikunde na tumbaku.

429. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itatoa elimu ya stakabadhi za shala na minada ya kidijiti kwa wakulima 3,200 ili kuimarisha biashara ya mazao ya kilimo. Vilevile, Wizara itaongeza mazao ya mahindi, njugumawe, kunde, pilipili manga, karafuu, iliki, vitunguu na mdalasini katika mifumo rasmi ya biashara kupitia Mfumo wa Stakabadhi ya Ghala, mfumo wa vituo rasmi vya mauzo na mfumo wa kilimo cha mkataba.

### 5.4.3 Kuimarisha Uongezaji Thamani kwa Kushirikisha Sekta Binafsi

430. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara itaendelea na ujenzi wa vituo jumuishi viwili (2) katika mikoa ya Iringa (Mufindi) na Mbeya (Rungwe) ili kuwezesha kuchambua, kuhifadhi na kuchakata mazao ya bustani. Vilevile, itaendelea na ujenzi wa miundombinu ya kukaushia, kuchakata na kuhifadhi muhogo katika Halmashauri za Kakonko na Kibondo na tangawizi katika Halmashauri ya Buhigwe.

431. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea na ujenzi wa vituo 20 vya ukusanyaji wa parachichi na mazao mengine ya bustani pamoja na kuweka miundombinu stahiki ili kuimarisha shughuli za ukusanyaji, uhifadhi na upatikanaji wa masoko ya mazao hayo katika mikoa ya Mbeya, Njombe, Iringa, Rukwa, Ruvuma, Tanga, Kilimanjaro, Kagera, Kigoma na Songwe.

432. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TARI itatafiti teknolojia tatu (3) za usindikaji na uongezaji thamani wa zao la korosho, mahindi na ufuta na utengenezaji wa ethanoli. Vilevile, itaendelea na utafiti wa aina 13 za teknolojia za kuongeza thamani ya mazao ya nyanya, muhogo, mtama, choroko, ulezi, uwele, viazi lishe, soya, kunde, mbaazi, migomba, zabibu

na matunda ya asili. Aidha, COPRA itanunua mashine 100 za kusafisha, kuchambua na kupanga madaraja ya mazao ya jamii ya mikunde na nafaka. Mashine hizo zitakabidhiwa kwa AMCOS kwa ruzuku katika mikoa ya Rukwa, Katavi na Songwe.

### 5.4.4 Kuimarisha Upatikanaji wa Mitaji

433. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2026/2027, itaendelea kushirikiana na taasisi za fedha katika kuimarisha utoaji wa mikopo yenye riba nafuu kwenye sekta ya kilimo. Vilevile, TADB itashirikiana na taasisi za fedha 22 zinazotumia mfuko wa dhamana wa TADB ili kurahisisha utoaji wa mikopo yenye riba nafuu katika shughuli za kilimo yenye thamani ya Shilingi Bilioni 330.

434. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia AGITF itatoa mikopo yenye thamani ya Shilingi 21,470,000,000 kupitia dhamana ya mikopo, mkulima nafuu *loan*, mkulima *loan* na *wholesale lending*. Kadhalika, itaendelea na ujenzi wa ofisi ya AGITF Makao Makuu katika Mkoa wa Dodoma.

### 5.4.5 Kuziwezesha Maabara za Kilimo Kufikia Viwango vya Ubora Vinavyotakiwa Kimataifa

435. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TPHPA itaanza ujenzi wa maabara ya kisasa katika Mkoa wa Njombe kwa ajili ya kupima ubora wa mazao ili kusogeza huduma karibu na wadau wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na mikoa ya jirani. Vilevile, TOSCI itakamilisha ukarabati wa maabara ya Makao Makuu katika Mkoa wa Morogoro na maabara ya kupima ubora wa mbegu iliyopo katika Mkoa wa Arusha. Pia, itajenga na kukarabati vyumba vya ubaridi katika maabara ya mbegu iliyopo Mkoa wa Mbeya na Arusha.

436. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itakamilisha ujenzi na ununuzi wa vifaa vya maabara ya magonjwa ya mimea (Patholojia) katika kituo cha TARI Naliendele na maabara ya kuzalisha miche kwa njia ya chupa katika kituo cha TARI Maruku. Vilevile, Wizara itaimarisha maabara za kuzalisha miche kwa njia ya chupa kwa kununua vifaa vya maabara katika vituo vya TARI Tengeru, TARI Mikocheni na TARI Mlingano. Pia, itakamilisha upatikanaji wa ithibati ya maabara ya udongo katika kituo cha TARI Mlingano.

### 5.5 Kuimarisha Maendeleo ya Ushirika

437. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Sita inatambua kuwa nguvu ya wakulima ipo katika uzalishaji, usindikaji, mitaji na masoko kupitia AMCOS na SACCOS. Hivyo, kuimarisha maendeleo ya ushirika si bahati mbaya bali ni kipaumbele chetu cha msingi katika kuwawezesha wakulima kuwa na sauti moja yenye maamuzi sokoni.

438. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na umuhimu huo katika mwaka 2026/2027, Wizara kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika itaimarisha ukaguzi na usimamizi wa uendeshaji wa vyama vya ushirika; itahamasisha ushirika kwenye sekta mbalimbali na makundi maalum; na kuhamasisha vyama vya ushirika kujiendesha kibiashara. Ili kufikia malengo hayo, Wizara kupitia Tume itatekeleza yafuatayo:-

#### 5.5.1 Kuimarisha Ukaguzi na Usimamizi wa Uendeshaji wa Vyama vya Ushirika

439. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha utendaji kazi wa vyama vya ushirika, Wizara kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) kwa mwaka 2026/2027, itafanya ukaguzi wa mara kwa mara katika vyama vya ushirika 6,545 na COASCO itafanya ukaguzi wa vitabu vya hesabu vya vyama vya ushirika 6,545 vilivyosajiliwa katika mfumo wa MUVU. Aidha, Tume itatoa mafunzo

kuhusu usimamizi wa vyama vya ushirika kwa Maafisa Ushirika 80. Vilevile, Tume itawapatia vitendea kazi Maafisa Ushirika 60 ikiwemo Kompyuta (60) na Pikipiki (60) kwa ajili ya kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Kadhalika, Tume itatoa mafunzo kuhusu utunzaji wa kumbukumbu na uandaaji wa vitabu vya hesabu kwa vyama vya ushirika 6,545 kwa lengo la kuwawezesha kuzingatia Sheria na taratibu katika uendeshaji.

440. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume itatathmini na kuvipanga vyama vya ushirika wa mazao 4,894 katika madaraja kulingana na umiliki wa mali za kudumu na utendaji ili kubaini aina ya usimamizi unaotakiwa katika chama husika. Vilevile, itaendesha kampeni ya **Linda Ushirika Chagua Uadilifu** kwa ajili ya kuelimisha wadau wakiwemo vyama vya ushirika, mahakama, polisi, TAKUKURU na wanasheria kuhusu ushirika, uadilifu na utatuzi wa migogoro.

### 5.5.2 Kuhamasisha Vyama vya Ushirika Kujiendesha Kibiashara na Kuviwezesha Kupata Mitaji

441. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume kupitia *Ushirika Joint Enterprise (UJE)* kwa kushirikiana na Benki ya Ushirika Tanzania itaendelea kuhamasisha vyama vya ushirika kuendelea kununua hisa katika Benki ya Ushirika kutoka asilimia 45 hadi 51. Vilevile, itahamasisha

vyama vikuu vya ushirika 25 kuwa mawakala wa Benki na kufungua matawi katika mikoa ya Kagera, Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya, Katavi na Ruvuma.

442. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza thamani ya zao la korosho Tume itaendelea kuratibu ujenzi wa kiwanda cha kubangua korosho chenye uwezo wa kubangua tani 3,500 kwa mwaka katika Wilaya ya Tandahimba ambacho kitajengwa na Chama Kikuu cha Tandahimba na Newala (TANECU). Vilevile, Tume itaendelea kuratibu ufufuaji wa kiwanda cha kuchakata pamba cha Magu kinachomilikiwa na Chama Kikuu cha Ushirika NYANZA.

443. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume itaendelea kuratibu ujenzi wa kiwanda cha kukamua mafuta ya kula na kusimika mitambo ya kukamua mafuta kinachomilikiwa na Chama Kikuu cha Ushirika cha Kahama (KACU) ili kuongeza thamani na kukidhi mahitaji ya soko.

444. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Tume itaendelea kuratibu ukarabati na ufufuaji wa kiwanda cha kuchakata pamba kinachomilikiwa na Chama Kikuu cha Pamba Mara. Vilevile, itaratibu ukarabati wa kiwanda cha maziwa kinachomilikiwa na Chama cha Ushirika CHAWAKIM katika Mkoa wa Pwani. Pia, itaendelea kuratibu Chama Kikuu cha

Tabora (WETCU) kujenga kiwanda cha kutengeneza nyuzi za kusukia tumbaku katika kongani ya viwanda vya pamba itakayojengwa katika Mkoa wa Simiyu.

445. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume kwa kushirikiana na wadau itaendelea kuhamasisha vyama vya ushirika kuuza mazao kupitia mifumo rasmi na jumuishi ya biashara na masoko ya mazao. Lengo ni kuongeza ushindani, uwazi na mauzo ya mazao ndani na nje ya nchi.

### 5.5.3 Kuhamasisha Ushirika kwenye Sekta mbalimbali na Makundi Maalum

446. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume itahamasisha uanzishaji wa vyama vya ushirika 26 vya vijana katika ngazi za mikoa ili kuwezesha kupata fursa mbalimbali za kiuchumi ikiwemo kupata mitaji ili viweze kujiendesha. Pia, itahamasisha vikundi 127 vya wafugaji na wavuvi ili kuanzisha ushirika wa wafugaji na wavuvi kwa ajili ya kuwezesha udhibiti wa malisho na kuongeza masoko ya mazao ya mifugo na uvuvi.

447. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Tume itafanya uhamasishaji kwa wakulima wa mazao ya chikichi, viazi mviringo ngano na tufaha ili waweze kujiunga na ushirika. Aidha, Tume, itawezesha uchakataji wa zao la chikichi kwa kutoa mashine 18 za kuongeza thamani ya zao hilo kwenye vyama 18 vilivyoanzishwa.

448. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume itaratibu maandalizi ya Kongamano la Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo Barani Africa (SACCA CONGRESS) litakalofanyika Oktoba, 2026 kwa mara ya kwanza nchini Tanzania. Vilevile, Tume itahamasisha vyama vya ushirika kutumia Kampuni ya Bima ya Ushirika inayomilikiwa na wanaushirika. Lengo ni kutoa huduma za bima zitakazowakinga na vihatarishi vya aina mbalimbali ikiwemo kushuka kwa bei za mazao, majanga yanayotokana na mabadiliko ya tabia nchi na magonjwa ya mazao na binadamu. Pia, Tume itaendelea kuhamasisha uanzishwaji wa SACCOS kwenye AMCOS zinazosimamiwa na vyama vikuu ili kurahisisha upatikanaji wa mikopo kwa wanachama.

### 5.6 Kuimarisha Matumizi ya Mifumo ya TEHAMA katika Uendelezaji wa Sekta ya Kilimo

449. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara itaendelea kuimarisha mifumo ya TEHAMA itakayowezesha wadau wa mnyororo wa kilimo kubadilishana taarifa zinazohusiana na kilimo. Hatua hii si tu itaongeza tija, bali italeta ufanisi na kuhakikisha wakulima wanapata huduma kwa wakati na kukuza uchumi. Ili kufanikisha azma hiyo, Wizara itatekeleza mikakati ifuatayo:-

### 5.6.1 Kuimarisha Mifumo ya Kidijiti itakayowezesha Upatikanaji wa Taarifa Sahihi kwa Wakati

450. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara itaendelea na ujenzi wa moduli ya taarifa za kilimo za kijiografia zitakazopatikana kwa kutumia ramani kwa lengo la kuwezesha upatikanaji wa taarifa kwa wakati. Vilevile, itaendeleza mawasiliano na kubadilishana taarifa za wadau wa mnyororo wa thamani wa takwimu za kilimo za kidijiti (*Agriculture data exchange and digitalization in value chain*).

451. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TPHPA itaendelea kufuatilia mazao (*crop traceability system*) yanayosafirishwa nje ya nchi ili kulinda soko la mazao ya kilimo. Vilevile, Wizara kupitia COPRA itasajili ghala 10,000 za kuhifadhia nafaka na mazao mchanganyiko na kufanya ufuatiliaji wa mazao (stock monitoring) katika mikoa ya Ruvuma, Mbeya, Katavi, Rukwa, Morogoro na Songwe. Aidha, Wizara itaendelea kutumia mifumo ya kidijiti kutoa huduma za ugani kwa wakulima ili kupanua wigo wa utoaji wa huduma hizo. Pia, Wizara itaendelea kuboresha huduma za ugani kwa kutumia teknolojia ya akili unde ambayo itasaidia kuboresha mawasiliano kati ya wakulima, wadau wa kilimo na Wizara.

### 5.6.2 Kuwekeza kwenye Matumizi ya Mifumo ya Kidijiti katika Sekta ya Kilimo

452. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TPHPA, itaendelea kujenga moduli ya afya ya mimea kwa ajili ya kukusanya na kutunza taarifa, kutoa vibali vya uingizaji na usafirishaji wa mazao na mimea nje ya nchi na vibali vya matumizi ya viuatilifu vya mimea na mazao. Vilevile, Wizara itaendelea kuboresha moduli ya mnyororo wa thamani wa mbegu kwa ajili ya upatikanaji wa taarifa zikiwemo za uchakataji, ukusanyaji, utunzaji na usambazaji wa mbegu bora.

453. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea na taratibu za kuanzisha kituo cha teknolojia za kilimo cha TEHAMA (AgriTech Hub) kilichopo katika Mkoa wa Dodoma (Mtanana) ili kusaidia wakulima ikiwemo vijana kujifunza na kufanya ubunifu wa kutumia teknolojia za kidijiti. Pia, Wizara kupitia AGITF itaboresha mfumo wa kieletroniki kwa ajili ya usimamizi wa mikopo ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa mikopo.

454. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha na kurahisisha huduma kwa wananchi kupitia Mifumo ya Kidijiti, Wizara kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika, imepanga kusimamia matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika vyama vya ushirika 290. Aidha, imepanga kujenga Mfumo wa Akili Unde (AI) na Taarifa ya Huduma ya Ziada

Isiyoundwa - *Unstructured Supplementary Service Data* (USSD) kwa ajili ya kurahisisha matumizi ya Mifumo na kupata taarifa katika sekta ya ushirika. Vilevile, itajenga mfumo wa kurahisisha taratibu za ajira na kutoa taarifa za ajira katika vyama vya ushirika sambamba na kuunganisha mifumo 12 ya vyama vya ushirika na Taasisi za Serikali.

**MAENEO MENGINE MUHIMU YATAKAYOTEKELEZWA NA WIZARA**

**Kuimarisha Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira, pamoja na Matumizi ya Mbinu na Teknolojia za Kilimo Himilivu**

455. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, hususan kwa wakulima wa Nyanda Kame, Wizara itaendelea kukijengea uwezo kituo cha TARI - Hombolo kuwa kituo mahiri cha Utafiti wa Mazao ya Ukame na Teknolojia za Uhimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi (Centre for Dryland Crops and Climate Change Research) katika maeneo ya: agronomia, uboreshaji wa mbegu, ulinzi wa mazao, usimamizi wa baada ya mavuno (uchakataji, ongezeko la thamani na matumizi), rasilimali asilia, matumizi ya miumbombinu ya kisasa (automated screenhouse and irrigation) na masuala ya kijamii na kiuchumi.

456. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kuratibu maandalizi na utekelezaji wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (TAM) kwa miradi na mashamba makubwa ya pamoja 20 kwa mujibu wa matakwa ya sheria, kanuni na miongozo ya usimamizi wa mazingira.

457. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imepanga kuendelea kutoa mafunzo kwa wadau 40,000 wa sekta ya kilimo kuhusu mbinu bora za usimamizi wa taka zitokanazo na shughuli za kilimo ikiwa ni njia rafiki ya utunzaji wa mazingira. Vilevile, itatoa mafunzo ya matumizi ya maji kwa ufanisi katika kilimo cha umwagiliaji na matumizi ya nishati mbadala katika shughuli za kilimo.

**Masuala ya Jinsia**

458. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuendelea kuhakikisha masuala ya kijinsia yanazingatiwa katika kilimo, Wizara itakamilisha mwongozo wa ujumuishaji wa masuala ya jinsia katika mnyororo wa thamani wa kilimo na kusambaza kwa wadau mbalimbali kwenye mnyororo wa thamani. Vilevile, Wizara itahakikisha kuwa masuala ya kijinsia yanazingatiwa katika utoaji wa pembejeo za kilimo ikiwemo utoaji wa ruzuku ya mbegu na mbolea pamoja na utoaji wa mafunzo kupitia vikundi vya wakulima katika mashamba darasa ya miradi mbalimbali ya Wizara.

459. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kutoa mafunzo jumuishi ya masuala ya jinsia kwa Maafisa Ugani, Maendeleo ya Jamii, Mazingira na Mipango kutoka katika Halmashauri 26. Pia, Wizara itaendelea kuanzisha madawati ya Jinsia katika taasisi na bodi za mazao zilizopo chini ya Wizara.

**Afya na Ustawi wa Watumishi**

460. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara itaendelea kutoa huduma ya lishe kwa watumishi wanaoishi na VVU watakaojitokeza. Vilevile, Wizara itaendelea kuhamamisha watumishi kushiriki michezo mbalimbali ili kuimarisha afya na kupunguza athari za Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

461. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaratibu vikao vinne (4) vya waelimisha rika kwa lengo la kubadilishana taarifa na kutathmini hali ya utekelezaji wa afua za VVU, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza mahala pa kazi katika Utumishi wa Umma. Vilevile, Wizara itaendelea kutoa elimu ya VVU, UKIMWI, Afya ya Akili na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza.

462. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara itaendelea kutoa elimu ya mapambano dhidi ya rushwa mahali pa kazi na

kuratibu vikao vinne (4) vya masuala ya rushwa na uzingatiaji wa maadili. Vilevile, Wizara itaendelea kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi kwa kuwapatia vitendea kazi, kununua mabasi mawili (2) ya watumishi pamoja na kutoa motisha na stahiki zao kwa mujibu wa Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu za utumishi wa umma. Pia, Wizara itahakikisha watumishi wote wenye sifa wanapatiwa nafasi za kujiendeleza kitaaluma kwa kadri ya mahitaji ya Wizara kwenye maeneo mahsusi.

**Kuwekeza kwenye Ujuzi kwa Wataalam wa Ndani**

463. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara kupitia mpango wake wa kuendeleza mafunzo itawawezesha watumishi 1,059 kupata mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika vyuo vya ndani na nje ya nchi ili kuendana na mahitaji ya taaluma. Kati ya hao, Shahada ya uzamivu (41), Shahada ya uzamili (188), Shahada (40) na Stashahada (3) na mafunzo ya ujuzi maalum (797).

**Wajibu kwa Jamii (Corporate Social Responsibility – CSR)**

464. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha mahusiano na jamii (Corporate Social Responsibility – CSR), Wizara kupitia taasisi zake itatekeleza

miradi itakayolenga kuimarisha uzalishaji wa mazao kwenye maeneo mbalimbali nchini kwa lengo la kuhamasisha na kutoa motisha kwa jamii husika kushiriki katika shughuli za kilimo hususan vijana na wanawake.

**Hitimisho na Shukrani**

465. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhitimisha hotuba yangu mbele ya Bunge lako Tukufu, ninapenda kuwakumbusha Watanzania wote kuwa kilimo ni biashara na mkulima ni mwekezaji. Serikali ya Awamu ya Sita kupitia uongozi mahiri wa Dkt. Samia Suluhu Hassan, umetafsiri dhana hiyo kwa vitendo kwa kuendesha **Kampeni ya Mali Shambani** yenye lengo la kuhakikisha kuwa mkulima wa kitanzania anahama kutoka kilimo cha mazoea na cha kujikimu na kuingia katika kilimo biashara chenye tija, endelevu, uhakika wa soko na manufaa kwa mkulima.

466. ***Mheshimiwa Spika,*** lengo si tu kujitosheleza kwa chakula kwa asilimia 100 bali tunalenga kuwa ghala la chakula kwa ukanda wa EAC, SADC na Afrika kwa ujumla, jambo litakaloongeza fedha za kigeni na kuimarisha thamani ya Shilingi yetu.

467. ***Mheshimiwa Spika,*** malengo hayo hayawezi kufikiwa bila ushirikiano wa karibu na sekta binafsi, hivyo, Wizara inaendelea

kuwakaribisha wawekezaji wa ndani na nje kwenye mnyororo wa kilimo ili kuzalisha ajira na kuwa na bidhaa zenye chapa ya *Made in Tanzania*.

468. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa unyenyekevu mkubwa nitumie nafasi hii ya kipekee kumshukuru tena Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye ameendelea kuweka nguvu kubwa katika kusaidia sekta ya kilimo na wakulima nchini. Aidha, nitumie nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuwa pamoja na wakulima na kuendelea kuhamasisha shughuli za kilimo katika majimbo yao.

469. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba nitumie fursa hii kuzishukuru nchi ambazo zimeendelea kuunga mkono juhudi za Serikali katika kutekeleza shughuli za kilimo nchini. Nchi hizo ni pamoja na:- Serikali za Japan, Marekani, Uingereza, China, Urusi, Indonesia, Korea Kusini, India, Italia, Misri, Kuwait, Israel, Saudi Arabia, Thailand, Iran, Ukraine, Ubelgiji, Ujerumani, Ufini, Norway, Brazil, Uholanzi, Ireland, Malaysia, Denmark, Austria, Ufaransa, Romania, Belarus, Vietnam, Sweden, Canada, Poland, Qatar, Oman, Uturuki pamoja na Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Umoja wa nchi za Afrika, Umoja wa Ulaya, Jumuiya ya Madola na Umoja wa Falme za Kiarabu.

470. ***Mheshimiwa Spika,*** ninayashukuru mashirika mbalimbali ya kitaifa na kimataifa ikiwemo Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, JICA, IMF, IFAD, FAO, WFP, AGRA, KOICA, Care International, World Vision, UNIDO, UNDP, TAHA, World Vegetable Centre, SAT, SUGECO, AGCOT, Aspires Tanzania, CIAT, RIKOLTO, HELVATAS, ENABEL, CAMFED, BIVAC, IRRI, Agriedo, Mazao Hub, Global Community, TASTA, GAIN, NORAD, IITA, AATI, AMDT, SNV, FSDT, ANSAF, MVIWATA, SWISS AID, TOAM, GIZ, UN Women, ESAFF, IFC, ESRF, PASS Trust, Action Aid Tanzania, EAGC, Global Crop Diversity Trust na EFTA.

471. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kuzishukuru taasisi za fedha ikiwemo CRDB, NMB, Benki ya Ushirika Tanzania, TADB, TIB, TCB, Azania Bank, Akiba Commercial Bank, Stanbic, NBC, PBZ, Equity Bank na Mwanga Hakika kwa kuendelea kuwezesha upatikanaji wa mitaji katika shughuli za kilimo.

472. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kuzishukuru taasisi zote za elimu ya juu na taasisi za utafiti. Vilevile, ninapenda kushukuru kampuni na wafanyabiashara wote wa mazao ya kilimo ambao tumekuwa tukishirikiana nao katika kutoa soko la uhakika kwa wakulima. Ninawashukuru pia wafanyabiashara na wasambazaji wa pembejeo za kilimo kwa kuhakikisha pembejeo zinawafikia wakulima kwa wakati.

473. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda pia kuzishukuru kampuni za mawasiliano nchini ikiwemo TTCL, Airtel, Vodacom, Yas na Halotel. Ninawashukuru pia kwa umuhimu wa kipekee wamiliki na wahariri wa vyombo vya habari vyote nchini pamoja na wanahabari wote wa vyombo vyote ikiwemo mitandao ya kijamii kwa kushirikiana nasi katika kuhabarisha umma na kutoa elimu kwa wakulima. Pia, ninawashukuru wasanii wote nchini kwa kuendelea kushirikiana nasi katika kutoa elimu kwa wakulima.

474. ***Mheshimiwa Spika,*** ninawashukuru sana viongozi wa dini kwa kuendelea kutuombea na kutushauri katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

## 6 MAOMBI YA FEDHA MWAKA 2026/2027

## FUNGU 43, 24 na 05

### 6.1 Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli

475. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2026/2027, inatarajia kukusanya Shilingi **28,600,000,000.00** kupitia Fungu 43, Fungu 24 na Fungu 05. Kati ya fedha hizo, Shilingi **25,000,000,000.00** zitakusanywa kutokana na ukaguzi wa mazao, kodi za majengo na uuzaji wa nyaraka za zabuni kupitia Fungu 43 na Shilingi **3,600,000,000.00** zitakusanywa kutokana na ada za huduma ya umwagiliaji na ukodishaji wa mitambo kupitia Fungu 05.

## 6.2 Fedha za Matumizi kwa Mafungu yote

476. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara ya Kilimo inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi **1,105,950,115,000.00** kupitia Fungu 43, Fungu 24 na Fungu 05.

### 6.2.1 Fedha kwa Fungu 43

477. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Shilingi **698,985,584,000.00** kinaombwa. Kati ya fedha hizo, Shilingi **567,345,730,000.00** ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ambapo Shilingi **360,678,811,000.00** ni fedha za ndani na kiasi cha Shilingi **206,666,919,000.00** ni fedha za nje. Aidha, Shilingi **131,639,854,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo Shilingi **84,956,697,000.00** ni mishahara na Shilingi **46,683,157,000.00** ni matumizi mengineyo ya Wizara, Bodi na Taasisi.

### 6.2.2 Fedha kwa Fungu 05

478. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi **384,290,761,000.00**. Kati ya fedha hizo, Shilingi **308,721,961,000.00** ni fedha za maendeleo na Shilingi **75,568,800,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha za maendeleo zinazoombwa, Shilingi

**259,617,801,000.00** ni fedha za ndani na Shilingi **49,104,160,000.00** ni fedha za nje. Aidha, kati ya Shilingi **75,568,800,000.00** ya fedha za matumizi ya kawaida zinazoombwa, Shilingi **65,148,830,000.00** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na Shilingi **10,419,970,000.00** ni kwa ajili ya mishahara.

### 6.2.3 Fedha kwa Fungu 24

479. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Tume ya Maendeleo ya Ushirika inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi **22,673,770,000.00.** Kati ya fedha hizo, Shilingi **21,976,594,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi **697,176,000.00** ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya Fedha za matumizi ya kawaida zinazoombwa, Shilingi **8,130,236,000.00** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na Shilingi **13,846,358,000.00** ni kwa ajili ya mishahara.

480. ***Mheshimiwa Spika,*** NINAOMBA KUTOA HOJA**.**

## VIAMBATISHO

**Kiambatisho Na. 1: Mchanganuo wa Usambazaji wa Mbegu**

| Na. | Aina ya Mbegu | Mkoa | Kiasi kwa Mkoa (Tani) | Halmashauri | Kiasi kwa Wilaya (Tani) | Kiasi (Tani) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Alizeti | GEITA | 93.00 | Nyang'hwale DC | 23.00 | 93.00 |
| | | | | Geita TC | 10.00 | |
| | | | | Geita DC | 18.00 | |
| | | | | Bukombe DC | 15.00 | |
| | | | | Mbogwe DC | 15.00 | |
| | | | | Chato DC | 12.00 | |
| 2. | Ufuta | PWANI | 6.00 | Kibiti DC | 21.00 | 37.93 |
| | | | | Rufiji DC | 2.00 | |
| | | | | Mkuranga DC | 1.30 | |
| | | | | Kisarawe DC | 0.20 | |
| | | | | Chalinze DC | 0.20 | |
| | | | | Bagamoyo DC | 0.10 | |
| | | | | Kibaha DC | 0.10 | |
| | | LINDI | 7.00 | Mtama DC | 0.94 | |
| | | | | Liwale DC | 0.94 | |

| Na. | Aina ya Mbegu | Mkoa | Kiasi kwa Mkoa (Tani) | Halmashauri | Kiasi kwa Wilaya (Tani) | Kiasi (Tani) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Ruangwa DC | 0.81 | |
| | | | | Nachingwea DC | 0.58 | |
| | | | | Kilwa DC | 3.00 | |
| | | | | Lindi MC | 0.73 | |
| | | MTWARA | 6.00 | Nanyumbu DC | 2.32 | |
| | | | | Mtwara MC | 0.12 | |
| | | | | Nanyamba TC | 0.16 | |
| | | | | Tandahimba DC | 0.20 | |
| | | | | Newala TC | 0.13 | |

| Na. | Aina ya Mbegu | Mkoa | Kiasi kwa Mkoa (Tani) | Halmashauri | Kiasi kwa Wilaya (Tani) | Kiasi (Tani) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Newala DC | 0.13 | |
| | | | | Masasi DC | 2.00 | |
| | | | | Mtwara DC | 0.54 | |
| | | | | Masasi TC | 0.40 | |
| | | KATAVI | 2.50 | Mpanda MC | 0.13 | |
| | | | | Nsimbo DC | 0.43 | |
| | | | | Tanganyika DC | 0.60 | |
| | | | | Mpimbwe DC | 1.00 | |
| | | | | Mlele DC | 0.35 | |

| Na. | Aina ya Mbegu | Mkoa | Kiasi kwa Mkoa (Tani) | Halmashauri | Kiasi kwa Wilaya (Tani) | Kiasi (Tani) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | RUVUMA | 8.00 | Songea MC | 0.27 | |
| | | | | Mbinga | 0.27 | |
| | | | | Songea DC | 1.50 | |
| | | | | Namtumbo DC | 3.00 | |
| | | | | Tunduru DC | 3.00 | |
| | | TANGA | 1.36 | Handeni DC | 0.80 | |
| | | | | Handeni TC | 0.26 | |
| | | | | Pangani DC | 0.30 | |
| | | MOROGORO | 3.57 | Mlimba DC | 0.50 | |

| Na. | Aina ya Mbegu | Mkoa | Kiasi kwa Mkoa (Tani) | Halmashauri | Kiasi kwa Wilaya (Tani) | Kiasi (Tani) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Ifakara TC | 0.50 | |
| | | | | Mvomero DC | 0.50 | |
| | | | | Morogoro DC | 0.57 | |
| | | | | Kilosa DC | 0.50 | |
| | | | | Malinyi DC | 0.50 | |
| | | | | Ulanga DC | 0.50 | |
| | | MANYARA | 0.50 | Simanjiro DC | 0.50 | |
| | | SONGWE | 1.00 | Momba DC | 1.00 | |
| | | MBEYA | 1.50 | Chunya DC | 0.70 | |

| Na. | Aina ya Mbegu | Mkoa | Kiasi kwa Mkoa (Tani) | Halmashauri | Kiasi kwa Wilaya (Tani) | Kiasi (Tani) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Mbeya DC | 0.50 | |
| | | | | Kyela DC | 0.30 | |
| | | RUKWA | 0.50 | Sumbawanga DC | 0.50 | |
| | Mbaazi | SONGWE | 2.90 | Songwe DC | 1.50 | 17.34 |
| | | | | Momba DC | 1.40 | |
| | | SIMIYU | 2.60 | Bariadi TC | 0.25 | |
| | | | | Bariadi DC | 0.55 | |
| | | | | Itilima DC | 0.55 | |
| | | | | Meatu DC | 0.50 | |

| Na. | Aina ya Mbegu | Mkoa | Kiasi kwa Mkoa (Tani) | Halmashauri | Kiasi kwa Wilaya (Tani) | Kiasi (Tani) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Busega DC | 0.25 | |
| | | | | Maswa DC | 0.50 | |
| | | DODOMA | 2.50 | Chemba DC | 1.00 | |
| | | | | Kondoa DC | 1.00 | |
| | | | | Kongwa DC | 0.50 | |
| | | MANYARA | 2.74 | Kiteto DC | 1.00 | |
| | | | | Hanang' DC | 0.54 | |
| | | | | Babati DC | 1.20 | |
| | | ARUSHA | 1.60 | Karatu DC | 1.00 | |
| | | | | Meru DC | 0.22 | |
| | | | | Monduli DC | 0.23 | |
| | | | | Arusha DC | 0.15 | |
| | | KIGOMA | 1.00 | Uvinza DC | 1.00 | |
| | | NJOMBE | 0.50 | Ludewa DC | 0.50 | |
| | | TANGA | 0.31 | Handeni DC | 0.31 | |
| | | KATAVI | 0.50 | Tanganyika DC | 0.37 | |
| | | | | Mpanda MC | 0.13 | |

| Na. | Aina ya Mbegu | Mkoa | Kiasi kwa Mkoa (Tani) | Halmashauri | Kiasi kwa Wilaya (Tani) | Kiasi (Tani) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | MWANZA | 0.19 | Kwimba DC | 0.19 | |
| | | MOROGORO | 1.00 | Gairo DC | 1.00 | |
| | | RUKWA | 0.50 | Sumbawanga DC | 0.50 | |
| | | TABORA | 0.50 | Nzega DC | 0.30 | |
| | | | | Nzega TC | 0.20 | |
| | | IRINGA | 0.50 | Iringa DC | 0.25 | |
| | | | | Kilolo DC | 0.25 | |
| 4. | Choroko | Simiyu | 3.00 | Bariadi TC | 0.20 | 10.70 |
| | | | | Bariadi DC | 0.80 | |
| | | | | Itilima | 1.00 | |
| | | | | Meatu | 0.30 | |
| | | | | Busega | 0.20 | |
| | | | | Maswa | 0.50 | |
| | | SHINYANGA | 3.00 | Shinyanga MC | 0.50 | |
| | | | | Shinyanga DC | 1.20 | |
| | | | | Kishapu | 1.30 | |
| | | MWANZA | | Misungwi | 0.75 | |

| Na. | Aina ya Mbegu | Mkoa | Kiasi kwa Mkoa (Tani) | Halmashauri | Kiasi kwa Wilaya (Tani) | Kiasi (Tani) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 1.50 | Kwimba | 0.75 | |
| | | TABORA | 1.20 | Nzega | 0.20 | |
| | | | | Igunga | 1.00 | |
| | | MARA | 1.00 | Bunda DC | 0.50 | |
| | | | | Musoma DC | 0.50 | |
| | | MTWARA | 0.50 | Masasi DC | 0.25 | |
| | | | | Nanyumbu DC | 0.25 | |
| | | LINDI | 0.50 | Ruangwa | 0.25 | |
| | | | | Nachingwea | 0.25 | |
| 5. | Dengu | SINGIDA | 4.00 | Itigi DC | 1.20 | 4.00 |
| | | | | Ikungi DC | 0.50 | |
| | | | | Manyoni DC | 0.50 | |
| | | | | Mkalama DC | 0.60 | |
| | | | | Singida MC | 0.20 | |
| | | | | Singida DC | 0.50 | |
| | | | | Iramba DC | 0.50 | |
| | Soya | RUVUMA | | Madaba DC | 0.18 | 1 |

| Na. | Aina ya Mbegu | Mkoa | Kiasi kwa Mkoa (Tani) | Halmashauri | Kiasi kwa Wilaya (Tani) | Kiasi (Tani) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 6. | | | 1.00 | Mbinga DC | 0.07 | |
| | | | | Namtumbo DC | 0.30 | |
| | | | | Songea DC | 0.20 | |
| | | | | Songea MC | 0.25 | |
| 7 | Ngano | NJOMBE | 70,000.00 | Makete | 70.00 | 500.00 |
| | | KILIMANJARO | 10,000.00 | Siha | 10.00 | |
| | | MBEYA | 320,000.00 | Chunya | 320.00 | |
| | | **Jumla ya Usambazaji** | | | **400.00** | |
| | | Usambazaji Unaoendelea | | | 100.00 | |

| Na. | Aina ya Mbegu | Mkoa | Kiasi kwa Mkoa (Tani) | Halmashauri | Kiasi kwa Wilaya (Tani) | Kiasi (Tani) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Jumla Kuu** | | | **500.00** | |
| 8 | Mpunga | MOROGORO | 77,600.00 | Morogoro Mjini | 77.60 | 500.00 |
| | | RUVUMA | 15,005.00 | Namtumbo | 15.01 | |
| | | SONGWE | 13,480.00 | Mbozi | 13.48 | |
| | | TABORA | 10,000.00 | Nzega | 10.00 | |
| | | IRINGA | 5,000.00 | Kilolo | 5.00 | |
| | | NJOMBE | 4,250.00 | Njombe Mjini | 4.25 | |
| | | Jumla Ndogo | | | 125.34 | |
| | | MBEYA | 7,000.00 | Mbarali (Azimio) | 2.00 | |

| Na. | Aina ya Mbegu | Mkoa | Kiasi kwa Mkoa (Tani) | Halmashauri | Kiasi kwa Wilaya (Tani) | Kiasi (Tani) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Mbarali (Matebete) | 1.11 | |
| | | | | Mbarali (Madibira) | 1.00 | |
| | | | | Mbarali (Uturo) | 1.00 | |
| | | Jumla Ndogo | | | 5.11 | |
| | | **Jumla ya Usambazaji** | | | **130.44** | |
| | | **Usambazaji Unaoendelea** | | | **369.56** | |
| | | **Jumla Kuu** | | | **500.00** | |

**Kiambatisho Na. 2: Orodha ya viuatilifu vilivyoondolewa sokoni**

| Na. | Viuatilifu vyenye Viambata Hatarishi | Majina ya Viambata Hatarishi | Aina za athari kwa kuzingatia vigezo vya FAO/WHO JMPM |
|---|---|---|---|
| 1 | Cocrakill Paste | Boric Acid | Huathiri mfumo wa uzazi |
| 2 | Dimilin 25WP | Diflubenzuron | Athari za kusababisha saratani |
| 3 | PilarStar 200SL | Glufosinate Ammonium | Huathiri mfumo wa uzazi |
| 4 | 1) Snowron 500 WP, | Linuron | Husababisha mabadiliko ya kinasaba (jenetiki) |
| 5 | 2) Multiron 50SC, | | |
| 6 | 3) Snowron 500 WP | | |
| 7 | Benomilo 50WP | Benomyl | Huathiri mfumo wa uzazi, husababisha saratani, na husababisha mabadiliko ya vinasaba (jenetiki) |
| 8 | 1) Elcazim 50SC, | Carbendazim | Husababisha mabadiliko ya vinasaba (jenetiki) na huathiri mfumo wa uzazi. |
| 9 | 2) Pearl 500 SC, | | |
| 10 | 3) Snow Shrf 500SC, | | |
| 11 | 4) Jazz 40%WP, | | |

| Na. | Viuatilifu vyenye Viambata Hatarishi | Majina ya Viambata Hatarishi | Aina za athari kwa kuzingatia vigezo vya FAO/WHO JMPM |
|---|---|---|---|
| 12 | 5) Funco 500WP, | | |
| 13 | 6) Seed Plus 30 WS, | | |
| 14 | 7) Suprano C, | | |
| 15 | 8) Innovex 360SC, | Carbendazim | Husababisha mabadiliko ya vinasaba (jenetiki) na huathiri mfumo wa uzaz |
| 16 | 9) Seedcare, Barbendazim | | |
| 17 | 10) Plus 500SC, | | |
| 18 | 11) Pro-Carben 59.7WP, | | |
| 19 | 12) Mult-triacaRb 500SC, | | |
| 20 | 13) Bendazim 500 SC, | | |
| 21 | 14) Seedwatch 20 WS, | | |
| 22 | 15) Bavistin 500 DF, | | |
| 23 | 16) Tanzim 50 SC, | | |
| 24 | 17) Tandem 250SC, | | |

| Na. | Viuatilifu vyenye Viambata Hatarishi | Majina ya Viambata Hatarishi | Aina za athari kwa kuzingatia vigezo vya FAO/WHO JMPM |
|---|---|---|---|
| 25 | 18) Switanza 250 SC, | | |
| 26 | 19) Bendera 50 WP, | | |
| 27 | 20) Stardom 500SC, | | |
| 28 | 21) Forsol 500WP, | | |
| 29 | 22) Jazz 40% WP, | | |
| 30 | 23) Indazole 25 SC, | | |
| 31 | 24) Polestar 75 WP, | | |
| 32 | 25) Treatseed 30 WS, | | |
| 33 | 26) Power - Guard 250 SC, | | |
| 34 | 27) SEED GUARD GOLD 415 FS, | | |
| 35 | 28) TWIN 75 WP | | |
| 36 | 1) Pirastar 183SE, | Epoxiconazole | Husababisha mabadiliko ya vinasaba (jenetiki) na huathiri mfumo wa uzazi |
| 37 | 2) Swing Xtra 497SC, | | |
| 38 | 3) Swing 250SC | | |

| Na. | Viuatilifu vyenye Viambata Hatarishi | Majina ya Viambata Hatarishi | Aina za athari kwa kuzingatia vigezo vya FAO/WHO JMPM |
|---|---|---|---|
| 39 | 1) Noxtar 40EC | Flusilazole | Huathiri mfumo wa uzazi |
| 40 | 1) Molgard 25EC, | Propiconazole | Huathiri mfumo wa uzazi |
| 41 | 2) Amistar Trio 255EC, | | |
| 42 | 3) Quilt Xcel 263.8 SE, | | |
| 43 | 4) PILLARPRO 295 SE, | | |
| 44 | 5) Artea 330EC, | Propiconazole | Huathiri mfumo wa uzazi |
| 45 | 6) Sipron Star 330EC, | | |
| 46 | 7) Filia 525 SE, | | |
| 47 | 8) Tilt 250EC, Subatil 250EC, | | |
| 48 | 9) Proazole 25 EC | | |
| 49 | 1) Bajuton 250 WP, | Triadimefon | Husababisha mabadiliko ya vinasaba (jenetiki) na huathiri mfumo wa uzazi |
| 50 | 2) Innovex 360SC, | | |
| 51 | 3) Farmleton 250WP, | | |
| 52 | 4) Timefon 250 WP, | | |

| Na. | Viuatilifu vyenye Viambata Hatarishi | Majina ya Viambata Hatarishi | Aina za athari kwa kuzingatia vigezo vya FAO/WHO JMPM |
|---|---|---|---|
| 53 | 5) Evermefon 25WP, | | |
| 54 | 6) Agtrol 250WP | | |
| 55 | 7) Metax 450WP, | | |
| 56 | 8) Trical 250 EC, | | |
| 57 | 9) Falfone 25WP, | | |
| 58 | 10) Sevenmefon 25WP, | | |
| 59 | 11) Bayleton 25 WP | | |
| 60 | 1) Badimenol 250EC, | Triadimenol | Huathiri mfumo wa uzazi |
| 61 | 2) Voltriad 25% EC, | | |
| 62 | 3) Agromenol 250 EC, | | |
| 63 | 4) Pacha 500 SC, | | |
| 64 | 5) Bayfidan 250 EC, | | |

| Na. | Viuatilifu vyenye Viambata Hatarishi | Majina ya Viambata Hatarishi | Aina za athari kwa kuzingatia vigezo vya FAO/WHO JMPM |
